# Nipashe

Ijumaa Aprili 12, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579890

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz ...ppmedia.com ...com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US





## HOMA YA DENGUE

UGONJWA wa homa ya dengue umeingia na kuenea katika mikoa ya Dar es Salaam na Tanga na hadi sasa zaidi...

UKURASA 3



## MAHAKIMU WAAGIZWA

JAJI Kiongozi, Dk. Eliezer Feleshi, ametoa maagizo mazito kwa viongozi wa mahakama wanaotafsiri haki na sheria...

UKURASA 21

UKURASA 13

# CAG abaini ufisadi polisi

• **Ni** ule wa magari 777 yaliyoagizwa uchaguzi mkuu uliopita, ataka uchunguzi posho za vigogo wa taasisi za serikali... *Endelea ukurasa 2*

## Usafiri wa DART kuenea kila kona DSM



UKURASA 3



UKURASA 2

Rais John Magufuli akiwasalimia wananchi wa Makambako, baada ya kuwasili katika eneo la viwanja vya Polisi Makambako, mkoani Njombe jana. **PICHA: IKULU**

# Kijana aibua kashfa nzito mbele ya JPM


SPECIAL FEATURE ON INDUSTRIALIZATION DEVELOPMENT IN TANZANIA

"NCHI YA VIWANDA"





The Guardian Ltd, through its Leading Newspapers, The Guardian and Nipashe in collaboration with CTI will publish special supplement focusing on Industrialization Development in Tanzania, phase one on 18th April 2019.

We are inviting The Government and Private Institutions to participate in this special feature.

Contact:

Moses Masunga,
Email:moses.masunga@guardian.co.tz,
Phone No.0755 642851,

Charles Masele,
Email:masele7@gmail.com,
Phone No.0789 637363.

The Guardian Nipashe CTI

HABARI KITAIFA

## ...Aagiza uchunguzi posho za vigogo

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, ameitaka Ofisi ya Msajili wa Hazina ichunguze posho zote zinazolipwa katika taasisi mbalimbali za umma baada ya kubaini uwapo wa vigogo wanaolipana posho kinyume cha taratibu.

Amesema amebaini wapo vigogo wa taasisi za umma wanaolipana posho kubwa kinyume cha Waraka Namba Moja wa Mwaka 2010 uliotolewa na Msajili wa Hazina.

Prof. Assad amefichua changamoto hiyo katika Ripoti Kuu ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2017/18 iliyowasilishwa bungeni juzi.

Katika ripoti hiyo, CAG Assad anabainisha wakuu wa taasisi, wakurugenzi, wakuu wa vitengo na viongozi wenye ngazi ya mshahara ya PUTS/PHTS/PGMS/PRSS 18-21 wanavyolipana posho ambazo zimefikia asilimia 40 ya mishahara yao.

Akifafanua zaidi kuhusu changamoto hiyo, Prof. Assad anabainisha kuwa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) limeingia gharama ya Sh. bilioni 1.6 kulipa posho za nyumba.

Hata hivyo, mtaalamu huyo wa ukaguzi wa hesabu anabainisha kuwa kiasi hicho kimelipwa kwa watumishi wasiostahili, wakiwamo watumishi wa mkataba na wanafunzi, kinyume cha Waraka wa Msajili wa Hazina na miongozo ya TBS kuhusu posho ya nyumba.

Anabainisha kuwa Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mkoa wa Dar es Salaam (Dawasa), imelipa Sh. milioni 276.23 kama posho ya nyumba, ikiwa ni asilimia 15 ya mshahara kwa wafanyakazi wote, bila kujali nafasi zao, kitendo ambacho ni kinyume cha Waraka wa Hazina.

# CAG aibua ufisadi polisi

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

RIPOTI ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18, imefichua 'madudu' katika ununuzi wa magari 777 uliofanywa na Jeshi la Polisi.

Katika ripoti hiyo iliyowasilishwa bungeni juzi, CAG Prof. Mussa Assad, anabainisha kuwa ukaguzi maalum wa ununuzi wa magari hayo aina ya Ashok Leyland, ulifanywa na Jeshi la Polisi nchini kwa ajili ya uchaguzi mkuu uliopita.

"Nilibaini kuwa hadi kufikia mwezi Desemba 2018, gharama za kujitolea ya mkopo (commitment charges) ya Dola za Kimarekani 287,087.17 (Sh. milioni 642.257) zilizalishwa kwenye mkopo ambao haujatumiwa na serikali.

"Hakuna ushahidi uliowasilishwa kuthibitisha kama mahitaji ya magari haya yaliibuliwa na mtumiaji. Pia, nilibaini Ashok Leyland hakuwa na uwezo wa kuleta magari yote kwani kati ya magari 777, ni magari 507 (asilimia 65) yenye gharama ya Dola za Marekani 25,498,100 ndiyo yalitoka kwake.

"Magari 270 yaliyobakia (asilimia 35) yenye gharama ya Dola za Kimarekani 4,103,000 yaliagizwa kutoka kampuni ya Great Wall Motors (mtengenezaji kutoka China)," Prof. Assad anabainisha katika ripoti yake ya ukaguzi maalum.

Anabainisha kuwa mikataba yote iliyotiwa saini haikuwa na jedwali la uletaji magari (delivery schedule) na muda wa mkataba haukuonyeshwa wazi kwenye mkataba wa awali, nyongeza na mwisho.

Anasema alibaini magari 497 yaliletwa bila ya kuwapo kwa taarifa ya ukaguzi kutoka kwa mtengenezaji. Hivyo, hakuna uhakika kama magari hayo yalikaguliwa kabla ya kuwasili kwenye Bandari ya Dar es Salaam.

Anasema alibaini kabrasha la zabuni na barua ya mwaliko vilitumwa kwa mzabuni kabla ya mkopo kuidhinishwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

"Pia, nilibaini magari yote yalikaguliwa na Wakala wa Ufundi na Umeme (Temesa), lakini magari 181 yenye thamani ya Dola za Marekani 7,447,428 yalikuwa na hitilafu.

"Shehena hiyo haikutoa uhakika kama magari ni mapya au la. Pia, nilibaini magari 22 yenye thamani ya Dola za Kimarekani 572,506 yalikuwa na kasoro, na hayakupokewa na Jeshi la Polisi.

"Pia, nilibaini kuwa magari 497 yalitolewa bandarini bila ya hati ya kutolea mizigo (release order) toka Idara ya Forodha na Ushuru, kinyume cha taratibu za Idara ya Forodha na Ushuru CED-702-F.

"Hii pia ilisababisha taratibu za bandari kukiukwa na kusababisha madeni ya kodi na ada ya jumla ya Sh. bilioni 6.858 na Sh. bilioni 1.217 toka Mamlaka ya Mapato (TRA) na Mamlaka ya Bandari zikiwa ni kodi (Kodi ya Ongezeko la Thamani -VAT na tozo za bandari na ada za bandari (gharama za hifadhi na ubebaji), mtawalia. Fedha hizi zilikuwa hazijalipwa na Jeshi la Polisi hadi muda wa ukaguzi mwezi Februari 2019," Prof. Assad anabainisha katika ripoti yake hiyo.

CAG pia anabainisha kuwa ukaguzi wake katika mfumo wa forodha na mfumo wa utoaji wa mzigo TRA Mamlaka ya Bandari (TPA) umethibitisha magari yaliyotolewa bado yapo chini ya miliki ya forodha licha ya kuwa yameondolewa kutoka Bandari ya Dar es Salaam.

"Ununuzi wa magari 777 ulilenga yatumike wakati wa Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba 2015. Hata hivyo, nilibaini magari 104 tu kati ya 777 yaliletwa hadi kufikia mwezi Oktoba 2015.

"Magari mengine 393 yaliletwa kati ya Aprili 2016 na Mei 2018. Hadi kufikia Desemba 2018, nilibaini magari 280 yalikuwa bado hayajaletwa na Mzabuni Ashok Leyland.

"Kutokana na upungufu wa magari, mnamo mwezi Septemba 2015, Jeshi la Polisi lilipatiwa fedha za ziada jumla ya Sh. bilioni 42.931 ili kununua magari mengine 276 ili kufuta upungufu uliokuwapo hadi kufikia Oktoba 2015.

"Hivyo, nimebaini hakuna tija yoyote ya mkopo huu kwa serikali. Ununuzi wa magari haya ya Ashok Leyland ulikuwa ni wa gharama kubwa, isiyokuwa na tija na ufanisi," Prof. Assad anaeleza katika ripoti hiyo.

Anasema malengo yaliyokusudiwa hayakupatikana na anapendekeza magari 22 yenye thamani ya Dola za Marekani 572,506 yaliyopatikana na kasoro na kukataliwa na Jeshi la Polisi yabadilishwe.

Pia anapendekeza magari 280 yenye thamani ya Dola za Marekani 6,759,648 na vipuri vya thamani ya Dola za Marekani 5,510,429 viletwe mara moja ili kuepuka ongezeka la gharama za kujitolea (commitment charges) za mkopo wa Dola za Marekani 13, 477,570,30 ambao haujatumika.

"Ninahimiza serikali daima kuchambua mikopo yote kwa ufanisi na kuachana na mikopo yenye masharti ya kibiashara ambayo inaonekana kuwa ya gharama kubwa.

"Zaidi, ninahimiza Kamati za Usimamizi wa Madeni za Kitaifa kufanya kazi kitaaluma na kutekeleza taratibu zote kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mikopo ya Serikali, Dhamana na Ruzuku ya Mwaka 1974 (marekebisho ya mwaka 2003) na Kanuni zake," CAG Assad anasema katika ripoti yake hiyo.




# Kijana aibua kashfa nzito mbele ya JPM

**Na Romana Mallya**

KIJANA Albert, mkazi wa Makambako mkoani Njombe, ameibuka shujaa kwenye mkutano wa Rais John Magufuli baada ya kuibua kashfa ya mradi wa maji iliyowapa wakati mgumu Mhandisi wa Maji na Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo. Kijana huyo alifika kwenye mkutano huo ambao Rais Magufuli alikuwa kwenye uzinduzi wa barabara ya Mafinga-Nyigo-Igawa yenye urefu wa kilometa 138.7.

Uzinduzi huo uliofanyika eneo la Mtewele kwenye uwanja wa polisi, Makambako, ambako kijana huyo ambaye alikuwa na bango baada ya kubughudhiwa na polisi ndipo Rais Magufuli alipomuita mbele na bango lake ili kuelezea kero aliyonayo.

Alipofika mbele ya Rais Magufuli, Albert alimweleza kuwa eneo la Manga anakotoka halina maji kwa muda mrefu na viongozi wamekuwa na kawaida ya kutoa maji kila wanapofika viongozi wa kitaifa.

"Nakushukuru Rais kwa kuja, wewe ni Rais wa wanyonge sisi tunaumia tangu 2009, hatupati maji kila siku wageni wakija wanaweka maji, wakiondoka wanakata, sasa hivi tuna miezi zaidi ya sita hatujapata maji, ulivyoahidi kuja matengenezo yakafanyika wiki iliyopita, tunaomba utusaidie wanyonge," alisema.

Baada ya maelezo hayo Rais Magufuli alimwita meneja au mkurugenzi ili aende kueleza kwa nini viongozi wakienda huko ndipo maji yanapatikana na wakiondoka yanakatwa. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Makambako akizungumzia kuhusu suala hilo, alikiri kuwa mradi huo wa Manga una matatizo siku nyingi.

"Nimehamia hapa mwaka 2016 nikaukuta mradi umekamilika, lakini ulikuwa na matatizo kwenye usanifu wake, kuna eneo la takribani kilomita 1.6 ndilo linalosumbua, lakini tumewasiliana na mkoa na mhandisi wa maji alitutaka tulipitie eneo hilo ili tuweze kubaini tatizo," alisema.

Alisema baada ya kupitiwa lilionekana kuna changamoto ya mabomba na waliwasiliana na Wizara ya Maji, na kuwa wiki mbili zilizopita mhandisi wa maji wa wizara ni alifika na kuwataka waandike tatizo hilo kimaandishi ili asaidie. "Mara kwa mara kuna kupasuka kwa mabomba na viungio vyake, tatizo hili hata Mkuu wa Mkoa alishafika, siyo kwamba yanapasuka wakati Rais akija, mara kwa mara kuna usumbufu, hayachukui wiki mbili yanaleta shida, mradi ulighariumu Sh. bilioni 1.40," alisema.

Mkandarasi aliyejitaja kwa jina moja la Malisa naye alisema mradi huo ulisainiwa mwaka 2009 wakati huo halmashauri haikuwapo Makambako.

"Mradi wa awali uliosainiwa ulikuwa ni wa Sh. milioni 467, Mtaalamu Mshauri tuliyemkuta alitoa mapendekezo kubadilishwe kwa sababu kina cha maji kilikauka na kusababisha mradi uende kilometa 15 zaidi huko Wilaya ya Njombe kutoka ulikokuwa awali," alisema.

Alisema walipoingia kwenye mkataba, mradi ulikuwa umeshaanza na walipohama kilometa na gharama ziliongezeka kutoka Sh. milioni 467 hadi Sh. bilioni 1.40.

Kitendo cha albert kuibua sakata hilo kilimkuna Rais Magufuli ambaye alimpongeza kwa ujasiri wa kuwasemea wananchi wenzake kuhusu kero

INAENDELEA UK. 8

**HABARI KITAIFA**

# Watu 307 waugua dengue Dar es Salaam, Tanga

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imekiri kuwapo na ugonjwa wa dengue nchini kwenye majiji ya Dar es Salaam na Tanga na hadi sasa watu 307 wamethibitishwa kuwa na virusi vya homa hiyo.

Kufuatia hali hiyo, wananchi watakaopata dalili za ugonjwa huo wametahadharishwa kutotumia dawa ya kutuliza maumivu aina ya Diclopar, Brufen na Ibuprofen.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri, Dk. Faustine Ndugulile, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ugonjwa wa homa ya dengue nchini.

Alisema kuanzia Januari mwaka huu, ugonjwa huo umeibuka tena na kuendelea kuthibitishwa kuwapo hapa nchini hususan kwenye majiji hayo.

Dk. Ndugulile alisema dalili za ugonjwa huo huanza kujitokeza kati ya siku ya tatu hadi 14 tangu alipoambukizwa virusi vya homa ya dengue na mbu aina ya Aedes.

“Wakati mwingine zinaweza kufanana na za malaria hizi dalili, hadi Aprili 2, mwaka huu, kati ya watu 470 waliopimwa, wagonjwa 307 wamethibitishwa kuwa na virusi au walikwishapata ugonjwa huo na kati ya hao 252 ni kutoka Dar es Salaam na 55 ni kutoka Tanga,” alisema.

Alifafanua kuwa katika Jiji la Dar es Salaam wagonjwa wamethibitisha katika Hospitali za Mwananyamala, Ilala, Temeke, Vijibweni, Aga-Khan, Regency, IST na Ebrahim Haji.

Aidha, alisema kutoka Jiji la Tanga wagonjwa wamethibitisha katika Hospitali za Bombo, Aga-Khan, Burhani Street 4 na Safi Medics.

Alieleza kuwa ugonjwa wa homa ya dengue si mpya hapa nchini kwa kuwa umewahi kuripotiwa miaka ya 2010, 2013, 2014 na 2018 hasa ikizingatiwa uwapo wa mbu aenezae ugonjwa huo.

Aliwaasa wananchi kuwa makini kipindi wapatapo homa na wahakikishe wanakwenda kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya, ili waweze kupimwa na kupatiwa tiba sahihi.

Alieleza kuwa mbu huyo huwa ana tabia ya kuuma zaidi wakati wa mchana hasa asubuhi jua linapochomoza na jioni linapozama, huku akiasa wananchi kuwa na tabia ya kuvaa nguo za kuficha viungo vya mwili.

Alisema ugonjwa huo hauenezwi kutoka kwa binadamu mmoja kwenda kwa mwingine bila ya kuumwa na mbu mwenye vimelea.

Alisema hadi sasa hakuna chanjo ya homa dengue nchini wala tiba ya moja kwa moja ya ugonjwa huo.

“Mgonjwa mwenye homa hutibiwa kutokana na dalili zitakazoambatana na ugonjwa huo kama vile kupungukiwa maji au damu,” alisema.

Alisema hatua ambazo zimechukuliwa hadi sasa ni kupulizia dawa ya kuua mbu katika mazingira ya Jiji la Dar es Salaam, kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa ugonjwa uliopo kwenye vituo maalum Mkoa wa Dar es Salaam katika Hospitali za Mwananyamala, Ilala na Temeke.

INAENDELEA UK. 8

# Neema nyingine mwendokasi Dar

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAKALA wa Mabasi Yaendayo Haraka jijini Dar es Salaam (DART), umeanza maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya tatu ya mradi huo, ambao mabasi yake yatakwenda hadi Gongo la Mboto kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA).

Akiwasilisha bungeni mapitio, makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2019/20, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, alisema utekelezaji huo utahusisha barabara ya Azikiwe na Maktaba.

Pia alisema Barabara ya Bibi Titi na Nyerere kupitia JNIA hadi Gongo la Mboto, kituo kikuu cha mabasi Kariakoo Gerezani kupitia Mtaa wa Lindi, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi Tazara zenye urefu wa kilometa 23.6. “Serikali imetoa eneo la Gongo la Mboto kwa ajili ya ujenzi wa karakana ya mabasi, eneo ndani ya JNIA kwa ajili ya kujenga kituo cha mabasi kuunganisha uwanja huo na huduma ya mabasi,” alisema.

Alisema pia eneo la kujenga kituo mlisho cha Banana karibu na eneo zilizopo ofisi za TCAA na wananchi wapatao 78 wanaoguswa na mradi mali zao zimethaminiwa kwa ajili ya kulipwa fidia.

Kadhalika, alisema mwaka 2019/20 itafanyika tathmini ya gharama za kuhamisha miundombinu ya kijamii na fidia kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa mradi huo awamu ya nne.

“Awamu ya nne itahusisha barabara za Bagamoyo hadi Tegeta, Bibi Titi, Ali Hassan Mwinyi na Sam Nujoma zenye urefu wa kilometa 25.9 na awamu ya tano itahusisha ujenzi wa barabara za Mandela kuanzia eneo la Ubungo kupitia Tazara, Uhasibu kuungana na barabara ya Kigamboni na barabara ya kuanzia Tabata Relini hadi Segerea,” alisema.

Akizungumzia awamu ya pili, Jafo alisema wakala huo umekamilisha maandalizi ya utekelezaji wa awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu itakayohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang’ombe yenye urefu wa kilometa 20.3.

Alisema mradi huo utahusisha pia ujenzi wa barabara za juu (flyovers) katika makutano ya Chang’ombe na Uhasibu. “Utekelezaji wa mradi huo unafanyika kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB),” alisema.

Waziri Jafo alisema wananchi na taasisi 90 kati ya 105 wamelipwa fidia ya Sh. bilioni 28.52 kati ya Sh. bilioni 34.19 zilizopangwa kulipwa ili kupisha utekelezaji wa mradi.


**NATIONAL ENVIRONMENT MANAGEMENT COUNCIL (NEMC)**
**BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**TAARIFA KWA UMMA**

**MKUTANO WA WADAU KUHUSU USIMAMIZI NA UDHIBITI WATAKA HATARISHI**

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) linawatangazia wadau wote wanaofanya biashara ya Taka hatarishi (zenye madhara)-harzadous waste, kuwa, utakuwapo mkutano wa wadau siku ya JumapiliTtarehe 14/ 04/2019 kuzungumzia na kujadili suala la usimamizi na udhibiti wa taka hizi hatarishi kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja.

Mkutano huu utafanyika katika ukumbi wa LAPF (Millennium Tower) Makumbusho, Jijini Dar es Salaam kuanzia saa 4.00 kamili asubuhi, wadau wote ikiwa ni pamoja na wakusanyaji , wanunuaji, wauzaji, wanaoingiza nchini ama kusafirishaji nje ya nchi, warejereshaji na wateketezaji taka hizo, mnaalikwa na mnaombwa kuhudhuria mkutano huu muhimu. Mamlaka mbalimbali za serikali zinazoshughulika na suala hili la Taka hatarishi pia zimealikwa. Mgeni rasmi atakuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mhe.January Makamba (Mb)

Taka hatarishi (zenye madhara)-harzadous waste ni pamoja na vyuma chakavu, taka za kieletroniki, dutu hatarishi, mafuta machafu, taka za hospitali, Betri na Tairi zilizotumika na aina ya taka zote zinazotoka migodini. Taka hizi hatarishi zinaweza kusababisha athari mbaya kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira. Ili kuzuia na kudhibiti athari mbaya zitokanazo na taka zenye madhara, mfumo mahsusi unaofanya kazi kwa ufanisi wa kudhibiti taka hizi unapaswa ufuatwe kama ulivyobainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009.

Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu mazingira nchini kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, 2004 na Kanuni zake. Aidha, usimamizi na udhibiti wa taka zenye madhara umebainishwa kwenye Vifungu vya 133 -139 vya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2004. Pia Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Taka za Sumu) za Mwaka 2009 zimetoa miongozo ya kudhibiti taka sumu hapa nchini pamoja na mambo mengine yahusuyo uhifadhi wa mazingira.

Katika mkutano huo, mada inayohusu utaratibu wa kisheria kuhusu usimamizi wa taka hatarishi na changamoto zake itawasilishwa na wadau watapata fursa ya kuchangia maoni juu ya masuala ya ukusanyaji, usafirishaji, urejereshaji na uteketezaji wa taka hatarishi ili kufikia uelewa wa pamoja juu ya suala hili.

**Taarifa hii imetolewa na:**

**Mkurugenzi Mkuu ,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC)**

**Na kusambazwa na:**
**Kitengo cha Habari,Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma,**
**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**
**Plot No. 28, 29 &30-35 Regent Street, P.O. Box 63154, Dar es Salaam.**
**Simu: +255 22 2774889, Direct line: +255 22 2774852**
**Mobile: 0713 608930/ 0692108566**
**Fax: +255 22 2774901, Email: dg@nemc.or.tz**

215770002

# CITIBANK TANZANIA LIMITED

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

| | 2018 TZS '000 | 2017 TZS '000 |
|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 28,766,540 | 37,917,849 |
| Gharama za Riba | (4,766,002) | (7,640,034) |
| **Mapato Halisi ya Riba** | 24,000,538 | 30,277,815 |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 437,635 | 172,191 |
| **Mapato Halisi ya Riba baada ya Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo** | 24,438,173 | 30,450,006 |
| Ada na Kamisheni | 9,841,675 | 7,406,116 |
| Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 9,792,157 | 10,682,663 |
| Mishahara na Mafao | (8,980,564) | (9,260,646) |
| Gharama za kiutawala | (17,580,981) | (17,203,665) |
| Uchakavu wa Mali | (182,007) | (959,570) |
| **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | 17,328,663 | 21,114,904 |
| Tengo la Kodi ya Mapato | (5,267,883) | (6,012,756) |
| **Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | 12,060,780 | 15,102,148 |
| **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa** | | |
| – Mapato ambayo hayajakamilika | (2,672,864) | 3,143,134 |
| – Tengo la Kodi ya mapato ambayo hayajakamilika | 801,859 | (942,940) |
| Mapato mengine baada ya kodi ya mapato | (1,871,005) | 2,200,194 |
| **Jumla ya Faida Iliyojumuishwa** | 10,189,775 | 17,302,342 |

| VIASHIRIO VYA UFANISI | 2018 | 2017 |
|---|---|---|
| Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Fedha za Wanahisa | 11.46% | 11.35% |
| Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Mali | 1.31% | 2.34% |
| Uwiano wa gharama na mapato | 61.29% | 56.70% |
| Uwiano wa mapato halisi ya riba kwa mali zinazozalisha | 3.33% | 6.75% |
| Uwiano wa Mapato yasiyo ya riba kwa Pato | 45.00% | 37.40% |
| Uwiano wa Mikopo kwa amana za wateja | 23.00% | 35.13% |
| Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 0.00% | 0.10% |
| Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 77.99% | 69.68% |
| Ongezeko la Mali | 43.33% | 0.61% |
| Ongezeko la Mikopo Halisi kwa wateja | 8.20% | (19.23%) |
| Ongezeko la Amana za wateja | 65.23% | 5.88% |

### WARAKA MIZANIA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

| | 2018 TZS '000 | 2017 TZS '000 |
|---|---|---|
| **MALI** | | |
| Fedha Taslimu na Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 155,164,014 | 150,966,547 |
| Mikopo Halisi kwa benki | 386,481,802 | 112,697,947 |
| Mikopo Halisi kwa wateja | 177,825,515 | 164,355,829 |
| Miamala ya Kushughulikiwa | 221,747 | 82,016 |
| Malipo ya kodi yanayotarajiwa baadae | 3,456,453 | 2,500,123 |
| Uwekezaji katika amana | 155,963,097 | 171,812,068 |
| Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 9,120,931 | 7,046,398 |
| Mali Nyingine | 35,261,525 | 34,797,800 |
| **JUMLA YA MALI** | 923,477,084 | 644,157,727 |
| **DHIMA** | | |
| Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 1,781,370 | 565,244 |
| Amana za Wateja | 773,030,346 | 467,843,919 |
| Dhima Nyingine | 43,264,579 | 42,458,724 |
| Dhima ya kodi ya kampuni | 151,948 | 280,785 |
| **JUMLA YA DHIMA** | 818,228,243 | 511,148,672 |
| **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 9,659,900 | 9,659,900 |
| Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,147,556 | 3,018,561 |
| Mapato Yaliyobakizwa | 92,054,612 | 118,804,894 |
| Tengo la ziada ya jumla | 2,386,773 | 1,525,700 |
| Tengo la ziada ya kisheria | - | - |
| **Jumla ya fedha za wanahisa** | 105,248,841 | 133,009,055 |
| **Jumla ya fedha za wanahisa na dhima** | 923,477,084 | 644,157,727 |

Taarifa hizi ziliptishwa na Bodi ya Wakurugenzi tarehe 28 Machi 2019 na kutiwa saini kwa niaba yake na:

Joseph Carasso
**Ofisa Mtendaji Mkuu**

Iddi Msonga
**Mkuu wa Fedha**

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2014, na zinaonesha hali halisi.

Godwin Rutashobya
**Mkaguzi Mkuu wa Ndani**

Emilian Busara
**Mshirika Mkurugenzi Mtendaji**

Yande Panya
**Mshirika Mkurugenzi Mtendaji**

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

| | 2018 TZS'000 | 2017 TZS'000 |
|---|---|---|
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Faida ya Uendeshaji | 17,328,663 | 21,114,904 |
| *Marekebisho kwa Ajili ya:* | | |
| Uchakavu wa Mali | 182,007 | 959,570 |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa - mali | 32,260 | (24,882) |
| Faida/(hasara) ya mapato mengine yaliyojumuishwa - dhima | (13,520) | (143,264) |
| Mapato Halisi ya Riba | (24,000,538) | (30,277,815) |
| | (6,471,128) | (8,357,812) |
| **Mabadiliko katika shughuli za uendeshaji wa mali na madeni** | | |
| Mikopo Halisi kwa wateja | (14,109,460) | 39,135,140 |
| Mikopo Halisi kwa benki | 1,216,126 | (10,075,488) |
| Uwekezaji wa amana | 13,186,108 | (16,542,666) |
| Hifadhi ya chini ya kisheria | (13,060,325) | 2,490,713 |
| Mali Nyingine | (485,985) | 2,900,568 |
| Amana za Wateja | 305,186,427 | 25,976,759 |
| Dhima Nyingine | 819,375 | (8,134,930) |
| **Fedha iliyozalishwa kutokana na shughuli za uendeshaji** | 286,281,137 | 28,392,282 |
| Riba iliyopokelewa | 28,766,540 | 37,917,849 |
| Riba iliyolipwa | (4,766,002) | (7,640,034) |
| Kodi iliyolipwa | (5,361,259) | (8,355,146) |
| **Fedha Halisi zilizotumika kwa shughuli za uendeshaji** | 304,920,416 | 50,314,951 |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji** | | |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (2,256,541) | (6,272,625) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | 12,291 |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji** | (2,256,540) | (6,260,334) |
| **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha** | | |
| Gawio lililolipwa | (37,502,148) | (20,287,745) |
| **Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Kifedha** | (37,502,148) | (20,287,745) |
| | 217,322,863 | 193,555,991 |
| Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji | 304,920,416 | 50,314,951 |
| Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Uwekezaji | (2,256,540) | (6,260,334) |
| Fedha Halisi Zilizotumika kwa Shughuli za Kifedha | (37,502,148) | (20,287,745) |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka** | 482,484,590 | 217,322,863 |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DESEMBA 2018

| | Mtaji wa Hisa | Akaunti nyingine za mtaji | Mapato Yaliyobakizwa | Tengo la ziada ya jumla | Tengo la ziada ya kisheria | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka uliokwisha 31 Desemba 2018** | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 |
| Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2018 | 9,659,900 | 3,018,561 | 118,804,894 | 1,525,700 | - | 133,009,055 |
| Mabadiliko juu ya matumizi ya awali ya IFRS 9 | - | - | (447,841) | - | - | (447,841) |
| **Salio lililorekebishwa tarehe 1 Januari 2018** | 9,659,900 | 3,018,561 | 118,357,053 | 1,525,700 | | 132,561,214 |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 12,060,780 | - | - | 12,060,780 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | (1,871,005) | - | - | - | (1,871,005) |
| Jumla ya Faida Iliyojumuishwa kwa mwaka | - | (1,871,005) | 12,060,780 | - | - | 10,189,775 |
| Miamala na wanahisa | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | - | - | (37,502,148) | - | - | (37,502,148) |
| Hamisho la ziada ya kisheria | - | - | (861,073) | 861,073 | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2018** | 9,659,900 | 1,147,556 | 92,054,612 | 2,386,773 | - | 105,248,841 |
| **Mwaka Uliokwisha 31 Desemba 2017** | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka 1 Januari 2017 | 9,659,900 | 818,367 | 123,299,153 | 1,770,501 | 437,447 | 135,994,468 |
| Faida Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 15,102,148 | - | - | 15,102,147 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | 2,200,194 | - | - | - | 2,200,194 |
| Jumla ya Faida Iliyojumuishwa | - | 2,200,194 | 15,102,148 | - | - | 17,302,341 |
| Miamala na wanahisa | | | | | | |
| Gawio lililolipwa | - | - | (20,287,745) | - | - | (20,287,745) |
| Kutolewa kwa tengo la ziada ya kisheria | - | - | 437,447 | - | (437,447) | - |
| Kutolewa kwa tengo la ziada ya jumla | - | - | 253,801 | (253,801) | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31 Desemba 2017** | 9,659,900 | 3,018,561 | 118,804,894 | 1,525,700 | - | 133,009,055 |

citi®

215172302

# TANGAZO

# UNITED BANK FOR AFRICA (TANZANIA) LIMITED

UBA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA 2018

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31-DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|---|
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 1,844 | 2,457 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 4,879 | 2,794 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 41,308 | 34,584 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 2,017 | 9,098 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | - |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 40,347 | 32,626 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 34,677 | 35,489 |
| 12 | Mali Nyingine | 4,146 | 4,957 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,203 | 966 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **130,420** | **122,972** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 44,553 | 41,898 |
| 18 | Amana za Wateja | 44,455 | 31,540 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 8,757 | 6,258 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 265 | 9 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 1,225 | 2,587 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 857 | 322 |
| 27 | Dhima Nyingine | 1,363 | 1,843 |
| 28 | Madeni | 10,587 | 17,092 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **112,063** | **101,551** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **18,358** | **21,421** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 31,420 | 31,420 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 29,104 | 29,104 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | - | - |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | (39,521) | (33,649) |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | (3,048) | (5,805) |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 402 | 351 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **18,358** | **21,421** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | - | - |
| 39 | Mikopo Chechefu | 1,526 | 2,146 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 1,526 | 2,195 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 14.1% | 16.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 4.4% | 5.7% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 65.5% | 99.7% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 26.6% | 27.9% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 89.2% | 80.7% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 40.8% | -18.0% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 6.1% | 24.0% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Limbikizo la Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-17 |
|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 10,097 | 13,338 |
| Gharama za Riba | (4,839) | (8,920) |
| **Mapato Halisi ya Riba (1 kutoa 2)** | **5,258** | **4,418** |
| Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (434) | (517) |
| **Mapato Yasiyo ya Riba:** | **3,501** | **3,464** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 845 | 448 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 2,122 | 2,360 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | 534 | 656 |
| **Gharama Zisizo za Riba:** | **(14,103)** | **(10,715)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (4,885) | (4,185) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | (9,218) | (6,530) |
| **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(5,779)** | **(3,349)** |
| Tengo la Kodi ya Mapato | - | - |
| **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(5,779)** | **(3,349)** |
| **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | (26) | - |
| **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(5,805)** | **(3,349)** |
| Idadi ya Waajiriwa | 85 | 85 |
| Mapato kwa Hisa | (924) | (1,976) |
| **Idadi ya Matawi** | 4 | 3 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -5.09% | -7.69% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -31.01% | -75.48% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 103.72% | 63.77% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.45% | 3.56% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Limbikizo la Mwaka ya sasa 31-Dec-18 | Limbikizo la Mwaka linganishi 31-Dec-17 |
|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | **(5,779)** | **(3,349)** |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| - Hasara Katika Mali | 244 | 517 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo iliyoharibika | 434 | 285 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | (4,418) |
| - Mabadiliko Halisi ya riba | (5,258) | 2 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (0) | 2,183 |
| - hasara ya mabadilisho ya mkopo | 630 | - |
| - Kodi Iliyolipwa | (24) | (26) |
| - hasara ya mabadilisho ya mtaji | | 1 |
| **II. Mabadiliko ya mtaji wa kazi** | | |
| - Badiliko Halisi Katika amana iliyobakizwa | 2,243 | 1,903 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 6,267 | 76,714 |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya serikali | (2,179) | 339 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (2,120) | (854) |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya bank zingine | 24,647 | (7,573) |
| - Badiliko Halisi Katika amana ya mteja | (8,121) | (11,011) |
| -Riba iliyopokewa | 9,662 | 9,173 |
| -Riba iliyolipwa | (4,920) | (8,364) |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 2,086 | 1,155 |
| *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **17,814** | **56,677** |
| **II. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (13) | (2) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | (593) | (336) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 2 | 2 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **(604)** | **(336)** |
| ***III. Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:*** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | (6,726) | (62,461) |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 11,205 | 10,962 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | (1,520) |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha*** | **4,479** | **(53,019)** |
| IV. Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu: | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **21,689** | **3,322** |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Mwaka | 22,452 | 19,130 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Mwaka | **44,141** | **22,452** |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la ziada ya jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka wa sasa 2018 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,454) | - | 351 | - | 21,421 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | - | - | - | - | - |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | (3,048) | - | - | - | (3,048) |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | (51) | - | - | - | (51) |
| Mengineyo | - | - | (16) | - | 51 | - | 35 |
| Share issued | - | - | - | - | - | - | - |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (42,568) | - | 402 | - | 18,358 |
| Mwaka uliopita 2017 | | | | | | | |
| Salio la mwanzo wa mwaka | 28,125 | 21,194 | (33,995) | 290 | 407 | - | 16,021 |
| Faida/(Hasara) Halisi baada ya kodi ya mapato | - | - | (5,805) | - | - | - | (5,805) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | 3,296 | 7,909 | - | - | - | - | 11,205 |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya kisheria | - | - | 290 | (290) | - | - | - |
| Tengo la ziada ya jumla | - | - | 56 | - | (56) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| Share issued | - | - | - | - | - | | |
| Salio la mwisho wa mwaka | 31,420 | 29,104 | (39,454) | - | 351 | - | 21,421 |

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | |
|---|---|---|---|
| 1 | 1 .Isiaka Usman<br>**Ofisa Mtendaji Mkuu** | *Imesainiwa* | *12th April, 2019* |
| 2 | Chomete Hussein<br>**Mkuu wa Fedha** | *Imesainiwa* | *12th April, 2019* |
| 3 | Joseph Ringa<br>**Mkaguzi Mkuu wa Ndani** | *Imesainiwa* | *12th April, 2019* |

Katika kuanda taarifa za hizi za fedha, sera za uandaaji ni zilizile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita (kama kulikuwa na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha robo mwaka ya/mwaka wa sasa, mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8).

| | ***Jina na Cheo*** | ***Saini*** | |
|---|---|---|---|
| 1 | 1. Farhiya Hersi Warsame<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *12th April, 2019* |
| 2 | 2. Emeke Iweriebor<br>**Mkurugenzi** | *Imesainiwa* | *12th April, 2019* |

United Bank for Africa (T) Ltd is a subsidiary of United Bank for Africa Plc, a leading Pan African bank offering universal banking to more than 13 million customers in over 1000 branches and outlets in Africa, USA and Europe.

**East & South Africa**
- Tanzania
- Kenya
- Congo DRC
- Mozambique
- Uganda
- Zambia

**Central Africa**
- Cameroon
- Gabon
- Chad
- Congo Brazzaville

**West Africa**
- Ghana
- Benin
- Burkina Faso
- Cote D'Ivoire (CDI)
- Liberia
- Sierra Leone
- Senegal
- Mali
- Guinea

**Europe**
- UK
- France

**USA**
- New York

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali ijielekeze utafiti kuelekea uchumi wa kati

**UTAFITI** ni suala lenye umuhimu mkubwa katika maendeleo ya jamii. Utafiti kuwezesha kuibuliwa kwa changamoto kadhaa na kutoa mapendekezo kuhusiana na hatua za kuchukua kwa ajili ya kuzipatia ufumbuzi.

Utafiti pia huwezesha kuibua fursa mbalimbali za maendeleo kama ugunduzi wa rasilimali mpya, dawa na mambo mengine.

Kutokana na umuhimu huo ndio maana nchi hususan zilizoendelea hutenga fedha nyingi kwa ajili ya kufanya utafiti. Pia kuanzisha taasisi za utafiti na kuziwezesha kwa njia ya kibajeti. Kwa hiyo utafiti hutoa majibu ya kitaalamu kwa kwa masuala yasiyoeleweka, hivyo ni muhimu kwa nchi zinazoendelea kujenga utamaduni wa kuwekeza katika utafiti na kuutumia katika masuala ya maendeleo.

Jambo linalotia moyo ni kuwa serikali yetu inatambua umuhimu wa utafiti na kuutumia katika kuleta maendeleo nchini.

Hilo linathibitishwa na kauli ya Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ambaye amesema kuwa serikali inatambua na kuthamini utafiti mbalimbali unaofanywa nchini na itautumia kwa ajili kuboresha maisha ya Watanzania.

Makamu wa Rais alisema hayo juzi jijini Dar es Salaam, alipofungua warsha ya 24 ya watafiti wa masuala ya uchumi, watunga sera na viongozi wa serikali za mitaa iliyoandaliwa na Taasisi ya Utafiti ya Kuondoa Umaskini (Repoa).

Kwa mujibu wa Samia, utafiti wowote unaolenga kubadilisha maisha ya watu unafanyiwa kazi na serikali na kwamba bado unahitajika katika kipindi hiki cha mabadiliko makubwa ya kiuchumi.

Alieleza kuwa serikali inatambua na kuheshimu utafiti unaofanywa mara kwa mara na Repoa katika kukuza uchumi wa nchi. Katika kulipa msukumo suala la utafiti, Samia aliahidi kwamba serikali itaendelea kuweka mazingira bora ili kuwezesha watafiti kufanya kazi kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania na kwamba utafiti wowote ulenge kuonyesha njia bora ya kufikia maendeleo ya kweli.

Kwa upande wetu tunaona kwamba kwa kuzingatia kuwa visheni ya nchi yetu ni kufikia uchumi wa kati kupitia ujenzi wa viwanda ifikapo 2025, ni wakati mwafaka kwa serikali yetu kuweka kipaumbele maalum katika utafiti.

Tunasema hivyo kwa kuwa uchumi wa viwanda msingi wake ni sayansi na teknolojia ambayo vinategemea utafiti.

Kipaumbele hicho ni kwa kuwekeza katika utafiti kupitia kuziwezesha taasisi za utafiti zilizopo kama Repoa, ESRF pamoja na vyuo vikuu vyetu, ambavyo pamoja na majukumu ya kufundisha na kutoa ushauri, pia vinafanya utafiti mbalimbali.

Vyuo vyetu vikuu vya umma kama UDSM, UDOM, Mzumbe, OUT, SUA, Ardhi kwa kutaja baadhi, vinafanya utafiti wenye matokeo chanya; tukimaanisha kuwa utafiti wao umeleta mabadiliko katika maendeleo ya nchi yetu, lakini kumekuwapo na kilio cha bajeti finyu ya kuviwezesha kufanya utafiti zaidi.

Kutokana na changamoto hiyo, tunaona umuhimu wa vyuo hivyo kuongezewa bajeti ya kufanya utafiti, hatua ambayo tumaamini italeta ufanisi katika safari yetu ya kuelekea uchumi wa kati.

Aidha, kuna umuhimu wa kuwawezesha watafiti wetu kwa njia mbalimbali, Ikiwezekana kuwazawadia wale watakaofanya utafiti ambao utainufaisha nchi zaidi.

Kitu kingine ambacho ni muhimu ni watunga sera kuwa na mahusiano ya karibu na wasomi pamoja na taasisi za utafiti, na ikiwezekana wakutane mara kwa mara kubadilishana mawazo na uzoefu kwa lengo la kufikia lengo ka uchumi wa kati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tanzania inahitaji kina Sokoine wengi zaidi

Na Lazaro Mateko

**LEO** ni kumbukumbu ya miaka 35 ya kifo cha aliyekuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Awamu ya Kwanza, Hayati Edward Moringe Sokoine, alifariki dunia kwa ajali ya gari mwaka 1984 mkoani Morogoro.

Katika uhai wake, yapo mambo mengi ambayo aliyafanya na kujijengea umaarufu mkubwa akiwa kama mtetezi wa wanyonge, hasa hatua yake ya kupambana na wahujumu uchumi bila ya kuyumba.

Alisimama kidete kupinga dhuluma na kufuatilia kwa karibu malalamiko ya wananchi kwa karibu, kama ambavyo inafanyika kwenye Serikali ya Awamu ya Tano. Kwa kifupi ni kwamba, alionyesha uzalendo wa hali ya juu.

Sokoine alikuwa muumini wa kina wa haki, usawa na uwajibikaji, katika siasa za Ujamaa na Kujitegemea na mabadiliko chanya. Aliamini kwamba, ili kuleta maendeleo, ni lazima kujituma kwa bidii katika kufanya kazi halali.

Aidha, marehemu Sokoine alikuwa mzalendo kwa taifa lake, kwani alichukia vitendo vya rushwa, hujuma, uhujumu uchumi, ulanguzi na magendo, alikuwa mtu wa vitendo na hakuwa mtu wa kupenda kulalamika.

Kwa wale walioshuhudia utendaji wake, watakumbuka kwamba alikuwa mpole, lakini pia alikuwa adui wa wazembe wasiotimiza wajibu wao sehemu ya kazi na hivyo walimuogopa.

Mtanzania huyo alipambana kuweka usawa ndio maana wahujumu uchumi walitupa vitu mbalimbali, ambavyo walipata kwa njia zisizo halali, baada ya kusikia akiwatangazia vita.

Alisimamia utekelezaji wa maagizo Mwalimu Julius Nyerere ya kupambana na wahujumu uchumi na kimsingi ndiye alikuwa kinara wa kusimamia utekelezaji wa maagizo hayo, waliotuhumiwa kuhujumu uchumi watakuwa wanakumbuka kibano walichokutana nacho.

Wapo waliotupa vitu ambavyo walipata kwa njia zisizo halali, baada ya kutangaziwa vita na kiongozi huyo aliyejipambanua kama mtetezi wa wanyonge, na kweli wanyonge walipenda.

**Alisimamia utekelezaji wa maagizo Mwalimu Julius Nyerere ya kupambana na wahujumu uchumi na kimsingi ndiye alikuwa kinara wa kusimamia utekelezaji wa maagizo hayo, waliotuhumiwa kuhujumu uchumi watakuwa wanakumbuka kibano walichokutana nacho.**

Kwa ujumla ni kwamba, wahujumu uchumi na wazembe kazini waliipatapata, kwani Sokoine hakuwa na msalie mtume, alichotaka ni kila mmoja kutimiza wajibu wake, siyo ubabaishaji.

Leo anatimiza miaka 35 mbele ya haki, lakini mambo makubwa aliyofanya kwa ajili ya nchi yake, bado yanaendelea kukumbukwa. Kimsingi, ni kwamba wanahitajika akina Sokoine wengine zaidi, ili kulijenga taifa letu.

Habari njema ni kwamba, hata Serikali ya Awamu ya Tano, hivi sasa inaonyesha uhai wa kumuenzi Hayati Sokoine kwa vitendo, kwani inapamba na kila aina ya uozo ndani ya nchi, ikiwamo rushwa na uhujumu uchumi.

Watanzania wamekuwa wakishuhudia jinsi inavyopambana kwa vitendo ikiwanasa watu mbalimbali wanaotuhumiwa kujihusisha na rushwa na uhujumu uchumi kuwafikisha mahakamani.

Nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma vimejengwa, huku wale ambao ni wazembe wakichukuliwa hatua za kinidhamu na wengine kuondolewa kazini.

Ninadiriki kusema kuwa, huu ni mwendelezo wa kumuenzi Sokoine kwa vitendo, ambaye katika uhai wake alifanya kila njia kuhakikisha anapambana kwa nguvu zote kuondoa kila aina ya uozo nchini.

Enzi za uhai wake, Sokoine aliamini katika matumizi bora ya fedha za umma. Hii pia inaonekana kwenye serikali iliopo madarakani, kwa jinsi inavyosimamia matumizi sahihi ya kodi kwa kupunguza matumizi ya anasa na zisizo za lazima, kwa kuongeza matumizi ya fedha za maendeleo.

Hiyo ni mifano michache, ambayo inaonyesha jinsi gani Sokoine anaenziwa kwa vitendo, Hivyo, ni vyema kuendelea kuenzi mambo makubwa ambayo kiongozi huyo anaifanyia nchi, hii katika nafasi ya uwaziri mkuu.

Sokoine alitangulize mbele taifa kuliko ubinafsi na pia alifanya kazi kwa bidii akitambua kwamba hakuna mtu kutoka nje atakayeiendeleza nchi hii bali ni Watanzania wenyewe.

# BENKI YA STANBIC TANZANIA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

### Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na 8 ya kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014

## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa | Mwaka uliopita |
|---|---|---|---|
| | | 31-Dec-18 | 31-Dec-17 |
| | **A. MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 14,823 | 12,444 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 132,530 | 111,852 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 69,112 | 56,484 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 119,874 | 45,703 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - 896 | 473 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 35,743 | 21,168 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 76,591 | 50,930 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 193,426 | 352,408 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 672,899 | 533,178 |
| 12 | Mali Nyingine | 42,916 | 34,494 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | - | - |
| 14 | Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 47,266 | 51,813 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **1,404,282** | **1,270,947** |
| | **B. DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 160,352 | 50,025 |
| 18 | Amana za Wateja | 851,380 | 876,289 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 | Amana Maalumu | 49,911 | 48,687 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 58 | 2,042 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 26 | 26 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 37,608 | 36,949 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 35,743 | 21,168 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 334 | - |
| 27 | Dhima Nyingine | 21,745 | 9,907 |
| 28 | Madeni | 18,502 | - |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **1,175,658** | **1,045,092** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **228,624** | **225,855** |
| | **C. FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 7,390 | 7,390 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 75,487 | 75,487 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | 121,540 | 112,059 |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 16,221 | 19,314 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 7,987 | 11,606 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **228,625** | **225,855** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 593,169 | 699,156 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 56,488 | 33,680 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 39,273 | 24,043 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| | **D. BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16% | 18% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 8% | 6% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 80% | 61% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 53% | 46% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 72% | 78% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | -1% | 11% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 10% | 13% |

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa | Mwaka Uliopita |
|---|---|---|---|
| | TAARIFA | **31-Dec-18** | **31-Dec-17** |
| 1 | Mapato ya Riba | 93,005 | 95,130 |
| 2 | Gharama za Riba | 10,588 | 15,603 |
| **3** | **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **82,417** | **79,527** |
| 4 | Madeni Viza Yaliyofutwa | - | - |
| 5 | Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 7,940 | 4,563 |
| | **Mapato baada ya tengo katika mikopo** | **74,477** | **74,964** |
| **6** | **Mapato Yasiyo ya Riba** | **52,745** | **56,055** |
| | 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 28,492 | 31,392 |
| | 6.2 Ada na Kamisheni | 23,482 | 21,854 |
| | 6.3 Gawio | - | - |
| | 6.4 Mapato Mengine | 771 | 2,809 |
| **7** | **Gharama Zisizo za Riba** | **102,683** | **101,339** |
| | 7.1 Mishahara na Mafao | 53,919 | 52,913 |
| | 7.2 Ada na Kamisheni | 15,004 | 14,644 |
| | 7.3 Gharama Nyingine | 33,759 | 33,782 |
| **8** | **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **24,539** | **29,680** |
| 9 | Tengo la Kodi ya Mapato | 8,318 | 10,367 |
| **10** | **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **16,221** | **19,314** |
| 11 | **Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha)** | - | - |
| | i) Mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | - 3,488 | 8,363 |
| | ii) Kodi ya mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika | 1,039 | - 2,509 |
| **12** | **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **13,773** | **25,168** |
| 13 | Idadi ya Waajiriwa | 539 | 559 |
| 14 | Mapato kwa Hisa | 2.2 | 2.6 |
| 15 | Idadi ya Matawi | 9 | 9 |
| | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) | Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.2% | 1.6% |
| (ii) | Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 7.3% | 9.1% |
| (iii) | Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 70.5% | 67.0% |
| (iv) | Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 7.6% | 8.4% |

*Tarakimu za wastani zitakokotolewa kwa kujumlisha salio la mwisho kwa miezi inayohusika katika kipindi na kugawanya kwa idadi ya miezi katika kipindi hicho*

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa | Mwaka Uliopita |
|---|---|---|---|
| | TAARIFA | 31-Dec-18 | 31-Dec-17 |
| **I:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | **16,221** | **19,314** |
| | Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| | - Hasara Katika Mali | 7,669 | 7,155 |
| | - Badiliko Halisi Katika Mikopo | - 154,295 | - 4,461 |
| | - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - 215 | 2,462 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 101,218 | 112,866 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 146,355 | - 196,690 |
| | - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 10,847 | 6,187 |
| | -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 1,898.95 | 3,655 |
| | - Kodi Iliyolipwa | - 9,886 | - 11,557 |
| | - Mengineyo (bainisha) | 2,778 | 7,339 |
| | *Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji* | **122,590** | **- 53,731** |
| **II:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | - | - |
| | Gawio Lililopokewa | - | - |
| | Ununuzi wa Mali za Kudumu | - 3,590 | - 9,541 |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 248 | 3,033 |
| | Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - | - |
| | *Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji* | **- 3,342** | **- 6,507** |
| **III:** | **Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| | Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | - |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| | Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 18,502 | - |
| | Mengineyo (bainisha) | - 13,452 | 5,909 |
| | Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha | ***5,050*** | ***5,909*** |
| **IV:** | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| | Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | 124,298 | - 54,330 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 148,077 | 202,407 |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 272,374 | 148,077 |

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DECEMBER 2018

(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mabadiliko thamani katika amana zinazouzika | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| ! **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 131,372 | 2,496 | 4,648 | 4,463 | 225,855 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 16,221 | - | - | - | 16,221 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - 2,448 | - 2,448 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 1,424 | - 2,496 | 1,072 | - | 0 |
| Mengineyo | - | - | - 11,256 | - | - | 253 | - 11,003 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **7,390** | **75,487** | **137,761** | **0** | **5,719** | **2,267** | **228,624** |
| " **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 7,390 | 75,487 | 113,140 | 0 | 5,138 | - 521 | 200,633 |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 19,314 | - | - | - | 19,314 |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | 5,854 | 5,854 |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | - | - | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - 2,006 | 2,496 | - 490 | - | 0 |
| Mengineyo | - | - | 925 | - | - | - 871 | 54 |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **7,390** | **75,487** | **131,372** | **2,496** | **4,648** | **4,463** | **225,855** |

**BAADHI YA MAELEZO**
**KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DECEMBER 2018**

Mabadiliko ya thamani katika amana zinazouzika yamesababishwa na kubadilika kwa faida katika amana za serikali. Tengo kwa mikopo chechefu limekokotelewa kwa kutumia muongozo mpya wa utunzaji fedha na mali wa kimataifa (IFRS 9)

Taarifa hizi zimetoka katika hesabu ya Fedha ya Benki kwa mwaka 2018. Taarifa hizi zimekaguliwa kwa mujibu wa muongozo wa utunzaji fedha na mali wa kimataifa (International Financial Reporting Standards - IFRS). Hesabu hizi zimekaguliwa na Pricewaterhousecoopers (PWC) na kupata hati safi. Taarifa hizi zimepewa idhini na Bodi ya wakurugenzi na kusainiwa kwa niaba ya bodi na:

| *Jina* | *Saini* | *Tarehe* |
|---|---|---|
| 1. Prof. Marck Mwandosya **(Mwenyekiti wa bodi)** | | 14-Mar-19 |
| 2. Ken Cockerill **(Ofisa Mtendaji Mkuu)** | | 14-Mar-19 |

215173002

TRA
TANZANIA REVENUE AUTHORITY

**TAARIFA KWA UMMA**

**MWISHO WA KUUZA AU KUENDELEA KUWEPO SOKONI KWA BIDHAA ZISIZO NA STEMPU ZA USHURU WA BIDHAA ZA KIELEKTRONIKI**

*08 Aprili, 2019 – Dar es Salaam*

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inapenda kuutaarifu umma kuwa, bidhaa zote ambazo ziko sokoni na zimebandikwa stempu za zamani (zisizo za kielektroniki) na zile ambazo hazijabandikwa stempu za ushuru wa bidhaa kabla ya kuanza kwa Mfumo wa Stempu za Kodi za Kielektroniki (ETS), zinaruhusiwa kuendelea kuwepo sokoni hadi tarehe **30 Aprili, 2019.**

Ruhusa hii ni kwa mujibu wa matakwa ya **Kanuni ya 44 (3)** ya Kanuni za Stempu za Kodi za Kielektroniki ya Mwaka 2018. Bidhaa husika ni **Sigara, Mvinyo, Pombe Kali, Bia na aina zote za Vileo** zinazozalishwa au zinazoingizwa nchini.

Baada ya tarehe hii ya ukomo kupita, bidhaa zote zenye stempu za kodi za zamani zitatakiwa kuwa na stempu mpya za kielektroniki. Hivyo, wasambazaji, wazalishaji na waingizaji wa bidhaa husika wanatakiwa kufanya utaratibu wa kuhakikisha kwamba bidhaa hizo zinakuwa na stempu za kieletroniki kabla hazijaingia sokoni.

Kwa taarifa hii, wafanyabiashara na umma kwa ujumla wanajulishwa kwamba, baada ya tarehe **30 Aprili, 2019,** TRA itafanya operesheni maalum ya kuondoa sokoni bidhaa zote zenye stempu za zamani na zisizo na stempu za kielektroniki na hakuna fidia au marejesho yoyote yatakayofanyika.

Ikumbukwe kwamba, tarehe **15 Januari, 2019,** ilikuwa ni tarehe rasmi ya kuanza kutumika kwa Stempu za Kodi za Kielektroniki kwa bidhaa za awamu ya kwanza zilizoainishwa hapo juu, na tarehe hii ilitangazwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania katika vyombo mbalimbali vya habari.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na ofisi ya TRA iliyo karibu, tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania **www.tra.go.tz** au Kituo cha Huduma kwa Wateja kwa namba za bure **0800 750 075 au 0800 780 078** au barua pepe; **huduma@tra.go.tz**. Pia, unaweza kutuma ujumbe kwa njia ya **WhatsApp** kwenda namba 0744 – 233 333.

*"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"*

**Imetolewa na;**

**Charles E. Kichere**
**KAMISHNA MKUU**
**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

# Watu 307 waugua dengue

INATOKA UK. 3

Nyingine ni kuimarisha ufuatiliaji wa magonjwa nchi nzima kwa kutumia mfumo uliopo wa ukusanyaji wa taarifa na wanaendelea kupata taarifa za kila siku kuhusu mwenendo wa ugonjwa huo na mengine.

"Kuimarisha uwezo wa utambuzi wa ugonjwa katika maabara ili kuthibitisha ugonjwa huo na kuhimiza ufuatiliaji wa homa hiyo ni kwa mikoa yote nchini," alisema.

Aliwasihi wananchi kutokuwa na hofu, bali kuwahi kwenda katika vituo vya kutolea huduma za afya mara waonapo dalili za ugonjwa huo kama zilivyoainishwa.

"Pia, jamii ihakikishe kuwa mazalio yote ya mbu yanaangamizwa hasa kipindi hiki cha mvua na kwamba hata maji yaliyopo kwenye kisoda huweza kusababisha mazalia ya mbu," alisema.

Akizungumzia kuhusu dawa, Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Mohamed Kambi, alisema kuwa dawa hizo si salama mgonjwa mwenye dalili au ayeugua ugonjwa wa dengue kwa kuwa inaweza kusababisha kutokwa damu sehemu mbalimbali za mwili.

"Hivyo anapozitumia zinaweza kumsababishia kupoteza damu nyinyi, na hii Diclopar ina mchanganyiko wa Diclofenac na Paracetamol, hivyo dawa za aina hiyo zinaweza kuwa tatizo kwa mgonjwa mwenye ugonjwa huo inaweza kuchangia mtu kupoteza damu nyingi," alisema.

Alitaja dawa zingine mbali na Diclopar zenye jamii ya Diclofenac, Brufen au Ibuprofen hazitakiwi kutumia mgonjwa wa ugonjwa huo.

"Mara chache hutokea mgonjwa wa homa ya dengue kutokwa na damu sehemu za fizi, mdomoni, puani, kwenye macho na pia kwenye njia ya haja kubwa au ndogo akinywa hizi dawa damu itazidi kutoka nyingi," alisema.

# Kijana aibua kashfa nzito mbele ya JPM

INATOKA UK. 2

ya maji na kuwataka viongozi wa mkoa huo wakiwamo askari kumlinda na kuhakikisha hakuna mtu atayembugudhi.

Mbali na hilo, Rais Magufuli alimwita kwenye jukwaa kuu kijana huyo na kupeana mkono kisha kuagiza na yeye akae jukwaa kuu wakati akiendelea na hotuba yake.

Awali, Rais Magufuli alisema uhakiki wa miradi ya maji uliofanywa na wataalamu wa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kuanzia mwaka 2013 hadi 2018, ilibainika kati ya miradi iliyogharimu Sh. bilioni 119, miradi ya Sh. bilioni 102 ilikuwa hewa.

"Kati ya Sh. bilioni 119, miradi ya kweli ni ya Sh. bilioni 17 kwa hiyo mingine yote ilikuwa hewa, watu walikuwa wanadai fedha kuwa wamefanya miradi ya maji, lakini maji yalikuwa hayapo, hii maana yake ni kwamba haina tofauti na kusema miradi hewa, hizi fedha hazikulipwa," alisema.

Rais Magufuli alimtaka Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, aisimamie vizuri miradi ya maji inayotekelezwa.

Rais Magufuli alitolewa mfano mradi mmoja uliokuwa ukitekelezwa Kanda ya Ziwa ambao zilitumika Sh. milioni 800, lakini maji hayakuwapo.

"Waziri na watendaji wako mkawe wakali, kama waziri una uwezo wa kuvuta bangi ya Njombe kaivute, ili ukienda kwenye mradi wa maji makandarasi wafanye kazi," alisema.

Pia alisema alishatoa maagizo kuwa makandarasi wote wa Halmashauri za Wilaya wahamie Wizara ya Maji ili miradi itekelezwe huko badala ya kuzungumza miradi iliyopo kwenye makaratasi.

Rais Magufuli alisema haiwezekani mji mkubwa ukose maji halafu watu wake wapate ugonjwa wa kipindupindu na kusababisha kutumika kwa fedha nyingi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
Tarehe 11/04/2019.

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano tarehe 14/4/2019** kampuni ya **EFFCO SOLUTION LTD** itasafirisha Mzigo wako wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar es salaam kuelekea Nairobi,** gari hilo lenye namba za usajili:
   **T 875 CZT / T 901 CZT**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **19.50** |
| **Upana** | - | **mita** | **2.70** |
| **Kimo** | - | **mita** | **4.60** |

3. Njia itakayotumika: Dar es salaam mpaka Nairobi kupitia Moshi, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

215173602

HABARI KITAIFA

# Nyaya za kupitiwa mawasiliano marufuku

**Na Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Viwango Tanzania (TBS) limepiga marukufu kuuzwa kwa nyaya za kupitiwa mawasiliano (Data Cable) zilizokuwa zikiuzwa kwenye baadhi ya maduka ya vifaa vya kielektroniki baada ya kubainika hazikidhi viwango.

Marufuku hiyo ilitolewa na maofisa wa shirika hilo kwenye baadhi ya maduka jijini Dar es Salaam baada ya sampuli za nyaya hizo kupimwa kwenye maabara na kuthibitika hazikidhi viwango.

Mkaguzi wa TBS, Saimon Emmanuel, alisema wenye maduka yaliyokuwa yakiuza nyaya hizo wamepewa siku 14 kujieleza ni kwa nini wasichukuliwe hatua.

Emmanuel alisema baada ya kujiridhisha kuwa nyaya hizo hazikidhi viwango, hatua ya kwanza iliyochukuliwa ni kuzuia nyaya hizo kuendelea kuuzwa na ametoa mwito kwa Watanzania kutozinunua na kigezo kimoja wapo wanachoweza kutumia kuzitambua ni kuuzwa bei ndogo. Alisema baada ya kupimwa kwenye maabara za shirika pamoja na kasoro nyingine, nyaya hizo zilibainika kuwa na kiwango kidogo cha madini ya shaba (copper) na kwamba hata nguvu kinzani kwenye nyaya hizo zilifeli kwenye maabara.

"Hivyo tumezizuia kwenye maduka tukisubiri hatua nyingine," alisema. Alitoa mwito kwa wafanyabiashara wanapotaka kununua bidhaa kutoka nje ya nchi kuhakikisha zinakaguliwa ubora wake nje ya nchi kabla hazijaingia nchini, mpangao ambao kitaalamu unaojulikana kama Pre-Shipment/Export Verification of Conformity to Standards (PVoC). Alisema wanaoingiza bidhaa kutoka nje ya nchi bila kukaguliwa kupitia PVoC, bidhaa zao zinapofika nchini wanatozwa faini ya asilimia 15 kulingana na thamani ya mzigo, kulipia gharama za upimaji kwenye maabara na kwamba zinapofeli kufikia viwango mwagizaji anaamuriwa kuzirudisha alikozitoa kwa gharama zake au kuteketezwa hapa nchini pia kwa gharama zake.

Emmanuel alisema hiyo ni kwa mujibu wa Sheria Na:2 ya Viwango ya mwaka 2009. Alitoa mwito kwa wafanyabiashara kuhakikisha wazingatia sheria na taratibu ili kuepuka hasara.

Shirika hilo linaendesha awamu ya pili ya msako wa kushtukiza wa bidhaa zilizopo sokoni ili kubaini bidhaa ambazo hazina ubora na kuziondoa kwenye soko.



Mamalishe akipeleka chakula kwa mteja wake katika eneo la Mabibo, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# PM akerwa alikofia Sokoine kutelekezwa

**Na Beatrice Moses**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ametembelea eneo alipopata ajali Waziri Mkuu mstaafu wa awamu ya kwanza, hayati Edward Moringe Sokoine, Aprili 12, 1984, ambapo ameonyesha kukerwa kwa jinsi kulivyotelekezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa Ofisi ya Waziri Mkuu Dodoma, Waziri Mkuu kutokana na hali hiyo ameuagiza uongozi wa Mkoa wa Morogoro uhakikishe unaboresha eneo hilo la kumbukumbu ya Sokoine lililoko Wami-Dakawa, wilayani Mvomero mkoani Morogoro.

Alitoa maagizo hayo kwa Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Steven Kebwe, Mkuu wa Wilaya ya Mvovero, Mohammed Utali na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Florent Kyombo, wasimamie haraka uendelezaji na utunzaji wa eneo hilo ili paanze kutumika kwa shughuli ya kumbukumbu.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa Majaliwa alitoa agizo hilo jana wakati akizungumza na viongozi wa mkoa na watumishi wa Wilaya ya Mvomero baada ya kukagua ujenzi wa shule hiyo.

"Hili eneo ni maalum. Tulikubaliana ndani ya serikali liwe sehemu ya kumbukumbu ya Mheshimiwa Edward Moringe Sokoine, na keshokutwa ni miaka 35 ya kumbukumbu yake, lakini hakuna chochote ambacho kimeandaliwa hapa kwa ajili hiyo," alisema.

"Eneo hili liko jirani kabisa na Makao Makuu ya Halmashauri ya Mvomero. Mngekuwa mmepaendeleza tangu halmashauri ilipoanza, hata bustani mnayosema mnataka kuiweka ingekuwapo hapa."

Waziri Mkuu aliweka wazi jinsi anavyoshangazwa kuona eneo hilo limetelekezwa, wakati Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya wapo.

"Hili eneo kama lingeendelezwa, naamini hata mbio za kumbukumbu yake zilizofanyika Arusha mwishoni mwa wiki iliyopita, zingefanyika hapa. Hata wanafamilia wangekuwa wanapita hapa kwa ajili ya kumbukumbu hiyo," alisema.

"Mkurugenzi wa Halmashauri hapa ni lazima pasafishwe, huku mbele pawe na bustani na hii miti ya mbele iachwe ili papendeze. Mkuu wa Wilaya una Kamati yako ya Ulinzi na Usalama, tumia watu wako ili zoezi hili likamilike," alisisitiza.

## Walimu, wanafunzi waokoa fedha ujenzi wa shule

**Na Sabato Kasika**

WALIMU na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mugango iliyoko Musoma mkoani Mara, wameokoa zaidi ya Sh. milioni mbili, ambazo zingetumika kulipa wasombaji wa mawe, moramu, maji na miti ya mbao kwa ya ujenzi wa madarasa, ofisi ya walimu na choo.

Mkuu wa shule hiyo, Chacha Rugita, alisema juzi wameamua kusomba vitu hivyo badala ya kazi hiyo kufanywa na watu wengine na kutumia fedha ambazo zingefanya kazi zingine.

Mwalimu huyo alisema hayo alipokuwa akizungumzia maendeleo ya uboreshaji wa miundombinu ya shule hiyo.

"Walimu na wanafunzi wamesomba moramu tripu 18 zenye thamani ya Sh. 900,000 na wamechangia vipande vya miti ya mbao 88 vya Sh. 176,000," alisema.

Aliendelea kufafanua kuwa wamesomba mawe tripu 10 yeye thamani ya Sh. 350,000 na wamesomba maji kwa ajili ya ujenzi yenye thamani ya Sh. 500,000. "Ukipiga hesabu hiyo utagundua kwamba tumeokoa zaidi ya Sh. milioni mbili ambazo tungewapa watu watusombee, lakini tumefanya kazi hiyo wenyewe ili fedha zitumike kwa mambo mengine ya shule," alisema Rugita.

Aidha, mwalimu huyo alisema wananchi nao wakiongozwa na madiwani wao, wamesomba mchanga tripu 40, mawe tripu 15 na kokoto tripu tisa.

"Kwa ujumla ni kwamba hayo yote ni kuunga mkono juhudi za serikali za kuboresha elimu, kwa kuwa tayari imetukabidhi Sh. milioni 66.6 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa matatu, ofisi ya walimu na choo cha matundu saba," alisema.

Alisema mbali na ujenzi wa madarasa, ofisi na choo, pia wana mpango wa kujenga jengo la maabara ya baiolojia kwa vile vifaa vya ujenzi ikiwamo saruji wanavyo.

"Mbunge wetu Profesa Sospeter Muhongo ambaye pia ni mdau mkubwa wa elimu, alishatukabidhi mifuko 50 ya saruji, hivyo itatumika kwa ajili ya ujenzi huo," alisema.

# Bil. 34/- kulipa fidia wananchi waliopisha mradi wa umeme

WIZARA ya Nishati inatarajia kutenga Sh. bilioni 34 kupitia bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi wa maeneo ya Kisarawe, Kibaha Mjini, Vijijini, Chalinze na eneo la Kiluvya.

Sambamba na hilo, Sh. bilioni 21.6 zinatakiwa kulipwa fidia kwa wananchi katika maeneo ya Halmashauri za Kisarawe, Kibaha Mjini, Wilaya ya Kibaha, Chalinze na Kiluvya na taratibu zote za uandaaji taarifa na majedwali ya malipo ya fidia zimekamilika.

Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, alisema hayo jana, bungeni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kibaha Mjini(CCM), Silyvestry Koka.

Mbunge huyo katika swali lake, alihoji serikali ina mpango gani wa kulipa fidia wananchi ambao maeneo yao yamechukuliwa kwa ajili ya mradi mkubwa wa umeme wa msongo wa KVA 400 kutoka Kinyerezi kupitia Pwani, Morogoro, Singida na Arusha.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mgalu alisema wananchi hao watalipwa baada ya kukamilika kwa kazi ya kuhuisha upembuzi yakinifu na gharama za mradi kwa kipande cha kutoka Kinyerezi hadi Chalinze.

Aliomba wananchi hao waendelee kuvuta subira wakati serikali inaendelea kukamilisha taratibu za malipo yao ya fidia. Mgalu alifafanua kuwa serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) inatekeleza mradi wa kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi jijini Dar es Salaam na Rufiji mkoani Pwani kupitia Chalinze hadi Dodoma.

"Malengo ya mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa umeme katika ukanda wa mashariki, kati na kaskazini mwa nchi kutoka kwenye mitambo ya kuzalisha umeme ya Kinyerezi na mradi wa Rufiji,"alisema.

Mgalu alieleza awamu ya kwanza ya upimaji njia na kutathimini mali za wananchi watakaopisha mradi kutoka Kibaha hadi Chalinze ilikamilika Desemba, 2017 na kuidhinishwa na mthamini mkuu wa serikali Novemba, mwaka jana.

Hata hivyo, alisema serikali kupitia Tanesco Januari, mwaka huu, ilitangaza zabuni kwa ajili ya kumpata mtaalamu mshauri wa kufanya upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Rufiji hadi Chalinze na kuhuisha upembuzi yakinifu wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 400 kutoka Kinyerezi hadi Chalinze.



Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Robert Makaramba (wa tatu kulia), akifafanua jambo kwa Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi (wa pili kulia), alipotembelea chumba cha Mahakama ya Watoto Mbeya, akiwa katika ziara mkoani humo, jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Tathmini kufanywa mawasiliano Tabora

SERIKALI kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) itafanya tathmini kamili ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika vijiji vyote vya majimbo ya Tabora Mjini na Iramba Mashariki.

Hayo yalibainishwa bungeni jana na Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Atashasta Nditiye, wakati akijibu swali la Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), Emmanuel Mwakasaka.

Katika swali lake, mbunge huyo alisema maeneo mengi katika Jimbo la Tabora Mjini na Iramba Mashariki hayana mawasiliano ya simu na kuhoji serikali ina mpango gani wa kujenga minara ya simu maeneo hayo ili wananchi wa maeneo hayo wapate mawasiliano.

Nditiye akijibu swali hilo, alisema UCSAF itafanya tathmini kamili ya upatikanaji wa huduma za mawasiliano katika vijiji vyote vya kata za majimbo hayo.

Alisema vijiji vitakavyobainika kukosa mawasiliano au kuwa na mawasiliano hafifu vitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuisha katika zabuni zitakazotangazwa hivi karibuni.

"Serikali kupitia UCSAF inasimamia utekelezaji wa sera ya taifa ya Tehama ya mwaka 2016 inayoelekeza kufikisha huduma za mawasiliano katika maeneo yote yakiwamo yasiyo na mvuto kibiashara,"alisema.

Hata hivyo, alisema hadi sasa kata 703 katika mikoa yote nchini zimefikiwa na huduma za mawasiliano kwa jitihada za mfuko huo na Watanzania zaidi ya milioni nne wamepata huduma za mawasiliano.

"Tabora Mjini zaidi ya wakazi 12,992 wamefikishiwa huduma za mawasiliano katika kata za Kabila na kampuni ya Halotel, Kalunde na Vodacom na Uyui Vodacom,"alisema. Pia alisema kwa Iramba zaidi ya wakazi 12,320 wamefikishiwa huduma za mawasiliano katika kata za Mtekente na kampuni ya Vodacom na Urughu na TTCL kupitia mfuko wa mawasiliano kwa wote.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

## Mbunge alilia ruzuku ya maendeleo jimboni

MBUNGE wa Nsimbo (CCM), Richard Mbogo, ameitaka serikali kuangalia suala la utoaji ruzuku za maendeleo kwa Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo ambayo imeathirika kwa kiwango kikubwa kimapato.

Akiuliza swali bungeni jana, mbunge huyo alisema mabadiliko ya sheria ya fedha ya serikali za mitaa sura 290 yameleta nafuu sana kwa wakulima, lakini wakati huo huo halmashauri za wilaya zenye wakulima wadogo wadogo zimeathirika kimapato na kusababisha kushindwa kutatua kero za wananchi kwa wakati. "Je, serikali inaweza kuangalia upya suala la utoaji ruzuku za maendeleo? Maana Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo imeathirika kiwango kikubwa. "Je, serikali iko tayari kuipa ruzuku ili kutoa huduma za elimu na afya?" Alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Mwita Waitara, alisema hadi Machi, mwaka huu, serikali imepeleka Sh. milioni 416 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo kwa ajili ya kugharamia elimu ya msingi bila malipo.

Pia alisema Sh. milioni 250 zimetolewa kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma 20 ya shule ya sekondari na Sh. milioni 411 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vitendanishi na vifaa tiba.

Alisema serikali itaendelea kuongeza utoaji wa ruzuku kwa mamlaka za serikali za mitaa kwa kadiri ya upatikanaji wa fedha.

Awali, alisema sheria ya fedha ya serikali za mitaa sura 290 imefanyiwa marekebisho na bunge Juni mwaka 2017 kwa kupunguza kiwango cha ushuru wa mazao kutoka asilimia 5 hadi 3 kwa mazao ya chakula na baishara.

Hata hivyo, alisema mamlaka za serikali za mitaa zimeendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo katika vyanzo vilivyopo ili kuongeza mapato na kuboresha utoaji huduma kwa wananchi. Alisema kutokana na mikakati hiyo mapato ya ndani ya halmashauri yameendelea kuongezeka kila mwaka, huku akitolea mfano katika mwaka wa fedha 2017/18, halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya Sh. bilioni 687 na zilikusanywa Sh. bilioni 553.39 sawa na asilimia 81. Alifafanua pia katika mwaka wa fedha 2018/19 halmashauri zimeidhinishiwa kukusanya Sh. bilioni 735.58 na hadi Februari mwaka huu, zimekusanywa Sh. bilioni 401 sawa na asilimia 55.

Aidha, katika mwaka wa fedha 2019/20 halmashauri zinakadiria kukusanya Sh. bilioni 765.

Alisema hali halisi kwa ujumla inaonyesha makusanyo ya halmashauri yameendelea kuongezeka pamoja na kupungua kwa ushuru wa mazao kutokana na kubuniwa kwa vyanzo mbadala vya mapato.



Mtaalamu mwezeshaji wa kunyunyiza viuatilifu kutoka TPRI, Justin Ringo (kulia), akiwafundisha baadhi ya wakulima katika Kijiji cha Endadoshi, Kata ya Qash, kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu, mabomba ya kunyunyizia na vifaa vyake, usafi wa vifaa na namna ya kuhifadhi, ili kuepusha madhara kwa walaji katika mafunzo yaliyofanyika wilayani Babati juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakulima wapewa mafunzo matumizi bora ya viuatilifu

**Na Mwandishi Wetu,** BABATI

TAASISI ya Utafiti wa Viuatilifu vya Kudhibiti Visumbufu katika Ukanda wa Tropiki (TPRI), imetoa mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu kwa wakulima zaidi ya 200, ili kuepusha jamii na magonjwa yatokanayo na matumizi mabaya ya sumu za kuulia wadudu waharibifu wanaoshambulia mazao.

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa mafunzo hayo kwa wakulima maeneo mbalimbali nchini.`

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Matumizi kutoka TPRI, Dk. Mwema Felix, alisema mafunzo yaliyotolewa kwa wakulima hao yatawawezesha kutumia kwa usahihi viuatilifu na hivyo kuzuia au kupunguza athari zake kwa walaji na wakulima.

Mafunzo hayo yalifanyika kwa wakulima wa maeneo ya Dareda, Riroda, Kijiji cha Endadoshi katika Kata ya Qash na Kijiji cha Endanoga kilichopo Kata ya Gallapo, wilayani Babati na kumalizika juzi.

Mtaalamu mwezeshaji wa kunyunyiza viuatilifu mashambani kutoka TPRI, Justin Ringo, aliwaeleza wakulima hao kuwa matumizi ya sumu nyingi bila kuzingatia vipimo inasababisha magonjwa kwa walaji wa mazao hayo.

Katika ufundishaji wake, Ringo alipata maelezo ya aina ya mazao wanayolima kama vile mahindi, mbaazi, maharagwe, alizeti, ufuta, dengu, choroko, mtama na mbogamboga, wadudu wasumbufu wanaoshambulia mazao hayo na aina ya viuatilifu wanavyotumia.

Aliwataka wakulima kusoma maelekezo yaliyomo kwenye vibandiko vya chupa za sumu vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza ili kujua masharti na namna bora ya kuzitumia.

Baadaye aliwafundisha kuhusu aina ya vifaa vinavyotumika kunyunyizia, seti kamili ya mabomba na namna ya kutayarisha sumu na inavyotumika, muda mzuri wa kunyunyia na namna ya kusafisha na kutunza vifaa na dawa baada ya kazi ya kunyunyiza.

Aliwafundisha namna ya uvaaji wa nguo maalum, miwani ya kuzuia sumu kuingia machoni, au mwilini na kuuzia pua wakati wa kuchanganya, kukoroga na kunyunyiza sumu kwenye mazao.

Kwa upande wake, mtafiti James Simon, alisema, sumu inatengenezwa kuua, hivyo, isipotumika vizuri mashambani inaweza kusababisha vifo kwa walaji wa mazao hayo.

Alisema kwa mfano kumekuwa na ongezeko la magonjwa kama ya saratani ambayo kwa kiasi yanasababishwa na matumizi yasiyo sahihi ya viuatilifu na yanayofanywa na baadhi ya wakulima.

Alisema wengi wanatunza sumu vyumbani mwao au kwenye dari baada ya kutumika mashambani kwa kubaki, jambo ambalo linahatarisha uhai wao.

Aliwafundisha kuhusu namna ya kufanya usafi wa vifaa vilivyotumika kunyunyizia sumu mashambani kwa kuwa na sehemu moja maalum ya kufanyia usafi na siyo mtoni au kwenye mifereji na chupa zilizokwishatumika zisitupwe bali vichomwe moto.

"Tusioshe mabomba mtoni yaliyotumika kwa viuatilifu, chagua mahali maalumu pa kuoshea mabomba na vifaa vya viuatilifu bali viondolewe na kuchomwa moto," alisema.

Kuhusu utumiaji wa sumu hizo mashambani, alisema, wapo wadudu waharibifu ambao wanahitaji viuatilifu vinavyopenya (vya mfumo) hadi ndani ya mmea na kuua mdudu anapogusa na zipo sumu zingine za kawaida.

Alisema kwa wadudu wanaokaa ndani ya mmea, wanatakiwa kutumia sumu zinazopenya na siyo za kawaida ambazo zinafaa zaidi kwa wadudu wanaokaa juu ya mimea au majani.

Kwa upande wake, Ofisa Kilimo wa Kata ya Qash, Adelta Macha, alisema wakulima wengi wamekuwa na tabia ya kutotoa taarifa mapema pale wadudu waharibifu wanapozuka.

Alisema badala yake wanachofanya ni kwenda kununua viuatilifu na kuvitumia kwa mazoea pasipokujua vinatumikaje na wanapoona tatizo linazidi kuwa kubwa ndipo wanapowasilisha malalamiko yao.

Aliwaomba waendelee kushirikiana mara kwa mara kuhusu kilimo cha mazao na utunzaji bora wa mazao.

# Kituo cha afya kuhudumia watu 10,000

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

KITUO cha Afya Manyire, katika Halmashauri ya Arusha DC, kitakachotoa huduma kwa watu zaidi ya 10,000 kilichojengwa na Serikali kwa msaada wa Serikali ya Japan, kimezinduliwa na Balozi wa Japan nchini, Shinichi Goto.

Akizungumza wakati wa kuzindua na kukabidhi jengo hilo kwa Halmashauri ya Arusha DC, Balozi Goto, alisema Japan ilichangia dola za Marekani 87,872 sawa na sh milioni 191.

Alisema Februari 22, mwaka jana Ubalozi wa Japan na Halmashauri ya Arusha DC, walisaini makubaliano ya ujenzi wa kituo hicho.

Alisema Japan, ilitoa msaada huo, kutokana wananchi wa eneo hilo kuwa na uhitaji mkubwa wa huduma za afya na walikuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilomita 25, kwenda maeneo ya mjini kutafuta huduma za matibabu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Wilson Mahera, alisema hadi kukamilika kwa ujenzi huo, umegharimu fedha kiasi cha sh 478, 643, 016.

Alisema wananchi walichangia sh. milioni 20 na sh. 64,257,800 zilitolewa na halmashauri hiyo wakati sh milioni 120, zilitolewa na mfanyabiashara Mathias Manga mkazi wa eneo hilo kama sehemu ya mchango wake katika jamii.

# Chanjo ya kinga homa ya ini kufanyika Julai Mosi

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, inatarajia kutoa kinga ya homa ya ini kwa wananchi katika hospitali za rufani mikoani, kuanzia Julai Mosi, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu juzi, Waziri Ummy Mwalimu, alisema kutokana na kuonekana kuenea kwa kasi kwa ugonjwa wa homa ya ini B na C nchini, kinga hii imeanza kutolewa kwa baadhi ya hospitali hapa nchini.

"Tunaanza kusambaza hospitali zote za mkoa pamoja na vituo vya forodha (OSBP) Julai, ila kwa sasa kinga inatolewa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Taasisi ya Saratani Ocean Road na Hospitali ya Benjamin Mkapa," alisema.

Alieleza ugonjwa wa homa ya ini unatibika kama hatua zake ni za awali, lakini kama umekomaa hauwezi kutibika.

"Homa hii ya ini imegawanyika kuna A, B, C, D, na E, ila unaosumbua hapa nchini ni B na C, chanjo yake ipo, ni dozi ya mara tatu kila baada ya miezi miwili, unatakiwa kuchoma sindano, hivyo, chanjo yake ni ndani ya miezi 6," alieleza.

Aliwataka wananchi kujenga utamadauni na desturi ya kupima afya mara kwa mara, hususani, kwa magonjwa ambayo si ya kuambukiza. Akitolea mfano ugonjwa wa kisukari, saratani, ugonjwa wa moyo pamoja na shinikizo la damu na kusema hata ufanyaji wa mazoezi husaidia kujenga mwili.

Aidha, alisisitiza wananchi kukata Bima ya Afya kwa ajili ya kuwasaidia kupunguza gharama za matibabu na kuepusha usumbufu nyakati za kuhudumiwa pindi wawapo hospitali.

"Watanzania wengi wanapenda kuchangia, kitchen party, harusi na sherehe mbali mbali, lakini panapo tokea tatizo la maradhi hakuna aliyepo tayari kuchangia, wajenge utamaduni wa kutumia bima ya afya kuokoa maisha na kupunguza gharama za matibabu," alidai Ummy.

Ofisa Afya Mfawidhi OSBP, Dk Gabriel Mdachi, alisema kazi kubwa wanayoifanya katika eneo hilo ni kudhibiti na kufuatilia magonjwa ya kuambukiza yanayoripotiwa kitaifa.

"Tunadhibiti magonjwa ya milipuko, mfano homa ya manjano, ebola na homa ya Bonde la Ufa," alisema.

Alisema hapa mpakani wanatoa kinga ya homa ya manjano na kinga hii inatolewa kwa wasafiri wa EAC na wale wa nje ya EAC lakini hata mwananchi ambaye yupo mpakani na si msafiri anaruhusiwa kupata kinga hii.

"Gharama za matibabu kwa wananchi wa EAC kwa kinga ya homa ya manjano, mtu mmoja ni ni sh 30,000 na wale wanaotoka nje ya EAC dola 50," alisema.

Hata hivyo, alisema kituo hicho kinatarajia kuanza kutoa kinga ya homa ya ini pindi Wizara ya Afya itakapo kamilisha taratibu zake.

"Ugonjwa wa homa ya ini unaenea kwa kasi nchini na maambukizi yake ni kugusana jasho na hata kwa kufanya mapenzi, hivyo kuna umuhimu wa kuthibiti kwa haraka" alisema.

# Serikali yakiri wananchi vijijini wanateseka kufuata matibabu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imesema wananchi wanaoishi maeneo ya vijijini ambao wanahitaji kupata huduma za afya kwa njia za upasuaji, wanalazimika kutembea umbali wa kilometa 119 hadi 300.

Inaelezwa kuwa wananchi hao hufanya hivyo ili kupata huduma bora za afya kwa gharama nafuu katika hospitali za rufani, jambo ambalo limekuwa likichangia wagonjwa wenye kipato cha chini kushindwa kupata matibabu kutokana na changamoto za upatikanaji wa huduma hizo maeneo ya karibu.

Mkurugenzi wa Mafunzo na Uendelezaji Rasilimali Watu wa wizara hiyo, Dk. Saitore Laizer, ameyasema hayo jana, wakati akizungumza na wataalamu na wanafunzi wa masomo ya udaktari wanaobobea katika upasuaji kwa njia ya matundu katika Hospitali ya Rufani ya KCMC.

Dk. Laizer alisema asilimia 70 ya wananchi wanaoishi vijijini, wamekuwa hawapati huduma bora za afya za upasuaji kwa gharama nafuu. Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, hali hiyo imebainika baada ya utafiti kufanyika mwaka 2012, ambapo taarifa hiyo imeeleza bayana kwamba huduma bora za upasuaji ni changamoto kubwa. "Kwa sasa serikali imetenga shilingi bilioni 2.5 kwa ajili ya kusomesha wataalamu wa afya 350 kila mwaka ili kukabiliana na changamoto za upungufu wa rasilimali watu katika sekta ya afya. Mimi niwashauri KCMC kutoa huduma za upasuaji kwa njia ya matundu kwa siku moja katika hospitali mbalimbali zilizopo katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini ili kutoa fursa kwa wananchi kupata huduma za upasuaji kwa karibu," alisema mkurugenzi huyo.

Katika mkutano huo wa wataalamu, Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Dk. Kondo Chilonga, alisema upasuaji wa njia ya matundu umeanza takribani miaka 15 iliyopita na kwamba hadi sasa wamefanikiwa kufanya upasuaji kwa njia ya matundu wagonjwa 150. Amesisitiza kuwa idadi ya wagonjwa hao iliyofikiwa ni ya mwaka mmoja na kuwa mpango huo umeweza kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa kukaa hospitalini kwa mufa mrefu.

Hata hivyo, baadhi ya wanafunzi wanaosoma masomo ya upasuaji kwa njia ya matundu KCMC, wameeleza kuwa elimu inahitajika zaidi kutolewa kwa jamii juu ya faida za kutumia upasuaji kwa njia ya matundu.

Wanafunzi hao wameeleza kwamba faida za upasuaji kwa njia ya matundu zinavyopunguza gharama na kupunguza maumivu kwa mgonjwa na hivyo kuondoa msongamano kwa wagonjwa wanaofanyiwa upasuaji katika hospitali hapa nchini.



Mjasiriamali Neema Moshi (kulia), akitengeneza mashada mbalimbali ya maua tayari kuwauzia wateja kwa shughuli mbalimbali za huduma ya mazishi eneo la Manispaa ya Moshi juzi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Migogoro ya ndoa yatikisa kwa miezi mitatu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAKATI robo ya kwanza ya mwaka ya Januari hadi Machi ikiwa imemalizika, migogoro ya ndoa katika eneo la Moshi Vijijini, mkoani Kilimanjaro 'imetia fora' kwa kuripotiwa mara nyingi zaidi katika Shirika la Wasaidizi wa Kisheria la Washemovi.

Hayo yamo katika ripoti ya huduma za msaada wa kisheria, elimu ya sheria na haki za binadamu iliyotolewa jana na shirika hilo katika mkutano wa wasaidizi wa kisheria Moshi Vijijini ambao uliwashirikisha wadau mbalimbali kutoka Idara za Maendeleo ya Jamii, Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi na Ustawi wa Jamii.

Akiwasilisha taarifa za kuongezeka kwa mashauri yanayohusu migogoro ya ndoa, ardhi, mirathi, matunzo ya watoto, madai unyanyasaji, ukatili dhidi ya wanawake, ubakaji, ulawiti, ukeketaji, utumwa wa ngono na shambulio la aibu, Mkurugenzi wa Shirika hilo la Washemovi, Kasira Kasira, alisema kesi nyingi zilizojitokeza zinahusu misuguano ya maslahi na mitazamo hasi katika ndoa.

"Mimi nawashukuru sana wenzetu wa Shirika la Kwieco kwa kutukutanisha na wadau hawa kujadili changamoto zinazotukabili, kutafuta utatuzi wa baadhi ya mashauri na kupeana uzoefu katika kushughulikia matatizo ya jamii inayotuzunguka.

Matatizo ya ndoa ni kama mlivyosikia," alisema.

Ofisa wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini wa Shirika la Kwieco ambalo ni walezi wa mashirika yote ya wasaidizi wa kisheria Mkoa wa Kilimanjaro, James Zacharia, wanategemea kujiimarisha katika baadhi ya changamoto zilizowasilishwa kwa kuhakikisha wanatengeneza uhusiano bora na wadau hao ili kufikia malengo ambayo wamejitengenezea na kuweza kufikia watu wengi zaidi.

"Jamani wasaidizi wa kisheria, moja ya majukumu yetu ni pamoja na kuhamasisha suala la uchukuaji wa mikopo ya uwezeshaji kiuchumi inayotolewa na kila halmashauri nchini, majukumu yetu sio tu kufundisha na kushughulikia migogoro ya ndoa, mirathi, umiliki wa mali na ukatili wa kijinsia.

Zaidi alisisitiza: "Watu watumie fursa mbalimbali ambazo zinajitokeza, ukimwelekeza yule mama pale kwenye kikundi kwamba kuna mikopo, halafu baadaye akaenda akapata ule mkopo, akashughulika, akafanya biashara, utakuwa umemsaidia kiuchumi na hata kama ana tatizo la kisheria inakuwa ni rahisi kufuatilia kwenda kupata haki yake kwa sababu atakuwa na nauli, ataacha chakula nyumbani kizuri, atafanya na huduma nyingine zitaenda vizuri, kuliko mtoto analalamika njaa na hana nauli ya kukufikia pale ofisini kwako, lakini bado unamhubiria akapate haki yake, ataipataje?

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Habiba Bomu, akizungumza na wasaidizi hao wa kisheria alisema wakati Serikali ya Rais Dk. John Magufuli ikijiandaa kuingia kwenye uchumi wa kati wa viwanda, halmashauri hiyo haitaki kuacha wanawake na vijana nyuma, kwa sababu wao ndio walezi wa familia sasa.

## Askari wasiofuata maadili wawashiwa taa nyekundu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Meja Jenerali Jackob Kingu, ameagiza Jeshi la Polisi kuwaondoa kazini askari polisi ambao watabainika kulichafua jeshi hilo kwa kuwanyanyasa raia, kushirikiana na wahalifu na kuwabambikia kesi wananchi.

Meja Jenerali Kingu aliagiza hilo jana, wakati wa hafla fupi ya makabidhiano ya jengo la kisasa litakalotumika kufundishia askari mambo mbalimbali ya uhalifu wa kimtandao.

Makabidhiano hayo kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani na Ubalozi wa China yalifanyika katika Shule ya Polisi Moshi (MPA).

"Askari yeyote atakayewabambikia kesi raia au kunyanyasa, RPC (Kamanda wa Polisi wa Mkoa) mwondoe kazini. Wako askari wanalichafua Jeshi la Polisi, hao hatutacheka nao," alisema Meja Jenerali Kingu.

Awali wakati wa makabidhiano hayo, Mwakilishi wa Balozi wa China nchini, Xu Chen, alimweleza Jenerali Kingu kuwa kazi waliyoifanya ilikuwa ni ujenzi wa majengo saba ya kisasa yatakayotumika kutoa mafunzo mbalimbali yakiwamo ya uhalifu wa kimtandao.

Aidha, mwakilishi huyo alisema ujenzi huo umegharimu kiasi cha Sh. bilioni 20.3

Katika makabidhiano hayo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini (IGP), Simon Sirro, alisema bado kumekuwa na changamoto katika makosa ya kimtandao kwa kuwa Watanzania wengi wameendelea kuibiwa kupitia mtandao.

"Bado tuna tatizo kubwa sana maana watu wetu wanaibiwa kwa njia ya mtandao, kwa hiyo jengo hili litatumika kufundishia askari masuala ya cyber crime (uhalifu wa kimtandao). Hapa ndipo tutakapowajengea uwezo askari wetu kupambana na wahalifu wa mtandao," alisema Sirro.



Ukurasa 18

EDWARD MORINGE SOKOINE AKUMBUKWA




Ukurasa 16

Teknolojia mawasiliano inavyoteka taaluma ya fedha kila kona nchini


# BUFE

Ijumaa Aprili 12, 2019

Nipashe

BIASHARA ... MI NA FEDHA




## SMZ; Marufuku mapambo ya pesa kwenye sherehe

Ukurasa 15



# Maprofesa Mbilinyi, Ngowi walipotathmini maudhui ya bajeti inayowafaa wanyonge

**Na Theodatus Muchunguzi**

WAKATI bajeti ya Taifa ya mwaka 2019/20 inatarajiwa kuwasilishwa bungeni Juni 16, makundi kadhaa katika jamii hususan ya watetezi wa usawa wa kijinsia, yameanza kuichambua na kufanyia tathmini, kuona kama itakuwa yenye kukidhi mahitaji ya makundi yote hususan ya wanyonge.

Tunapozungumzia wanyonge inamaanisha kuwa ni makundi ya pembezoni, wenye mahitaji maalum kama wanawake, watoto, wenye ulemavu na watu wanaoishi maeneo ya pembezoni; kwa lugha nyingine maskini.

Kutokana na hali hii, ni mategemeo ya wengi kwamba ili kuondoa changamoto zinazowagusa wanyonge wengi, bajeti hiyo ya Sh. trilioni 33.1 hainabudi kuandaliwa kwa kulenga kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo.

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

KIUCHUMI ZAIDI Ukurasa 19

Takwimu za Biashara Ukurasa 20

Muhtasari wa Soko

## Biashara

Jumla ya Mauzo (bln) 22,136.24

Mauzo 109,584,255.00
Hisa 58,317

### Kielezo

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 4,207.58 | +0.00 |
| DSEI | 2,296.50 | -37.11 |

**ZILIZOPANDA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| KA | 180 | -2.70% |
| JHL | 9,500 | +1.06% |
| SWIS | 3,760 | +7.43% |
| EABL | 5,320 | -1.66% |

**ZILIZOSHUKA**

| KAMPUNI | Bei | Badiliko% |
|---|---|---|
| TCCL | 1,200 | -11.76% |
| ACA | 5,550 | -2.63% |
| NMB | 1400 | -1.41% |
| NMG | 2,510 | -1.57% |
| KCB | 840 | +2.44% |

UCHUMI

# Maprofesa Mbilinyi, Ngowi wa maudhui ya bajeti inayowafaa

• Watetezi jinsia walia walichokubaliana hakijatekelezw

INATOKA UK.13

Tunategemea bajeti itakayoandaliwa, kuwasilishwa bungeni na kujadaliwa itasimamia haki za binadamu kwa kuwajali wanawake na kupunguza kama si kuondoa vifo vya wajawazito na watoto wachanga. Ni bajeti itakayowagusa watu wanaoishi na ulemavu, mabinti, watoto wachanga na wazee. Tunategemea itatoa fedha na ruzuku zitakazojibu changamoto hizo. Aidha, itajenga mabweni ili mabinti wawe na haki ya kusoma na kulindwa dhidi ya wabakaji.

**MDAHALO WA TGNP**

Wiki iliyopita nilihudhuria jumuiko jijini Dar es Salaam ambalo jopo na wasomi na watatezi wa usawa wa kijinsia walichambua na kufanya tathmini kuhusu bajeti jumuishi, ambayo inazingatia usawa wa kijinsia.

Katika mdahalo huo ulioandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ziliainishwa changamoto mbalimbali zinazoendelea kuwa vikwazo kwa makundi ya wanyonge, jambo linalodhihirisha kuwa bado bajeti ya Taifa inayoandaliwa kila mwaka haijawa jumuisho; kwa maana ya kutokidhi mahitaji ya wanyonge.



Prof. Marjorie Mbilinyi.



Prof. Honest Ngowi.

Kwa mtazamo wake, Prof. Marjorie Mbilinyi, mambo yote muhimu yaliyobainishwa katika mpango wa maendeleo endelevu yanapaswa kuingizwa katika bajeti yenye mlengo wa kijinsia kwa lengo la kubomoa mfumo dume na kuleta udawa wa kijinsia.

Prof. Mbilinyi anaona kuwa inahitajika bajeti ambayo itakomboa nguvu kazi ya wanawake na wasichana, akisema wasichana wadogo wamegeuka kuwa wafanyakazi wa ndani wa kutunza watoto bila kuwa na elimu, uzoefu. Hivyo, anaeleza kuwa njia ya kuwakomboa wasichana na wanawake ni kuwapa elimu.

"Tutatumiaje rasilimali zetu kujenga mabweni kwa ajili ya wasichana, ili wasikatishwe masomo kwa kubakwa na baadaye kunyimwa fursa ya kuendelea na masomo," anasema na kuongeza:

"Tubomoe child labour (kazi za utotoni), ndoa za utotoni na kuweka mfumo rasmi wa uchumi ili kila mtu abaki na heshima ya kuutunza mwili wake."

> **"Je, sera zetu za bajeti tunazifanya kuwa shirikishi. Je, tunashirikisha katika kuongeza keki ya taifa na katika kugawana?**

Swamwely Mkatwa, mchambuzi wa sera kutoka asasi ya Actionaid, anasema kodi ndicho chanzo kikuu cha mapato, hivyo fedha zitokanazo na kodi hizo zipelekwe kutoa huduma kwa mujibu wa mlengo wa kijinsia na kodi hiyo ugawiwe sawa.

Mkatwa anaona kwamba ili kuhakikisha kuwa kodi ya wananchi inanufaisha watu wote na kwamba serikali iwajibishwe kwa sababu kodi ni ya wananchi, hivyo iangalie mlengo wa kijinsia.

Kwa upande wake Prof. Honest Ngowi, anaiona bajeti shirikishi kuwa ni inayoangalia katika matumizi kama makundi yote yanalengwa; kwa maana kila mmoja anapata anachotarajia kupata.

"Tunapaswa kuangalia mapato kwanza kwa mfano, kama watu wote wanaostahili kulipa kodi wanalipa, bila hivyo tukikopa tutarajue mzigo wa madeni (deni la taifa) litakua, huduma zitakosekana," anaeleza na kuhoji:

"Je, sera zetu za bajeti tunazifanya kuwa shirikishi. Je, tunashirikisha katika kuongeza keki ya taifa na katika kuigawana?"

Lilian Liundi, Mkurugenzi Mtendaji wa TGNP, anabainisha kwamba ulifanyika utafiti ambao ulibainisha ngawo wa rasilimali haukidhi mlengo wa kijinsia, hivyo ukafanyika uhamasishaji kwa kushirikiana na serikali na wafadhili kuhusiana na bajeti yenye mlengo wa kijinsia mwaka 2008, ambao sera, mipango na programu zilizingatiwa serikalini.

Kwa mujibu wa Liundi, ni masikitiko kwamba baadaye serikali ilionekana kutochukua hatua kosonga mbele kwa mfano, akitoa mfano ilipofika mwaka 2010, mambo ya jinsia yalibakia kwenye wizara

moja (Afya, Maendeleo ya Jam
Wazee na Watoto), badala ya kuv
ya wizara nyingi kwa ni suala mt

Anasema, ni hali iliyosababis
dhi ya nchi jirani za Rwanda na
zilizokuja kujifunza nchini, kwe
kasi na kuiacha nyuma Tanzan
suala la bajeti, yenye mlengo wa

Anaongeza kuwa mwaka 2015-
ionekana mageuzi kutokana na
kuongeza masuala ya jinsia kati
ingawa utekelezaji wake haujaw
ridhisha.

Licha ya Wizara ya Fedha na
kuandaa kitini cha bajeti ya kiji
der bajeti manual), lakini Liundi
kilibaki katika karatasi.

Licha ya changamoto hiyo, bad
anaeleza matumaini ya kupatika
yenye mlengo wa jinsia. Anase
sasa kuna hali chanya kutokana
semi (Ofisi ya Waziri MKuu Ta

BIASHARA

**Teknolojia mawasiliano inavyoteka taaluma ya fedha kila kona nchini**

Ukurasa 16

UCHUMI

**EDWARD MORINGE SOKOINE ALIVYOKUWA KATIKA ZAMA ZAKE ZA 'HAPA KAZI TU'**

Ukurasa 18

BIASHARA

**Ushirika wa kwanza wa wafugaji, sasa wakwepa mgogoro malisho**

Ukurasa 19


# lipotathmini
# wanyonge

wa



ii, Jinsia,
wa ndani
ambuka.
sha baa-
. Uganda
nda kwa
ia katika
kijinsia.
2016 yal-
a serikali
ka bajeti,
a wa ku-

Mipango
sia (gen-
anasema

lo Liundi
na bajeti
ma, kwa
na Tami-
awala za

Mikoa Serikali ya Mitaa), kwa kuungana mkono na TGNP na Shirika la Chakula Duniani (WFP), ambalo liko chini ya Umoja Mataifa.

Anafafanua kiwapo msukumo mkubwa, ikiwamo kuandaliwa kwa kitini cha bajeti ya kijinsia, ili kuanza kutumika katika ngazi ya wilaya.

**MWELEKEO WA BAJETI**

Kuhusu mwelekeo wa bajeti ijayo ya mwaka 2019/20, Prof. Ngowi anatathmini kwamba haitakuwa tofauti na zile za miaka miwili iliyopita, ambazo zilijiekeleza katika miundombinu na miradi mikubwa.

Anasema, kwa kiasi kikubwa itakuwa ya uchaguzi, kwa kuwa mwaka huu, kuna uchaguzi wa serikali za mitaa na mwakani ni uchaguzi mkuu. Anaeleza mtazamo wake:

"Ni fursa, ni wakati wa kudai zaidi. Wakati wa uchaguzi wanasiasa hujipendekeza kwa wananchi, hivyo kuwapo kodi ndogo, chache kwa lengo la kuwafurahisha wananchi."

Kwa upande mwingine, Prof. Ngowi na Mkwata wana mawazo yanayofanana, kwamba ili kuwapo bajeti ya kutosha inayoweza kukidhi mahitaji ya wengi wakiwamo wanyonge, kuna haja kwa serikali kupanua wigo wa makusanyo ya mapato kwa kuacha kodi za mazoea kama vinywaji na sigara, badala yake ijielekeze katika kampuni kubwa, sambamba na kufuta misamaha ya kodi ambayo ni mzigo kwa wananchi.




Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, akionyesha bungeni, begi lenye hotuba ya bajeti. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**JICHO LA TAMISEMI**

Dennis Londo, kutoka Tamisemi, anaeleza kuwa serikali ina dhamira ya dhati kuhakikisha rasilimali zinaelekezwa katika utoaji huduma kwa watu wote.

Anafafanua kuwa, kwa sasa serikali inachukua hatua kadhaa kuzirekebisha athari zilizosababishwa na masharti ya nchi wafadhili, hususan ya kuwataka wananchi kuchangia huduma za jamii ambazo zilikuwa zikitolewa bure na serikali.

Londo anatoa mfano wa elimu bila ya malipo kwa shule za msingi na sekondari, imepunguza athari ya watoto wa kike waliokuwa wakishindwa kwenda shule, badala yake waliajiriwa kufanya kazi za ndani, majumbani.

Anasema kutokana na hatua hiyo katika sura chanya kwa waathiriwa, kwamba hivi sasa kuna malalamiko kuwa wasichana wa kufanya kazi za ndani wameadimika, hali inayotoa ujumbe kwamba wengi wako bado wako shuleni.

Kadhalika, anataja kushuka kodi za viwanja na majengo kutaiwezesha serikali kupata kidogo, lakini pia wananchi wananufaika kwa kutoa kiasi kidogo cha fedha.

Mengi yalizungumzwa katika mdahalo huo, lakini jambo la msingi ni kufanyika ufuatiliaji ili kuhakikisha yanapewa kipaumbele katika mipango na utekelezaji wa bajeti.

Kuna baadhi ya halmashauri zimeanza angalao kutenga bajeti kwa ajili ya taulo za kike kwa ajili ya wanafunzi. Pia hatua ya serikali ya kufuta kodi kwa taulo za kike katika bajeti ya mwaka huu (2018/2019).

Kwa mwaka ujao wa fedha 2019/2020 bila shaka serikali itakuwa imeyazingatia mahitaji ya msingi ya makundi ya wanyonge kama uwezeshaji (mikopo), miundombinu (mabweni), kuongeza bajeti ya kilimo ambacho ni tegemeo kubwa kwa wanawake pamoja na barabara katika maeneo ya kuingia kwenye masoko.

# SMZ; Marufuku mapambo ya pesa kwenye sherehe



**Na Salma Said,** Zanzibar

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imepiga marufuku matumizi ya fedha za noti kwenye mapambo ya harusi na sherehe nyingine. Ni baada ya kuibuka taarifa juu ya kikundi kinachotengeneza fedha bandia.

Maofisa waandamizi kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BOT) na Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib, Ayoub Mohammed Mahmoud, wamesema marufuku kutengeneza pesa bandia na kuwa ni lazima kila mtu athamini pesa za nchi kwa kuzingatia matumizi sahihi kwa sababu ni tunu ya taifa.

Pamoja na kuwa baadhi ya watu wasio waaminifu hutengeneza fedha bandia na kuzisambaza kwa matumizi, lakini kumeibuka tabia hivi karibuni ya kutumia fedha hizo za noti.

Inadaiwa wanazitumia kama mapambano kwa kushonea nguo, makoti, khanga, na kuzigandisha kwenye meza, jambo ambalo limeonekana kama ni kushindana na kutambiana.

Kwa mujibu wa sheria ya Tanzania, mtu yeyote, bila mamlaka, kwa kunuwia anaeharibu, anayechana, anayekata au vinginevyo inatumika kihalali, atakuwa anatenda kosa na anaweza kukuhumiwa au kutozwa faini.

Pia, Sheria ya SMZ, inapiga marufuku, mambo hayo pia ikitaja kuiyeyusha au kuibandika alama au kuiwekea jina au maneno au alama, ina adhabu tofauti, ikiwemo kifungo.

Kutokana na kuonekana bado matumizi sahihi ya fedha hayapo sawia, Benki Kuu inasema imeanza kufundisha matumizi sahihi ya fedha kwa maofisa wa serikali na wananchi wa ngazi mbali mbali. **DW**



**BEI YA MAZAO** >> MCHELE 184375/- | ULEZI 142642.9/- **FEDHA** >> RAND 164.66 | KSH 22.75 | USH 0.61

UCHUMI

# Teknolojia mawasiliano inavyoteka taaluma ya fedha kila kona nchini

- ATM, simu zachuana ufanisi wa kuhudumia
- Mapya ya 'Tigo Pesa App' kusalimisha fedha

**Na Mwandishi Wetu**

KADRI miaka inavyoenda, kuna mabadiliko makubwa yanaendelea nchini katika mustakabali wa uchumi ukipiga hatua kubwa.

Hapo katika sekta ya fedha, kuna mageuzi makubwa yanayoshuhudiwa katika sekta ya fedha na hasa teknolojia ya mawasiliano ya habari, ikijikita zaidi katika matumizi ya simu za mkononi. Jamii inafikiwa kila kona na hasa katika maeneo ambayo huduma za kibenki hayajafikiwa.

Kadri kunavyoshuhudiwa mageuzi hayo, kila asasi na hasa benki na kampuni za simu ambazo sasa zimeibuka kuwa mdau mkubwa wa biashara za fedha, zimepiga hatua kubwa.

Ni wastani wa miongo mwili tu iliyopita, ripoti za taasisi hizo za fedha, zilitawaliwa kwa njia ya maandishi, huku kiwango cha mawasiliano yake yakitawaliwa na mfumo wa analoingia, ikiwemo katika benki.

Lakini ghafla, mageuzi makubwa yanayofanyika duniani, sasa yameleta sura mpya katika mfumo wote wa fedha umezaa tija yenye sura nne kuu, ambazo ni: Usahihi, haraka, salama na huduma nyingi kama vile malipo kwa njia ya 'ATM' na mitandao ya simu.

Katika eneo hilo la mitandao ya simu ambayo inashika kasi zaidi, huduma za kuhifadhi, malipo na mikopo rahisi imezidi kutanuka, huku kukiwapo maendeleo makubwa ya ufanisi, hasa katika suala la malipo.

Ni moja ya maeneo yanayotiliwa mkazo, kupitia vyombo mbalimbali vya elimu na asasi za kiserikali, likiwemo jukwaa la ufundi nchini (Costech).

Ikiwa ni mwendelezo wa elimu hiyo, Nipashe inayapata kutoka kwa watendaji wa kampuni ya simu ya Tigo, inaeleza hatua inayochukuliwa katika eneo la maboresho hayo ya kiteknolojia, ambazo kitaalamu zinaitwa 'Application' kazi zake ni nyingi zikiwemo usalama na ubora wake.

Jerome Albou, Ofisa Mkuu wa Kitengo cha Ufundi, wa kampuni ya Tigo, anasema usalama kwa watumiaji wa huduma za kifedha kwa njia mpya ya simu anayoitambulisha kwa jina 'Tigo Pesa App,' kwamba inasaidia kuharakisha miamala ya kifedha, huku ikiwa rahisi kutumia.

Albou anasema, ni mfumo uliotengenezwa kwa namna rafiki na rahisi kila mtumiaji nchini. Anafafanua: "Tunasikiliza na kupokea maoni yanayotolewa na watumiaji na huwa tunachukua maoni pamoja na mapendekezo yanayotolewa na watumiaji 'App' hii na kuyaongezea kwenye mapitio ya kila mwezi.

"Tumekuwa tukikidhi mahitaji ya matarajio ya wateja wetu, kwa namna ambayo wanataka mitandao yetu ya kijamii," anasema na kuongeza:

" Pia, inatoa mchango mkubwa kuongeza uelewa kuhusiana na 'App' hii na kuwezesha kuiweka katika nafasi nzuri, huku tukiendeleza utamaduni wa kidigitali na kujenga ubunifu wa bidhaa zetu, kama ailivyo kawaida ya kampuni."



Moja ya wakala wa simu za mkononi, mjini Moshi. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

> **"Ili kumrahisishia mteja kutuma kwenye namba sahihi, tunamwonyesha jina la anayetaka kumtumia kabla ya kutuma.**


Jerome Albou, Ofisa Mkuu, Kitengo cha Ufundi na Taarifa kampuni ya simu Tigo: **NA MPIGAPICHA WETU.**



Huduma za ATM.

### USALAMA JE?

Kuhusu usalama wa mfumo huo wa kiufundi, Albou anasema, imewekwa kiufundi, katika namna inayohakikisha taarifa zote za mtumiaji zinabaki salama, dhidi ya hujuma au kuingiliwa kwa namna yoyote, kupata taarifa hizo au kufanya muamala pasipo ruhusa ya mtumiaji.

Pia, anadokeza umuhimu wa mtumiaji kuhakikisha anaziweka taarifa zake salama, dhidi ya uwezekano wa kuingiliwa na mtumiaji mwingine, huku bosi huyo wa ufundi akitetea mfumo wake una kinga na usalama, wenye uhakikia wa ithibati ya kimataifa, inayotambulika kama 'GSMA' na 'ISO.'

"Kwa upande mwingine, pia tunafuatilia 'App' hii saa 24 kila siku ili kubaini majaribio yoyote ya hujuma au uhalifu kufanywa na tunapogundua uhalifu umefanyika, tunachukua hatua kwa kuongezea usalama zaidi," anasema.

"Mbali na usalama eneo lingine analolitaja kuwa 'Tigo Pesa Apps' ni rafiki kwa mtumiaji ni kile anachokifatsiri " inapatikana muda wote kwa njia tofauti" akitoa mifano mbalimbali.

Albou anaeleza nafasi ya mtumiaji wa kampuni yake ya simu, akitumia kauli: "Anapotaka kutuma pesa anaweza kutumia majina ambayo yapo kwenye simu yake, pasipo kulazimika kuandika namba pembeni."

Anataja mustakbali huo, mbali na mtu mmoja mmoja, pia kuna njia za malipo ya simu na televisheni.

### INAPOKOSEWA JE?

Alipotakiwa na Nipashe kufafanua namna panapotokea makosa, Albou anasema, wanayarekebisha katika njia kuu mbili za malipo kurudisha fedha, wadau husika wanatumia njia mbili, moja ikiwa katika mfumo wa kawaida na nyingine katika mfumo wa malipo wa 'Tigo Pesa App'kwa kuzizuia zisitolewe na mtu aliyemtumia kwa makosa.

"Pesa zinaweza kurudishwa baada ya aliyetumiwa kukubali kuzirudisha kwa aliyemtumia kimakosa. Hata hivyo, ni muhimu kwa mteja kuhakikisha anakuwa makini anapotuma pesa kwa kuhakikisha namba anayotaka kuitumia pesa ni sahihi.

"Ili kumrahisishia mteja kutuma kwenye namba sahihi, tunamwonyesha jina la anayetaka kumtumia kabla ya kutuma. Endapo ataona jina ni sahihi, anaingiza namba yake ya siri, ikiisha anatuma," anasema.

Anasema, huduma hiyo haifanyi kazi katika maeneo yasiyokuwa na mtandao wa intaneti kwa sababu za kiusalama, lakini ikitumika ambako kuna mtandao wa simu hiyo na hakuna 'kifurushi' husika, bado aina hiyo ya simu hizo ina njia mbadala iitwayo 'zero rated' akimaanisha haitozi gharama yoyote.

"Inaweza kufanya kazi kwenye mitandao mingine ya intaneti ikiwa ni pamoja na 'Wifi' lakini, kwa sababu za kiusalama, utahitajika kuweka neno la siri litalothibitisha kuwa wewe mtumiaji ndiyo mmiliki halali na ndiye anayetumia 'Tigo Pesa App' kufanya muamala," anasema Albou

Huku akitumia tafsiri za kitaalamu, ofisa huyo wa ufundi, anahitimisha kuwa ni huduma zinazopatikana katika mifumo ya aina nyingi za simu ambazo zinaangukia huduma azozitaja za 'IOS.'

# Biashara katika picha


Wakazi wa jiji wakichagua nguo za mitumba katika soko la Ilala, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**


Mchuuzi wa mito akisaka wateja kando ya Barabara ya Mandela, eneo la Buguruni jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Mto aliuza kwa bei ya 5,000/-. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**


Muuza pipi akiwa 'ameuchapa' usingizi wakati akisubiri wateja katika eneo la shule ya msingi Daimond, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

BEI YA MAZAO >> MAHINDI 52625/-| MAHARAGE 170000/-

AGOSTI 1938 - APRILI 1984

# EDWARD MORINGE SOKOINE ALIVYOKUWA KATIKA ZAMA ZAKE ZA 'HAPA KAZI TU'

**Na Peter Orwa**

HAYATI Edward Sokoine ni mtu mwenye historia kubwa kwa nchi. Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alikuwa kipenzi chake, akiwa na historia ya kipekee. Siku ya kifo chake ni tarehe kama ya leo, ambayo Rais Nyerere ni miongoni mwa waliopata simanzi kubwa.

Ilikuwa mwaka 1984, majira ya asubuhi nilimshuhudia mwalimu wetu katika shule ya sekondari ya bweni iliyoko kijijini kwenye baridi na unyevu wa mvua kama zinazoendelea sasa nchini, Johnson Mwakikali, katika sura ya upole na yenye huzuni kubwa.

Huku akiwa amekumbatia redio yake ya mkononi, ukali wake aliuweka kando akifuatilia kwa karibu taarifa redioni. Nasi wanafunzi tukajongea alikosimama, tusidadisi kulikoni redioni? Ndipo tukasikia sauti ya Rais Nyerere, akitangaza taarifa ya kifo hicho.

Sisi tukaingia kwenye huzuni na mijadala ya mino'ngono, hali kadhalika walimu na ndicho kilikamata taifa zima kwa wakati huo, kila mahali kukazizima. Ni ishara tosha kwamba alikuwa kipenzi wa wakubwa na wadogo, isipokuwa mashabiki wa wizi, dhuluma na maovu.

Ni msiba uliompata Mwalimu Nyerere kwa kumgusa mtendaji wake mkuu serikalini, uliomuumiza kisaikolojia, huku ikimkatisha bashasha ya maandalizi ya saa 24 mbele, kuadhimisha siku ya kuzaliwa kwake kijijini Butiama,.

Kwanini nchi ilizizima kwa kifo hicho? Sokoine ana sifa nyingi. Inajumuisha uzalendo, uchapakazi, makini na mtu anayedai matokeo ya kweli katika utendaji wake, kwa maana ya kufanya ufuatiliaji wa kila alichokitekeleza au kuahidiwa.

Hata kifo chake, alikuwa safarini akitokea akiwa kwenye safari ya gari eneo la Dakawa Morogoro, akitokea Bungeni Dodoma kuelekea Dar es Salaam. Sababu kuu ya kutumia barabara, ilikuwa haja ya kukagua ustawi wa mazao shambani, lakini bahati mbaya uwanda wa mauti ukampata.

Dhana ya ubora wa utendaji na umahiri wa kufuatilia mambo, nilibahatika kupata ushuhuda kwa marehemu Mzee Geofrey Mhagama, ambaye ana simulizi kubwa ya uchapakazi wa Sokoine, binafsi akajifunza muundo mpya wa utendaji serikalini.

Anasema, akiwa naibu waziri katika wizara mpya iliyoanzishwa mwanzoni mwa miaka ya 1970, Sokoine alimfunza kufanya kazi kwa mipango, udhibiti na ufuatiliaji makini.

Kwa mujibu wa Mzee Mhagama, alijikuta anaingia katika tabia na utaratibu wa kuandika kila jambo



Gari alilopatia ajali Edward Sokoine (picha ndogo kulia)





Mnara wa kumbukumbu katika eneo alikopata ajali marehemu Edward Sokoine, wilayani Mvomero, Morogoro.

> **Mwaka 1970, alipandishshwa, akishika nafasi ya uwaziri wa nchi na miaka miwili, 1972, baadaye aliteuliwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa.**

la kikazi, ikiwamo ahadi wanazopewa kazini na namna ya kufuatilia matokeo yake, ili asiponyokwe na 'umakini' na 'ufuatiliaji.'

Anasema, kuna wakati alishangazwa alipoitwa na bosi wake, Waziri Sokoine, aliyemuuliza matokeo aliyopata kutokana na ahadi walizopewa kote walikopita, ikiwamo zile alizodhani ni 'blabla'za ziarani, jambo lililomfanya anyanyuke ofisini mara moja, kwenda kufuatilia majibu ya ahadi hizo.

Mbali na nafasi katika Baraza la Waziri, Mhagama alikuwa mbunge wa Songea na baadaye alikuwa mkuu wa wilaya katika maeneo tofauti nchini na katika maisha yake ya ustaafu, alihitimshia na uenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoa Ruvuma, kabla ya umauti wake wastani wa muongo mmoja sasa.

Ikirejewa hata katika vita dhidi ya uhujumu uchumi, ufisadi na rushwa, ilityofungiliwa mahakama yake maalum ya uhujumu uchumi, msukumo unaoendeshwa na serikali iliyoko madarakani sasa, ina wasifu wote wa kupokea kijiti cha kazi nzuri iliyoanzia ngazi ya awamu ya kwanza na kupitia awamu nyinginezo.

Miongoni, inajumuisha hatua ya maboresho ya kisheria; huduma za kipolisi kuhamia Taasisi ya Kuzuia Rushwa (Takuru), iliyoboreshwa zaidi kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru).

Vivyo hivyo, huduma hiyo ya polisi ilisafiri hadi kuanzishwa Tume ya Kudhibiti Dawa za Kulevya, iliyopitia hatua sasa kuwa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya.

Mambo hayo yote na yale ambayo leo hii yana ubatizo wa 'ufisadi' huko nyuma yalibeba jina la asili la 'uchumu uchumi' katika hilo, Waziri Mkuu Sokoine, anakumbukwa sana alivyopambana katika nafasi ya utendaji mkuu wa serikali.

Bado kumbukumbu imebaki, kwamba mwanzoni mwa miaka 1980, anakumbukwa ukamanda wake kupitia kioo cha 'Vita ya Uhujumu Uchumi' ambayo hadi leo imebaki mfano wa kuigwa na kwa kiasi kikubwa, kinachofanyika sasa katika vita hivyo, kinashabiliana na matendo ya zama za Sokoine.

**HISTORIA YAKE**

Sokoine, alizaliwa Agosti Mosi ya mwaka 1938, huko Monduli mkoani Arusha, Ilipofika mwaka 1948 alianza elimu ya Msingi kwao Monduli na baadaye akafaulu darasa la nane, akachaguliwa kuendelea katika Shule ya Sekondari Umbwe, iliyoko Moshi, alikohitimu mwaka 1958

Mwaka 1961, ambao nchi ilipata uhuru, ikiwa ni miaka mitatu baada ya kumaliza shule na alijiunga na chama cha TANU na mwaka mmoja baadaye, alipata fursa ya kwenda mafunzoni nchini Ujerumani, alikohitimu mafunzo ya miaka miwili mwaka 1963.

Baada ya kurudi masomoni, aliteuliwa kuwa Ofisa Mtendaji wa Wilaya ya Masasi na ndipo akagombea na kupitishwa ubunge kwao. Hapo ndipo neema ilimfungukia, akiteuliwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Usafirishaji na Kazi.

Mwaka 1970, alipandishshwa, akishika nafasi ya uwaziri wa nchi na miaka miwili, 1972, baadaye aliteuliwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, alikoendelea kudumu hata katika baraza lingine la mawaziri, baada ya uchaguzi wa mwaka 1975.

Pia, wakati huo mwaka 1977, ikiwa imeanzishwa CCM, aliteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati Kuu ya chama hicho, huku akipanda zaidi kuwa Waziri Mkuu, alikodumu hadi mwaka 1981 na kisha akateuliwa tena katika nafasi hiyo, mwaka 1983, hadi kifo chake, siku kama ya leo miaka 34 iliyopita.

Wasifu huo wa maisha ya marehemu Sokoine, haishangazi kuona leo hii ni Siku ya Taifa, mahali alikofia kunajengwa mnara maalum wa kumbukumbu na Chuo Kikuu cha Kilimo Mrgoro, kilichoanzia kuwa kitivo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, sasa ni Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine (SUA), sekta 'iliyomkosha' marehemu Sokoine, hata kifo chake kilikuwa katika mazingira ya kukagua maendeleo ya kilimo nchini.

**FEDHA >>** USD 2,300.96| Pauni 3,011.73| Euro 2,595.25

UCHUMI

MATEBETE

# Ushirika wa kwanza wa wafugaji, sasa wakwepa mgogoro malisho

- Yamvutuia Dk. Kamani, aahidi kuwa nao
- Waiweka sawa Mbarali vs Hifadhi Ruaha



Mwenyekiti wa Tume ya Ushirika nchini Dk. Titus Kamani (kulia), akizungumza na baadhi ya watoto wa kijiji cha Matebete, wilayani Mbarali, Mbeya wakati alipoenda kuzungumza na wanachama wa ushirika wa wafugaji. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

**Na Nebart Msokwa,** MBARALI

MBARALI ni miongoni mwa wilaya nchini, zinazokabiliwa na uharibifu wa mazingira, katika miaka ya hivi karibuni, kutokana na shughuli za kibinadamu ikiwamo ufugaji holela.

Kabla ya mwaka 2007, idadi kubwa ya mifugo iliyoingizwa wilayani humo mkoa wa Mbeya, ilitokea mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mara, Singida na kwingine kunakojishughulisha na ufugaji, hali iliyosababisha kuharibiwa vibaya kwa bonde la Ihefu, lenye ardhi oevu.

Hiyo inatajwa kuwa chanzo kikuu cha Mto Ruaha Mkuu, kupungua kwa kiasi kikubwa, hali iliyochangia serikali kuanza kutafuta mbinu za kuyanusuru mazingira hayo

Mwaka huo, serikali iliendesha operesheni ya kuondoa mifugo hiyo na kuipeleka maeneo mengine yaliyokuwa na malisho ya kutosha, ikiwamo mikoa ya Lindi na Mtwara, ili eneo hilo libaki na mifugo iliyoendana na uwezo wa malisho. Baada ya kupunguzwa, mifugo iliendelea kuongezeka na kuharibu mazingira kutokana na wafugaji wengi kutumia njia ya ufugaji wa kuhama, kutafuta malisho na maji.

Pia ufugaji wa aina hiyo, umesababisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji pamoja na migogoro kati ya wafugaji hao na Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, kutokana na wafugaji kuingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi.

Baadhi ya wafugaji wa wilaya hiyo, wamekuwa wakikerwa na uharibifu wa mazingira, pamoja na migogoro ya kila mara, inayosababishwa na ufugaji wao wa kuhama, hivyo kuanza kubuni njia za kuondokana na matatizo hayo.

Wafugaji jamii ya Kimasai waliopo katika Kijiji Cha Matebete kilichopo katika Kata ya Chimala, ni miongoni mwa makundi ya wafugaji yaliyoamua kubuni mbinu za kuondokana na tatizo hilo.

**WABORESHA MALISHO**

Mwenyekiti wa Kijiji hicho, Julius Tisho, anasema kijiji hicho kina ukubwa wa hekta 32,000 zilizotengwa na wilaya hiyo, kwa ajili ya wafugaji, ili kuepuka mwingiliano na wakulima wa vijiji jirani, hali iliyopelekea migogoro.

Anasema kijiji hicho kinakaliwa na wafugaji zaidi ya 3500, ambao kwa ujumla wana mifugo zaidi ya 5000 na kwa sasa wana mpango wa kupunguza mifugo hiyo, ili ibaki 5000 pekee, itakayoendana na eneo lao la ufugaji.

> **“Tunajua wapo watu waliokuwa wakinufaika na jasho lenu, hawatapenda kuona mnaungana na kuwa na nguvu, hivyo wataanzisha chokochoko...**

Tisho anasema, ili kuepuka ufugaji wa kuhama ambao unaharibu mazingira na kusababisha migogoro, wameamua kuboresha malisho ya mifugo yao, kwa kuchimba kisima kirefu kwa ajili ya kunywesha mifugo na hata matumizi yao wenyewe.

Anasema wameamua kufanya hivyo, ili kuepuka mifugo yao kwenda kutafuta maji kijijini Igumbilo, ambacho wamekuwa wakiingia kwenye migogoro isiyokuwa ya lazima.

“Ufugaji wa kuhamahama, umekuwa ukituletea matatizo kwa kuingia katika migogoro na wenzetu wakulima, lakini pia tumegundua kuwa ufugaji wa aina hiyo unachangia kwa kiasi kikubwa kuharibu mazingira, hivyo tunataka mifugo yetu isitoke nje ya kijiji chetu,” anasema Tisho.

Vilevile, mwenyekiti huyo anaeleza kuwa wafugaji hao, pia wana mpango wa kupanda nyasi katika maeneo yao, kwa ajili ya mifugo na kwamba watakuwa wanamwagilia kwa kutumia maji hayo waliyochimba.

Anasema, walishapata utaalamu wa kuboresha malisho kutoka kwa wafugaji wenzao wa nchi jirani ya Kenya na kwamba, watatumia mbinu hizo katika kuboresha malisho hayo.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Sitengas Satullo, anasema mradi huo umegharimu zaidi ya Sh. milioni 50, zilitokana na michango ya wafugaji na baadhi ya wadau.

Anasema, mradi umehusisha uchimbaji kisima kirefu na kutengeneza birika la kunyweshea mifugo kwenye vituo mbalimbali, ndani ya maeneo ya malisho yao.

Vilevile, Satulo anasema mbali na mpango ya kuyatumia maji hayo ya kunywesha mifugo, pia wanakusudia kuyatumia majumbani pamoja na kuboreshea malisho kwa kuwagilia nyasi.

Anasisitiza kuwa mradi utawasaidia zaidi kipindi cha kiangazi, ambacho nyasi hukauka na kusababisha mifugo kukosa malisho na kwamba, hali hiyo husababishia mifugo afya mbaya.

Satulo, anaishukuru serikali kwa kuwawezesha wafugaji hao kumiliki kisheria eneo hilo kwa kuwapimia eneo na kuwapatia hati miliki, walio nayo hadi sasa pamoja na kuipiga chapa mifugo yao.

**WAUNDA USHIRIKA**

Katika kuimarisha umoja wao na kuhakikisha wanatimiza azma yao ya kufuga kisasa kwa kuachana na mfumo wa kuhama hama, wafugaji hao wameanzisha chama cha ushirika wa wafugaji, wanaodai kitasaidia umoja wao.

**INAENDELEA UK.20**

# Takwimu za Biashara

Na Edward Ntwale & Elias Samweli

Bei ya Mazao Ya Chakula kwa Sh/kilo 100 Aprili 1, 2019

| Mkoa | Arusha | D'Salaam | Dodoma | Geita | Morogoro | Kagera | Kilimanjaro | Kigoma | Lindi | Manyara |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mahindi | 57000 | 70000 | 53000 | 57000 | 48000 | 60000 | 40000 | 45000 | 80000 | 60000 |
| Mchele | 200000 | 210000 | 195000 | 130000 | 165000 | 185000 | 180000 | 160000 | 200000 | 200000 |
| Mtama | 40000 | 60000 | 35000 | 180000 | 71000 | 100000 | 80000 | 100000 | 150000 | 42000 |
| Uwele | 40000 | 60000 | 34000 | 180000 | 71000 | 110000 | NA | 100000 | NA | 100000 |
| Ulezi | 72000 | 140000 | 75000 | NA | 155000 | 150000 | 180000 | 150000 | 200000 | 120000 |
| Ngano | 87000 | 130000 | 160000 | 180000 | 163000 | NA | 98000 | 150000 | NA | 120000 |
| Maharage | 150000 | 220000 | 170000 | 170000 | 185000 | 150000 | 180000 | 140000 | 200000 | 130000 |
| Viazi Mviringo | 70000 | 80000 | 66000 | 70000 | 82000 | 75000 | 50000 | 90000 | 100000 | 60000 |

## Mwenendo wa Shilingi




## Mafuta

Bei : Kuanzia Machi 6, 2019

| MKOA | DSM | Arusha | Pwani | Dodoma | Geita | Iringa | Kagera (Bukoba) | Katavi | Kigoma | Moshi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Petroli | 2,098 | 2,191 | 2,102 | 2,157 | 2,263 | 2,162 | 2,313 | 2,306 | 2,329 | 2,181 |
| Dizeli | 2,131 | 2,195 | 2,135 | 2,189 | 2,296 | 2,195 | 2,346 | 2,339 | 2,362 | 2,185 |
| M'Taa | 2,096 | 2,286 | 2,101 | 2,155 | 2,262 | 2,161 | 2,312 | 2,304 | 2,328 | 2,276 |

## Soko la Hisa la Dar es Salaam Kikao cha Aprili 10, 2019

### Muhtasari

| | | |
|---|---|---|
| TSI | 3,482.64 | -0.36 |
| DSEI | 2,088.34 | +20.35 |
| Thamani za Hisa (bln) | 20,129.19 | |
| Mauzo | 61,389,100.00 | |
| Hisa | 157,800 | |

### Zilizopanda na Zilizoshuka

| Kampuni | Bei | Badiliko |
|---|---|---|
| DSE | 1,260 | -3.08% |
| KA | 130 | +8.33% |
| EABL | 4,720 | +1.29% |
| JHL | 9,250 | +1.65% |
| ACA | 6,200 | +3.33% |

### Viwango vya kubadilisha

| Fedha | Nunua | Uza |
|---|---|---|
| EUR | 2,591.28 | 2,617.65 |
| USD | 2,268.07 | 2,290.76 |
| KES | 22.38 | 22.56 |
| GBP | 2,947.82 | 2,977.52 |

### Bei za hisa hadi kikao cha Aprili 10, 2019

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| ACA | 6,200.00 | 6,000.00 | 3.33 |
| CRDB | 125 | 125.00 | 0 |
| DCB | 340 | 340 | 0 |
| DSE | 1,260 | 1,300 | -3.08 |
| EABL | 4,720.00 | 4,660.00 | 1.29 |
| JHL | 9,250.00 | 9,100.00 | 1.65 |
| KA | 130.00 | 120.00 | 8.33 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| KCB | 1,020.00 | 1,020.00 | 0 |
| MBP | 490.00 | 490.00 | 0 |
| MCB | 500.00 | 500.00 | 0 |
| MKCB | 800.00 | 800.00 | 0 |
| MUCOB | 400.00 | 400.00 | 0 |
| NICO | 170.00 | 170.00 | 0 |
| NMB | 2,340.00 | 2,340.00 | 0 |

| Kampuni | Bei ya mwisho | Bei Iliyopita | Ba'liko % |
|---|---|---|---|
| NMG | 1,400.00 | 1,400.00 | 0 |
| PAL | 400.00 | 400.00 | 0 |
| SWALA | 490.00 | 490.00 | 0 |
| SWIS | 1,700.00 | 1,700.00 | 0 |
| TBL | 11,400.00 | 11,400.00 | 0 |
| TCC | 17,000 | 17,000.00 | 0 |
| TCCL | 600.00 | 600.00 | 0 |

## VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA

| FEDHA | KUNUNUA | KUUZA |
|---|---|---|
| KENYA SHS | 2,256.52 | 2,274.57 |
| UGANDA SHS | 57.08 | 61.16 |
| RWANDAN FRANC | 251.72 | 254.76 |
| BURUNDI FRANC | 218.12 | 219.77 |
| USD | 227,817.82 | 230,096.00 |
| POUND STG | 298,076.84 | 301,172.65 |
| EURO | 256,864.59 | 259,525.28 |
| CANADIAN $ | 170,867.64 | 172,524.56 |
| SWITZ. FRANC | 227,817.82 | 230,004.00 |
| JAPANESE YEN | 2,049.27 | 2,069.58 |
| SWEDISH KRONOR | 24,600.50 | 24,838.46 |
| NORWEG. KRONOR | 26,791.38 | 27,043.39 |
| DANISH KRONOR | 34,416.17 | 34,755.08 |
| AUSTRALIAN $ | 162,639.14 | 164,311.55 |
| INDIAN RPS | 3,294.66 | 3,327.37 |
| PAKISTAN RPS | 1,532.23 | 1,620.39 |
| ZAMBIAN KWACHA | 18,639.64 | 18,984.82 |
| MALAWIAN KWACHA | 289.92 | 309.04 |
| MOZAMBIQUE-MET | 3,537.54 | 3,567.38 |
| ZIMBABWE $ | 42.63 | 43.49 |
| SDR | 316,559.70 | 319,725.29 |
| GOLD (T/O) | 296,807,961.10 | 299,868,999.49 |
| S. AFRICAN RAND | 16,317.81 | 16,469.19 |
| UAE DIRHAM | 62,028.38 | 62,636.72 |
| SINGAPORE $ | 168,417.11 | 170,013.30 |
| HONK KONG $ | 29,066.55 | 29,356.09 |
| SAUD ARABIAN RIAL | 60,746.56 | 61,352.39 |
| KUWAIT DINAR | 749,006.52 | 756,223.09 |
| BOTSWANA PULA | 21,460.44 | 21,859.12 |
| CHINESE YUAN | 33,921.15 | 34,252.20 |
| MALAYSIA RINGGIT | 55,497.64 | 55,984.43 |
| SOUTH KOREA WON | 200.46 | 202.11 |
| NEWZEALAND | 153,708.68 | 155,337.81 |

## Interbank Foreign Exchange Market (IFEM)

| Tarehe | Idadi (Mn USD) | Juu | Chini | Wastani |
|---|---|---|---|---|
| **10/Apr/2019** | **1.65** | **2,310.00** | **2,298.50** | **2,300.96** |
| 9/Apr/2019 | 1.30 | 2,310.00 | 2,298.40 | 2,300.92 |
| 8/Apr/2019 | 1.25 | 2,310.80 | 2,298.45 | 2,300.93 |
| 5/Apr/2019 | 1.50 | 2,311.00 | 2,298.60 | 2,300.97 |

## Inter-bank Local Money Markets

| Tarehe | Kiasi (million-TZS) | Juu | Chini | Wastani (WAR) |
|---|---|---|---|---|
| **10/Apr/2019** | **43,300** | **6.00** | **4.90** | **5.18** |
| 9/Apr/2019 | 40,100 | 5.50 | 4.90 | 5.04 |
| 8/Apr/2019 | 31,500 | 5.50 | 4.90 | 5.12 |
| 5/Apr/2019 | 17,500 | 6.00 | 5.00 | 5.06 |
| 4/Apr/2019 | 49,000 | 5.50 | 4.75 | 5.02 |
| 3/Apr/2019 | 37,500 | 6.00 | 4.75 | 5.20 |

# Ushirika wa kwanza wa wafugaji, sasa wakwepa mgogoro malisho

Mwenyekiti wa ushirika huo, Philipo Kinei, anasema wametenga ekari 10,000 kwa ajili ya nyanda za malisho na kati ya hizo, wametenga ekari 1000 kwa ajili ya kuanzisha mashamba darasa na kuanzisha majani lishe ya mifugo.

Anasema, wanatarajia kuyatimiza hayo kufuatia namna watakavyoshauriwa na wataalamu ili kuhakikisha wanatekeleza kitaalamu na miradi yao inakuwa endelevu.

"Lengo letu ni kuhakikisha tunaachana kabisa na ule ufugaji wa kizamani uliokuwa unatuingiza kwenye migogoro, kutokana na kwamba tulishaanza mipango mikubwa muda mrefu hatukupata shida kuanza ushirika maana kila kitu kilikuwepo," anasema Kinei.

Anasema ushirika huo utakuwa unazalisha na kuuza maziwa katika maeneo mbalimbali kulingana na masoko yatakayokuwapo.

### WAPATA WAFADHILI

Kufuatia maendeleo yanayofanywa na wafugaji hao pamoja na mipango waliyonayo baadhi ya mashirika na taasisi mbalimbali za serikali zimeanza kuwatembelea na kuonyesha nia ya kuwasaidia ili wafanikishe malengo yao.

Mojawapo ni shirika la Heifer International Tanzania kupitia mradi wake wa uendelezaji sekta ya maziwa (EADD,) ambalo hivi karibuni liliwatembelea na kuahidi kuwasaidia kuwapelekea wataalamu ambao watawaandalia mipango kazi mizuri.

Meneja wa mradi huo wa EADD, Mark Tsoso, anasema ili wafugaji wafanikiwe, wanatakiwa kusaidiwa utaalamu utakaowafanya wasiyumbe na kuhakikisha mipango yao ifanikiwe.

Kaimu Msajili wa bodi hiyo, Jeremiah Temu, anasema ushirika huo utakuwa na manufaa makubwa kwa wafugaji, hivyo anawasisitiza waulinde.

"Tunajua wapo watu waliokuwa wakinufaika na jasho lenu, hawatapenda kuona mnaungana na kuwa na nguvu, hivyo wataanzisha chokochoko ili msambaratike, hivyo ni jukumu lenu kuulinda," anawaasa Temu.

### WAMSHUKURU JPM

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji Wilaya ya Mbarali, Moses Fute, anamshukuru Rais Dk. John Magufuli, kwa kusitisha uondoaji wa zaidi ya vijiji 360 vilivyodaiwa kuwa ndani ya hifadhi mbalimbali nchini.

Fute anasema, wafugaji wa Mbarali ni miongoni mwa makundi yaliyoathiriwa na uondoaji vijiji 32, kwa agizo la Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Anasema, ni muda mrefu wafugaji walilalamika kuhusu tangazo la serikali la mwaka 2008, linalowaondoa wafugaji na wakulima kwenye maeneo yao ya asili.

Anasema ushirika wa wafugaji ni miongoni mwa njia za kuondoa migogoro isiyokuwa ya lazima na kuwafanya wawe na sauti wakati wa kushughulikia maslahi yao.

### MWENYEKITI WA TUME

Mwenyekiti wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Dk. Titus Kamani, anafanya ziara mkoa wa Mbeya na alifika katika kijiji cha Matebete kwa ajili ya kuongea na wafugaji hao.

Anawataka wafugaji kuendelea kuungana na kuimarisha ushirika, ili kuwavutia wadau wanaoweza kuwasaidia kuimarisha na kufanya uwe na manufaa zaidi kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Dk. Kamani anasema Ushirika wa Wafugaji wa Matebete ndio wa kwanza nchini kuanzishwa, hivyo amewaahidi kuisaidia kumarika, ili uwe mfano kwa wafugaji wa maeneo mengine.

"Wafugaji wa baadhi ya maeneo wanakuwa na mawazo kwamba serikali ndio yenye jukumu la kuwapatia maeneo kwa ajili ya ufugaji na wasipopewa wanaanza kuhama hama hali ambayo inapelekea uharibifu wa mazingira sasa ninyi mmekuwa mfano," alisema Dk. Kamani.

Aidha alisema kitendo cha wafugaji kuhamahama na kuharibu mazingira, kinawafanya waonekane ni maadui wa kila wanakoenda, hivyo akawataka wafugaji wa maeneo mengine waende kujifunza Matebete.



# Diwani wa CCM ashikiliwa polisi kwa kudaiwa mauaji

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

DIWANI wa Kata ya Lusungo (CCM) katika Halmashauri ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, Veronika Kanyanyila, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kupanga njama na kumuua mwanamke anayefahamika kwa jina la Oliva Kyusa (57), kwa sababu ya wivu wa mapenzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, Veronica Kanyanyila, anatuhumiwa kuhusika na mauaji hayo kwa sababu alikuwa anamtuhumu marehemu kuwa na mahusiano ya kimapenzi na mume wake Alfred Mwankenja, hivyo kusababisha ugomvi wa mara kwa mara.

Kamanda Matei alisema marehemu, Oliva Kyusa mkazi wa kitongoji cha Lukwego, aliuawa nyumbani kwake kwa kupigwa na kitu butu kichwani.

Matei alifafanua kuwa tukio hilo lilitokea April 9 , majira ya saa sita usiku, ambapo marehemu alivamiwa na watu watatu waliokuwa wamefunika sura zao kwa kuvaa kofia aina ya mizura.

Alisema marehemu alikuwa akiishi na mume wa mtuhumiwa aitwaye Alfred Mwankenja (60) ambaye naye katika shambulio hilo alijeruhiwa kwa kuvunjwa mkono wa kushoto na wauaji hao.

"Mtuhumiwa Veronica alikuwa anamtuhumu mara kwa mara marehemu kwamba kumchukulia mume wake na kuishi naye jambo ambalo lilizua ugomvi na kumshambulia kwa kipigo," alisema Kamanda Matei.

Kamanda Matei alisema upelelezi wa mauaji hayo unaendelea ikiwa ni pamoja na msako mkali wa kuwasaka wale wote waliohusika na tukio hilo.

Katika tukio lingine Matei alisema wamekamata mabelo 14 ya mitumba ya nguo za ndani zilizopigwa marufuku kuingizwa nchini.

Alisema mabelo hayo yaliingizwa nchini kinyemela yakitokea nchi jirani ya Malawi na yalifichwa kwenye nyumba ya Hezron Mwakalinga, ili kusafirishwa na kwamba juhudi za kuwatafuta watuhumiwa kwa hatua zaidi za kisheria zinaendelea.



Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa Halotel, Mhina Semwenda, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, katika uzinduzi wa huduma mpya iliyoboreshwa iitwayo Tomato Plus ambayo inamwezesha mteja kuongea bure dakika tano za mwanzo mitandao yote. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji Feleshi atoa maagizo mazito kwa mahakimu

**Na Mwandishi Wetu,**
MBEYA

JAJI Kiongozi Dk. Eliezer Feleshi amewataka viongozi wa mahakama wanaotafsiri haki na sheria kutembelea magereza mbalimbali nchini, ili kujiridhisha kama kuna watoto wanaokinzana na sheria wameongezewa umri ili kutumikia kifungo wakiwa na watu wazima.

Jaji Feleshi alitoa kauli hiyo mkoani Mbeya wakati wa ziara yake ya kikazi ya kuangalia utendaji kazi wa Mahakama ya Watoto, ambapo aliwataka viongozi kutembelea magereza ili kubaini masuala mbalimbali ambayo yanawahusu watoto waliokinzana na sheria.

Alisema miongoni mwa masuala ambayo yanatakiwa kufanyiwa kazi ni kuangalia umri wa watoto waliopewa adhabu ya kutumikia vifungo katika magereza ya watu wazima.

"Jaji Mfawidhi, Hakimu Mkazi Mfawidhi na wengine jengeni utaratibu wa kutembelea magereza zetu na utaratibu huu utasaidia kubaini masuala mbalimbali ikiwamo uchepushaji na watoto ambao wameongezewa umri ili kupata sifa ya kuingizwa kwenye magereza za watu wazima alisema," Jaji Feleshi.

Alisema kwa mujibu wa Sheria ya Watoto, mtoto haruhusiwi kuchanganywa gereza moja na watu wazima, pia suala la mtoto kuwekwa kizuizini ni hatua ya mwisho kwa kuwa anaweza kupewa dhamana.

Naye Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Robert Makaramba, alishauri kuanzishwa kwa Mahakama ya Watoto na familia ili kuondoa changamoto ya ukinzani kwa baadhi ya sheria.

Jaji Makaramba alisema sheria ya mtoto inakinzana na sheria ya mirathi, hivyo kusababisha watoto wanaozaliwa nje ya ndoa kukosa haki zao.

Katika taarifa yake Hakimu Mfawidhi wa Mahakama ya Watoto Mbeya, Zawadi Laizer, alisema tangu mahakama hiyo ianzishwe mwaka 2017, jumla ya kesi za madai 29 na jinai 31 zilifunguliwa na kwamba hadi sasa kuna mashauri saba tu ambayo yote yana umri wa chini ya miezi sita.

# Ujenzi wa hospitali kukamilika Septemba

**Na Grace Mwakalinga,**
MBARALI

SERIKALI ya Wilaya ya Mbarali mkoani Mbeya, imewahakikishia wananchi kuwa ifikapo mwezi Septemba, mwaka huu, ujenzi wa hospitali ya wilaya utakamilika na kwamba wataanza kupata huduma bora za matibabu.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Kivuma Msangi, aliyasema hayo juzi alipofanya ziara pamoja na wataalamu kwa lengo la kukagua ujenzi. Msangi alisema ifikapo mwezi Septemba mwaka huu, hospitali hiyo itaanza kutoa huduma mbalimbali za matibabu ambazo zitatolewa kwenye mazingira bora ukilinganisha na ilivyo sasa ambapo kuna changamoto ya uhaba wa vifaa tiba na majengo ya kutolea huduma.

"Tumejipanga kuwa kufika mwezi Septemba hospitali mpya ya wilaya itaanza kutoa huduma katika mazingira bora yenye vifaa tiba vya kutosha, wataalamu na miundombinu mingine ya afya ili wananchi wafurahie huduma, lakini ili tufikie hatua hiyo kila mwananchi kwa nafasi yake awe sehemu ya kukamilisha ujenzi huu," alisema Msangi.

Mkuu wa Idara ya Ujenzi wilayani humo, Abbas Kitalima, alisema awamu ya kwanza walipokea jumla ya Sh. bilioni 1.5, kutoka Serikali Kuu ambazo zitakamilisha ujenzi wa majengo saba mapya sambamba na ukamilishaji wa jengo la ghorofa moja ambalo litatumika kwa shughuli za utawala pamoja na kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje (OPD) na kufanya jumla ya majengo tisa yanayohitajika.

Kitalima aliongeza kuwa kwa sasa ujenzi wa majengo hayo yote yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi na yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba mwaka huu.

Wataalamu waliotembelea mradi wa ujenzi huo, walimshauri Mhandisi Kitalima pamoja na kamati mbalimbali zilizoundwa kwa ajili ya usimamizi, kuongeza kasi ujenzi ili wananchi waanze kupata huduma na kuhakikisha ubora wa majengo unazingatiwa.

Majengo yanayojengwa mpaka sasa ni pamoja na wodi ya wazazi, maabara, mashine za mionzi (X-Ray), dawa za chanjo, kufulia nguo, ghala la dawa, mifumo ya umeme pamoja na ukarabati wa jengo la ghorofa moja ambalo litatumika kwa ajili ya wagonjwa wa nje pamoja na shughuli za utawala.





# Wizara yaandaa kanuni kupambana mifuko ya plastiki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WIZARA ya Muungano na Mazingira imeandaa kanuni rasmi zitakazotumika katika kuwawajibisha watakaoendelea kutumia au kutengeneza mifuko ya plastiki baada ya muda wa katazo kuisha.

Hayo yamesemwa juzi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, Januari Makamba, kufutia serikali kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya plastiki ifikapo Juni 1, mwaka huu.

Makamba alisema maamuzi yaliyotolewa na Waziri Mkuu ya kupiga marufuku matumizi ya mifuko hiyo, siyo ya kushtukiza kwa kuwa tayari serikali ilishirikisha wananchi pamoja na wadau mbalimbali.

Alisema baada ya serikali kupiga marufuku ya mifuko hiyo wizara yake tayari imeshaandaa kanuni ambazo zitatumika kusimamia katazo hilo la serikali juu ya matumizi ya mifuko ya plastiki.

"Tayari tumeshaandika kanuni za katazo hili lililotolewa na Waziri Mkuu na tayari tushazipeleka kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG) na baadaye zitaletwa ili kuanza kutumika," alisema Makamba.

Aidha, alisema kuwa kanuni hizo zitaeleza adhabu ambazo zitatumika wakati ambao mtu atabainika kutengeneza, kutumia au kusambaza mifuko hiyo iliyopigwa marufuku.

"Kanuni hizi zimeweka adhabu kwa watengenezaji pamoja na watumiaji kulingana na kosa, pia kanuni hizo zitaonyesha ni aina gani ya vifungashio havija pigwa marufuku na havitahusika katika kanuni hizo," alisema Makamba.

Alisema baadhi ya vifungashio vya plastiki vya dawa, vyakula kama vile maziwa, mifuko ya pembejeo na mbegu zinazotumika kwenye kilimo pamoja na chupa za plastiki havitahusika na kanuni hizo. Aliongeza kuwa kanuni hizo zitaundiwa kikosi kazi cha kuzisimamia, ambapo wajumbe wake watatoka katika maeneo mbalimbali ikiwamo Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) pamoja na Uhamiaji.

Alisema wajumbe wengine ni Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TAA), Shirika la Viwango nchini (TBS), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA), Polisi, Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na taasisi zingine.

"Kwa hawa watu wa TAA wao watakuwa na jukumu la kutoa matangazo katika vyombo vyao vya usafiri wa anga kuwatangazia abiria kuwa wanapoingia katika viwanja vyetu vya ndege kutoka nchi nyingine wasije na mifuko ya plasitiki," alisema.

Alisema kuwa serikali tayari imeshafanya utafiti na kujiridhisha kuwa upatikanaji wa mifuko mbadala ipo ya kutosha kwa kuwa walishakutana na wazalishaji ambao walikuwa wanasubiri katazo la serikali ili kuanza kuzalisha kwa wingi.

"Suala la mifuko mbadala ipo ya kutosha kwa kuwa wapo tayari wazalishaji na wengine walikuwa wanasubiri tu tangazo la serikali waanze kuzalisha kwa wingi au kuingiza mitambo, kwa nchi kama Kenya na Rwanda ambao wao walishapiga marufuku matumizi ya mifuko hii wanaitegemea kutoka hapa Tanzania, hivyo sisi hatutapata shida juu ya hili," alisema.



Waziri wa Madini, Doto Biteko (wa pili kulia) na Naibu Waziri wa Madini, Stanslaus Nyongo (kulia), wakimsikiliza Mwenyekiti wa Chama Cha Wafanyabiashara wa Madini Tanzania (Tamida), Sam Mollel (kushoto), wakati kikao hicho, kati ya waziri na viongozi wa chama hicho, jijini Dodoma juzi. Wengine wanaofuatilia ni Kamishna wa Madini, David Mulabwa na mmoja wa wajumbe wa chama hicho, Abe Latif. **PICHA: WM**

# Serikali yazitaka taasisi za utafiti kujiamini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imeitaka Bodi ya Taasisi ya Utafiti Mifugo Tanzania (TALIRI) kufanya utafiti wa kitaifa ili kuondoa dhana kwamba wenye uwezo wa kufanya kazi hiyo ni taasisi za kimataifa.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, wakati akifungua bodi hiyo jijini Dodoma.

Alisema bodi hiyo inatakiwa kwenda kufanya mabadiliko ili sekta ya mifugo ikue tofauti na ilivyo sasa.

"Naomba mkajikite kwenye utafiti wa kitaifa, tunahitaji kupata matokeo chanya," alisema Mpina.

Alisema lengo ni kuzionyesha taasisi nyingine ambazo hazina mpango wa kufanya utafiti za ndani ya nchi. Waziri Mpina alisema lengo ni kuona wanakwenda vizuri ili kuiaminisha jamii kuwa wanaweza.

Alisema Tanzania ni nchi ya pili Afrika kuwa na mifugo mingi, lakini uzalishaji wa maziwa bado upo katika kiwango cha chini, jambo ambalo halileti picha nzuri.

Alifafanua kuwa pamoja na Tanzania kuwa na mifugo mingi, lakini malisho mazuri yapo kwa hivyo kwanini tushindwe na nchi jirani kama vile Kenya katika uzalishaji.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Utafiti Mafunzo na Ugani, Dk. Angelo Mwilawa, alisema bodi hiyo iko kikazi na kuhakikishia kuwa italeta matokeo chanya katika utafiti wake. Dk. Mwilawa alisema wanafurahi kuzinduliwa kwa bodi hiyo, huku akisema watashirikiana na wizara hiyo kuhakikisha wanaleta tija kwa taifa.

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Sebastian Chenyembuga, alisema kuteuliwa kwao kutaleta manufaa makubwa kwa wananchi.

Alisema walihitaji bodi hiyo na wameipata na kuhakikisha wanaitendea haki nafasi hiyo ili kuleta matokeo chanya.

# NMB yamwaga madawati shule mbili

**Na Renatha Msungu,** ITIGI

BENKI ya NMB imezitaka shule mbalimbali nchini kutunza misaada ya madawati inayoyatoa kwa ajili ya kuzisaidia ili kuinua elimu nchini.

Hayo yalisemwa na Meneja wa Benki ya NMB Kanda ya Kati, Nsolo Mlozi, wakati wa mwendelezo wa utoaji wa msaada wa madawati katika shule mbili za Mjini Mpya na Pentagon zilizopo Itigi mkoani Singida.

Madawati 100, yalitolewa kwa shule hizo ambayo yanagharimu Sh. milioni 10, ambapo kila shule itapata madawati 50.

Alisema NMB imeamua kushirikiana na serikali ya awamu ya tano katika suala zima la kuinua elimu ikiwamo utoaji wa msaada wa madawati.

Alisema wanafanya hivyo kwa sababu wanajua umuhimu wa elimu ndio maana benki yao iko mstari wa mbele kugawana faida na wananchi kwa kutoa msaada wa madawati.

"Tunaomba mtunze haya madawati kwa sababu wengine watakuja kuyatumia," alisema Mlozi.

Alisema NMB imejiwekea malengo ya kusaidia maeneo ya elimu, afya, mafunzo ya kutunza fedha pamoja na kilimo ambapo napo kuna dawati la kusaidia kipengele hicho.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Itigi, Doreen Lutahanamilwa, aliishukuru NMB kwa msaada huo, huku akiahidi kuyatunza madawati hayo.

Alisema msaada huo utasaidia kutatua changamoto kubwa ya madawati iliyokuwa ikiwakabili kwa muda mrefu.

"Tunaomba NMB isichoke kuziangalia shule za halmashauri yetu kwa sababu zina uhaba wa madawati, tunaziomba na taasisi zingine ziige mfano huu wa kusaidia jamii," alisema Doreen.



## HABARI ZANZIBAR



Mchoraji kutoka Tingatinga Arts, Agnes Mpate, akimwonyesha picha ya kuchora Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya NMB, Albert Jonkergouw (wa pili kulia), wakati wa kongamano la wafanyabiashara wanachama wa Klabu ya Biashara ya NMB Ilala, lililofanyika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: NMB**

# Miche minazi sasa kusambazwa nchi nzima kuongeza uzalishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi inakusudia kusambaza miche ya minazi 100,000 katika kipindi cha mvua za masika ili kuimarisha na kurudisha hadhi ya zao la nazi Zanzibar ambalo hivi sasa uzalishaji wake umepungua.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Misitu na Mali zisizorejesheka, Soud Mohamed, wakati akizungumzia mikakati ya kuotesha miche ya mazao mbalimbali katika kipindi cha mvua za masika ambazo zimeanza kunyesha.

Alisema zao la minazi limeshuka uzalishaji wake kwa sababu mbalimbali ikiwamo ukataji wa miti hiyo kwa ajili ya matumizi ya mbao na shughuli za ujenzi.

Aidha, alisema miti hiyo inaendelea kupunguwa kwa kiwango kikubwa kutokana na kasi ya ujenzi katika maeneo ya vijijini ambapo mtu hulazimika kukata mnazi ili kupata nafasi ya kujenga.

"Wizara ya Kilimo Maliasili imejipanga vizuri kuotesha jumla ya miche ya minazi laki moja ambayo itapandwa huko katika shamba la serikali Selem," alisema.

Alisema wizara inatarajiwa kusambaza miche ya mikarafuu milioni moja ili kuimarisha zao hilo.

Mkuu wa vitalu vya Idara ya Kilimo, Khadija Mohamed Said, alisema tayari miche ipo na kwa sasa inasubiri kusambazwa kwa wakulima.

Aliitaja baadhi ya miti ambayo pia itasambazwa kwa wakulima ni ya matunda kama miembe kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa matunda hayo.

Alieleza kwamba miche hiyo inatarajiwa kusambazwa katika mashamba ya serikali pamoja na wananchi kwa ujumla.

# Jamii yatakiwa kulea watoto ngazi ya familia

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Ustawi wa Jamii, Wahida Maabadi, ameitaka jamii kuacha kuwapeleka watoto katika vituo vya kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu badala yake walelewe na familia zao.

Alisema serikali imesitisha kupokea watoto hao katika vituo vya kulelea watoto, ili watoto wapate malezi mazuri kutoka kwa familia zao.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maendeleo ya mradi wa malezi mbadala unaotekelezwa katika kisiwa cha Tumbatu Mkoa wa Kaskazini Unguja, alisema vituo vya malezi ya watoto siyo suluhisho la mwisho kwa kuwa mtoto anatakiwa kupata matunzo kutoka kwa wazazi wake.

Aliitaka jamii kujenga utamaduni uliokuwapo zamani katika kusaidia malezi ya mtoto wa mwezio.

"Serikali imepiga marufuku wazazi kuwapeleka watoto katika nyumba za kutunza watoto kwa sababu mwelekeo wa serikali ni kuona jamii inawajibika na jukumu la kutunza matunzo ya watoto katika familia," alisema.

Alizitaka familia zilizofaidika na mradi wa malezi mbadala huko Tumbatu kujituma na kuhakikisha watoto wanapata matunzo vizuri na malezi ikiwamo kuhudhuria shule na kufuatilia mwenendo wa masomo yao.

Naye Mratibu wa mradi wa malezi mbadala unaoendeshwa na Shirika la Kimataifa la Watoto Wanaoishi katika Mazingira Magumu (SOS), Nyezuma Simai, alizitaka familia zinazofaidika na mradi huo kuhakikisha kwamba wanafuatilia vizuri mwenendo wa watoto ikiwamo maendeleo ya elimu.

Alisema yapo mafanikio makubwa katika mradi huo tangu kuanza, lakini juhudi zaidi zinahitajika kwa wazazi katika kufuatilia mwenendo wa watoto wao. "Wapo wazazi katika mradi huu bado hawawajibiki vizuri ikiwamo kufuatilia mwenendo mzima wa watoto katika mahudhurio ya shule," alisema.

# Chama cha ADC chamwangukia Rais Magufuli

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

KATIBU Mkuu wa Chama cha Alliance for Democratic Change (ADC), Doyo Hassan Doyo, ameemwomba Rais John Magufuli, kuacha kudhibiti vyama vya siasa kufanya kazi za kisiasa bali awadhibiti wanasiasa wakorofi.

Akitoa taarifa kwa waandishi wa habari juu ya maandalizi ya mkutano mkuu wa chama hicho, alisema taarifa aliyoitoa rais ya kuwa vyama vya siasa vinavyoruhusiwa kufanya mikutano ya hadhara ni vile vyenye wabunge na madiwani ni kauli inayoziba haki za wasiokuwa na hatia.

Alisema chama chao hakina mbunge wala diwani, lakini kwa mujibu wa katiba kinaruhusiwa kufanya kazi za kisiasa.

Akizungumzia kuhusu maandalizi ya mkutano mkuu wa chama hicho, alisema madhumuni ya kufanya mkutano mkuu Zanzibar ni kuhuisha historia ya mapambano ya kisiasa na kiuchumi.

Alisema katika mkutano huo wanachama wa chama hicho watapiga kura ya kuwachagua viongozi ambao watakiongoza chama hicho.

"Mfumo wa chama ni kufanya uchaguzi ili kuwapa fursa wanachama wengine kuweza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwa maslahi ya chama," alisema.

Alieleza kuwa mkutano huo utafanyika Aprili 14, mwaka huu na watazindua mpango mkakati wa chama hicho ambao utajulikana kwa jina la ADC kaya kwa upande wa Bara na kwa upande wa Zanzibar ADC Shehia.

Alisema mpango huo utazaa matunda na kuweza kufanikiwa kuchukua ushindi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020.

Aidha, alisema katika mkutano huo pia watafanya marekebisho katika baadhi ya vipengele vya katiba ya chama hicho ambavyo vina upungufu.

Alisema miongoni mwa vipengele vya katiba hiyo ambavyo vitafanyiwa marekebisho ya kipengele cha ulinzi na usalama cha katiba ya chama hicho.

Naye Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho, Queen Cuthbert Sendinga, aliwataka wanawake wa chama hicho kuwa mstari wa mbele katika kuwania nafasi za uongozi.

Alieleza kuwa katika kuhakikisha wanawake wanakuwa na ushiriki mzuri katika kuwania nafasi za uongozi ndani ya chama hicho, kitaendelea na utaratibu wa kutoa elimu kwa vijana na wanawake na kuwajengea uwezo wa kuwa viongozi bora.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 8 April**
06:00 Al jazera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 9 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 10 April**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 11 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 12 April**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Iljimae
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Iljimae
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 13 April**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Iljimae
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Night of terror
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 14 April**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Series rpt: Iljimae
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 8 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Kesho Leo
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 9 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 10 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Documentary
22:00 Kipindi Maalum: Tatu mzuka
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 11 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Elininyo
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Elininyo
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Kipindi Maalum: TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Riziki
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 12 April**
05:30 Uwanja wa Ma0zoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: Tanesco
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi rpt
13:45 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
13:55 Habari za saa
14:00 Kipindi Maalum: Kesho leo rpt
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Shamba shape up
19:00 Uchumi na biashara
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 13 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Elininyo
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 14 April**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Illegal sisters
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Illegal sisters 2
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)









## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# TANGAZO

# International Commercial Bank (Tanzania) Limited.

**ISSUED PURSUANT TO REGULATIONS 7 AND 8 OF THE BANKING AND FINANCIAL INSTITUTIONS (DISCLOSURES) REGULATIONS, 2014**

## EXTRACT FROM AUDITED FINANCIAL STATEMENTS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2018

| | 2018 TZS '000 | 2017 TZS '000 |
|---|---|---|
| **Assets** | | |
| Cash and balances with Bank of Tanzania | 16,545,098 | 15,258,459 |
| Balances with other banks | 11,972,632 | 2,420,918 |
| Cheques in the course of collection | 441,010 | 318,015 |
| Placements with other banks | 10,374,852 | 15,622,361 |
| Loans and advances | 53,296,307 | 50,276,963 |
| Government securities held to maturity | 17,612,624 | 32,778,598 |
| Other assets | 172,548 | 502,358 |
| Property Plant and Equipment | 730,136 | 400,622 |
| Leasehold improvements | 27,165 | 42,280 |
| Intangible assets | 275,206 | 356,730 |
| Tax receivable | 457,827 | 451,327 |
| Deferred tax asset | 865,156 | 659,759 |
| **Total Assets** | **112,770,562** | **119,088,389** |
| **Liabilities** | | |
| Deposits from banks | 12,338,458 | 19,330,258 |
| Deposits from customers | 78,821,287 | 77,973,813 |
| Other liabilities | 569,657 | 546,790 |
| **Total Liabilities** | **91,729,402** | **97,850,860** |
| **Equity** | | |
| Issued capital | 20,025,247 | 20,025,247 |
| Accumulated losses | (1,825,461) | (2,392,549) |
| Regulatory reserve | 2,841,374 | 3,604,831 |
| **Total Equity** | **21,041,160** | **21,237,529** |
| **Total Liabilities and Equity** | **112,770,562** | **119,088,390** |
| **Selected Financial Condition Indicators** | | |
| Total issued capital to total assets | 18% | 17% |
| Non-performing loans to total advances | 10% | 9% |
| Gross Loans to total deposits | 60% | 55% |
| Loans to total assets | 47% | 42% |

### STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOME FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

| | 2018 TZS '000 | 2017 TZS '000 |
|---|---|---|
| Interest income | 8,922,176 | 9,872,439 |
| Interest expenses | (3,498,714) | (4,056,843) |
| **Net interest income** | **5,423,462** | **5,815,596** |
| Fees and commission | 968,931 | 950,452 |
| Foreign currency translation | 181,213 | 96,419 |
| Other operating income | 387,599 | 304,114 |
| **Operating income** | **6,961,204** | **7,166,581** |
| Recoveries made during the year | 364,471 | 559,406 |
| **Total operating income** | **7,325,675** | **7,725,987** |
| Impairment losses on loans and advances | (1,093,390) | (1,505,949) |
| impairment on other risk assets | (307,511) | (33,506) |
| **Total impairment** | **(1,400,902)** | **(1,539,455)** |
| **Net operating income** | **5,924,774** | **6,186,532** |
| **Operating expenses** | | |
| Personnel expenses | (2,300,728) | (2,259,821) |
| Depreciation and amortization | (349,040) | (488,519) |
| Other operating expenses | (3,563,262) | (3,164,406) |
| **Total operating expenses** | **(6,213,030)** | **(5,912,746)** |
| **Profit/ (loss) before tax** | **(288,256)** | **273,786** |
| Income tax (expense)/credit | 91,896 | (87,810) |
| **Profit/ (loss) for the year** | **(196,360)** | **185,975** |
| **Other comprehensive income** | - | - |
| **Total comprehensive income/ (loss) for the year** | **(196,360)** | **185,975** |
| **Selected Financial Performance Indicators** | | |
| Return on total assets | -0.17% | 0.16% |
| Return on Equity | -0.93% | 0.88% |
| Non-interest income to net interest income | 28.35% | 23.2% |
| Operating expenses to total assets | 5.51% | 5.0% |
| Interest margin to average earning assets | 6.67% | 5.9% |
| Non-interest expense to gross income | 59.40% | 52.7% |

### STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

| | 2018 TZS '000 | 2017 TZS '000 |
|---|---|---|
| **Cash flow from operating activities** | | |
| Profit before tax | (288,256) | 273,786 |
| **Adjustments for** | | |
| Impairment of loans and advances | 1,093,390 | 1,505,949 |
| Impairment of other risk assets | 307,511 | 33,506 |
| Depreciation of property and equipment | 204,360 | 216,917 |
| Amortisation of leasehold improvements | 38,577 | 151,786 |
| Amortisation of intangible assets | 106,103 | 119,816 |
| Gain on asset disposal | (1,290) | - |
| Foreign exchange gain | (181,213) | 96,419 |
| **Cash flows from operating profits before working capital changes** | **1,279,182** | **2,398,179** |
| **Changes in operating assets and liabilities:** | | |
| Statutory Minimum reserve | 1,515,788 | 1,139,839 |
| Loans and advances | (4,112,735) | 282,014 |
| Government securities held to maturities over 90 days | 15,215,987 | 2,133,450 |
| Other assets | 22,299 | (66,045) |
| Deposit from banks | (6,991,800) | 734,467 |
| Deposits from customers | 847,474 | 4,845,346 |
| Other liabilities | 22,858 | (137,507) |
| **Net cash inflows from/(used in) operating activities** | **7,799,053** | **11,329,743** |
| Tax paid | (120,000) | (210,000) |
| **Net cash inflows from/(used in) operating activities** | **7,679,053** | **11,119,743** |
| Additions to leasehold improvements | (23,462) | - |
| Proceeds from assets disposal | 1,290 | - |
| Purchase of property and equipment | (533,875) | (85,178) |
| Purchase of intangible assets | (24,579) | - |
| **Net cash used in investing activities** | **(580,626)** | **(85,178)** |
| **Increase/(decrease) in cash and cash equivalents** | **7,098,427** | **11,034,565** |
| **Foreign exchange gain** | **181,213** | **(96,419)** |
| Cash and cash equivalents at the beginning of the year | 40,781,927 | 29,843,781 |
| Cash and cash equivalents at the end of the year | **48,061,567** | **40,781,927** |

### STATEMENT OF CHANGES IN EQUITY FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

| | Share capital | Accumulated losses | Regulatory reserve (Other Assets) | Regulatory reserve | General Regulatory reserve | Total |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 | TZS '000 |
| **Balance as at 1 January 2017** | **20,025,247** | **(2,047,849)** | **9,022** | **3,516,723** | 453,894 | **21,957,037** |
| Capital injection | - | | - | - | - | |
| Profit for the year | - | 185,975 | - | - | - | |
| Transfer to regulatory reserve | - | 374,807 | - | (384,988) | 10,180 | |
| **Balance at 31 December 2017** | **20,025,247** | **(1,487,067)** | **9,022** | **3,131,735** | **464,074** | **22,143,011** |
| Changes on initial application of IFRS 9 | | **(905,482)** | | | | **(905,482)** |
| **Restated Balance as at 1 January 2018** | **20,025,247** | **(2,392,549)** | **9,022** | **3,131,735** | **464,074** | **21,237,529** |
| Capital injection | - | - | - | - | - | - |
| Loss for the year | - | (196,360) | - | - | - | **(196,360)** |
| Transfer to regulatory reserve | - | 763,448 | **(9,022)** | (686,762) | (67,673) | **(9)** |
| **Balance at 31 December 2018** | **20,025,247** | **(1,825,461)** | - | **2,444,973** | **396,401** | **21,041,160** |

In preparation of the yearly financial statements, consistent accounting policies have been used as those applicable to the previous year audited financial statements (Any changes during the period, shall be explained as per IAS 34 & IAS 8)

Signed By:

| | | |
|---|---|---|
| RAMA KRISHNA MARAKANI<br>Chief Executive Officer<br>Date: 29 March 2019 | AMANI MWIDETE<br>Finance Manager<br>Date: 29 March 2019 | JOHN MWAKASONDA<br>Head - Internal Audit<br>Date: 29 March 2019 |

The extract from audited financial statements of the Bank for the year ended 31 December 2018, which has been prepared in accordance to International Financial Reporting Standard (IFRS). Financial Statements were audited by Ernst & Young Certified Public Accountants and received a clean audit report

The financial statement were approved by Board of Directors and signed by:

| | | |
|---|---|---|
| **LIM TEONG LIAT** | Chairman | Date: 29 March 2019 |
| **CHARLES RWECHUNGURA** | Director | Date: 29 March 2019 |

215773901

TANGAZO

BancABC part of atlasmara

# TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA KWA UMMA

## IMETOLEWA CHINI YA KANUNI YA 7 NA YA 8 YA KANUNI ZA MABENKI NA TAASISI ZA FEDHA (UONESHAJI) YA MWAKA 2014

### TAARIFA YA UKAGUZI WA WARAKA MIZANIA KWA MWAKA 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|
| **A MALI** | | |
| 1 Fedha Taslimu | 2,895 | 3,952 |
| 2 Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 18,426 | 15,232 |
| 3 Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 40,609 | 53,184 |
| 4 Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 77,894 | 96,413 |
| 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | - | 149 |
| 6 Miamala Baina ya Matawi | - | - |
| 7 Bili Zilizoafikiwa | - | - |
| 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | - | - |
| 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | - | - |
| 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | - | - |
| 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 142,159 | 197,478 |
| | - | - |
| 12 Mali Nyingine | 21,343 | 16,701 |
| 13 Uwekezaji wa Hisa | 1,000 | 1,000 |
| 14 Akaunti za udhamini | - | - |
| 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 16,278 | 14,683 |
| **16 JUMLA YA MALI** | **320,603** | **398,793** |
| **B DHIMA** | | |
| 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 92,378 | 145,171 |
| 18 Amana za Wateja | 107,641 | 177,848 |
| 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | - | - |
| 20 Amana Maalumu | - | - |
| 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | - | - |
| 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | - | - |
| 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | - | - |
| 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | - | - |
| 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | - | - |
| 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | - | 1,551 |
| 27 Dhima Nyingine | 5,302 | 2,478 |
| 28 Madeni | 64,675 | 1,435 |
| **29 JUMLA YA DHIMA** | **269,996** | **328,484** |
| **30 MALI/(DHIMA) HALISI (16 kutoa 29)** | **50,607** | **70,309** |
| **C FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 116,014 | 116,014 |
| 32 Akiba ya Mtaji | 1,284 | 10,232 |
| 33 Mapato Yaliyobakizwa | (67,756) | (57,322) |
| 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 1,065 | 1,384 |
| 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | - | - |
| **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **50,607** | **70,309** |
| 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 2,225 | 4,524 |
| 39 Mikopo Chechefu | 20,069 | 68,353 |
| 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 17,083 | 24,866 |
| 41 Mali Nyingine Chechefu | - | - |
| **D BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (I) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 15.8% | 17.6% |
| (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 12.6% | 30.7% |
| (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 79.6% | 68.8% |
| (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 44.3% | 49.5% |
| (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 81.3% | 87.0% |
| (vi) Ongezeko la Amana | -38.1% | -6.0% |
| (vii) Ongezeko la Mali | -19.6% | -0.7% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 48,538 | 59,886 |
| 2 Gharama za Riba | (22,785) | (30,913) |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **25,752** | **28,974** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | (1,037) | - |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (3,633) | (5,397) |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba:** | **5,926** | **5,269** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 1,279 | 1,194 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 4,648 | 4,076 |
| 6.3 Gawio | - | - |
| 6.4 Mapato Mengine | - | - |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **(34,209)** | **(32,172)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (9,940) | (13,106) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | - | - |
| 7.3 Gharama Nyingine | (24,268) | (19,066) |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(7,200)** | **(3,326)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | (154) | 2,300 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(7,355)** | **(1,026)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | (320) | 1,038 |
| **12 Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(7,675)** | **13** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 157 | 152 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (780.80) | 1.29 |
| 15 | - | - |
| 16 Idadi ya Matawi | 7 | 6 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -2.00% | -0.83% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -11.91% | -5.42% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | -107.99% | -93.95% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 9.88% | 8.35% |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHIA DESEMBA 2018 (Kiasi kwa shilingi milioni

| | Mwaka wa sasa 31-Dec-18 | Mwaka uliopita 31-Dec-17 |
|---|---|---|
| **I Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (7,200) | (3,326) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | - | - |
| - Hasara Katika Mali | 7,771 | 8,201 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | 33,468 | (13,207) |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | - | - |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | (123,001) | (24,905) |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | 14,378 | 2,762 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | 1,555 | 9 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | (203) | (605) |
| - Kodi Iliyolipwa | (135) | (213) |
| - Mengineyo (bainisha) | 4,341 | 3,736 |
| **Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **(69,026)** | **(27,549)** |
| **II Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | - | - |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (5,746) | (7,079) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | - | - |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji** | **(5,746)** | **(7,079)** |
| **III Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | - | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 62,150.00 | - |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | - | 17,840.00 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | - | - |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | - | - |
| Mengineyo (bainisha) | - | - |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **62,150** | **17,840** |
| **IV Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (12,622) | (16,788) |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 85,402 | 102,190 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **72,780** | **85,402** |

### TAARIFA YA UKAGUZI YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2018

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2018** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(57,322)** | **9,119** | **1,114** | **1,384** | **70,308** |
| Marekebisho yatokanayo na IFRS 9 | - | - | (17,181) | - | - | - | **(17,181)** |
| Tengo la kodi litokanalo na IFRS 9 | - | - | 5,154 | - | - | - | **5,154** |
| **Salio la mwanzo wa mwaka lilorekebishwa** | **116,014** | **-** | **(69,349)** | **9,119** | **1,114** | **1,384** | **58,282** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (7,355) | - | - | - | **(7,355)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 9,118 | (9,118) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | (170) | - | 170 | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | (320) | **(320)** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(67,756)** | **0** | **1,284** | **1,065** | **50,607** |
| **Mwaka Uliopita 2017** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | **98,174** | **-** | **(49,717)** | **2,387** | **1,265** | **346** | **52,456** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | (1,026) | - | - | - | **(1,026)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (6,731) | 6,731 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 152 | - | (152) | - | - |
| Mengineyo | 17,840 | - | - | - | - | 1,038 | **18,878** |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **116,014** | **-** | **(57,322)** | **9,119** | **1,114** | **1,384** | **70,308** |

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi. Taarifa hizi za fedha zimekaguliwa na KPMG, Certified Public Accountants (T), na kupokea taarifa huru ya uhakiki wa ukaguzi.

Taarifa hizi za fedha ziliidhinishwa na bodi ya wakurugenzi siku ya tarehe 28 Machi 2019

I. John
(Kaimu Mkurugenzi mtendaji) Imesainiwa tarehe 11 April 2019

Mr. R. Dave
(Mkurugenzi) Imesainiwa tarehe 11 April 2019

215172602

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**VIWANJA VILIVYOPIMWA VINAUZWA** KWA BEI NAFUU Viwanja vilivyopimwa na mashamba vinavyofikika kwa urahisi. Vipo Kimbiji karibu na kwa Charle na Morris. Piga simu namba 0652 876 085 au 0745 665 955.

NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu:+255 26 2324455
Fax: +255 26 232233
Barua Pepe ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,
11/04/2019.

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya kesho JUMAMOSI tarehe **13/04/2019** kampuni ya M.M CORP LTD itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa Kutoka BAGAMOYO kuelekea DAR ES SALAAM, Gari hilo lenye namba za usajili:

   **T898 APY HORSE/ T933 AFZ TRAILER**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu -mita 22.00**
   **Upana -mita 3.50**
   **Kimo -mita 4.80**

3. Njia itakayotumika **BAGAMOYO hadi DAR ES SALAAM kupitia BAGAMOYO ROAD**. gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

115171802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**Evence Pius Moshi** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye usajili namba T196 ABU aina TOYOTA COROLA yenye chasis namba EE1013004755, engine namba 4E1300860.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

**Polisi Taarifa:**
**CHA/131/20/VOL/CHA/113**

115171902

*Kwa matangazo, madogo madogo,*

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie 0767 223 311

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# ALLEGRI AKISIFIA KIWANGO CHA AJAX



**AMSTERDAM,** Uholanzi

KOCHA wa Juventus, Massimiliano Allegri, amebainisha kwamba ameshtushwa baada ya Ajax kusawazisha haraka katika kipindi cha pili, lakini aliridhishwa na kiwango cha kikosi chake.

Juventus ilitoka sare ya kufungana bao 1-1 na Ajax kwenye mchezo wa kwanza wa robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Akicheza kwa mara ya kwanza tangu alipoifungia Bianconeri hao 'hat-trick' kwenye mchezo wa hatua ya mtoano wa timu 16 dhidi ya Atletico Madrid, Cristiano Ronaldo aliiweka mbele timu yake na kufukisha mabao 125 katika michuano hiyo.

Sasa timu hizo zinarudiana katika mchezo wa pili jijini Turin wiki ijayo na mshindi atafuzu hatua ya nusu fainali. Akizungumza mara baada ya mchezo huo,

Allegri alisema kuwa Juventus walicheza vizuri, lakini hakutarajia kama Ajax wangeweza kusawazisha bao hilo.

Alisema: "Ajax ina ubora. Walicheza kwa kutawala mchezo na hawakutaka kuacha nafasi.

"Nafikiri tulijitahidi kulinda vizuri katika mchezo na walionekana kuwa fiti kwa dakika zote 90.

"Tulikuwa kwenye wakati mgumu kwa sababu tuliruhusu bao na walionekana walikuwa na uwezo wa kuongeza bao jingine, hivyo katika mchezo ujao tutatakiwa kujilinda vizuri zaidi."



# Conte akaribia kutua Inter Milan

**MILAN,** Italia

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Antonio Conte anatarajiwa kuchukua nafasi ya ukocha katika Klabu ya Inter Milan, huku Nerazzurri wakitarajia kumfanya kuwa kocha anayelipwa ghali zaidi kwenye Ligi Kuu Italia maarufu Serie A.

Conte hajawa kwenye nafasi ya ukocha tangu alipofukuzwa na Chelsea kipindi cha majira ta joto, lakini alikuwa akihusishwa na mpango wa kuchukuliwa pale Real Madrid, kabla ya Zinedine Zidane kupewa nafasi hiyo.

Inaonyesha wazi kwamba, Inter ndio inayoonekana kuwa ina nafasi kubwa ya kumpa kibarua hicho, huku Luciano Spalletti akitajwa kuwa atatupiwa virago vyake.

Inter kwa sasa ipo nafasi ya tatu katika msimamo wa Ligi Kuu na ina nafasi ya kufuzu kucheza mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Hata hivyo, wamepitwa pointi 27 na vinara wa ligi hiyo, Juventus na inaonyesha kuwa na tofauti kubwa.

Gazeti la Daily Mail limeripoti kuwa rais, Steven Zhang amempa maelekezo Meneja Mkuu, Giuseppe Marotta kumchukua Conte kuwa kocha wa klabu hiyo wakati wowote kuanzia sasa.

Imebainisha kwamba, Conte anataka mshahara wa pauni milioni tisa baada ya kodi na kama akipewa kitita hicho atamzidi kocha wa Juve, Massimiliano Allegri ambaye kwa sasa ndiye anayelipwa mshahara mkubwa zaidi nchini Italia.

## Klopp: Bado tuna kazi kwa Porto



**LIVERPOOL,** England

KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp amesema ushindi alioupata dhidi ya Porto sio mwisho wa vita kwani kikosi chake kinatakiwa kujipanga kwa ajili ya mechi ya marudiano.

Mechi za robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya zilizochwa Jumanne usiku, Liverpool imeibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya FC Porto huku Tottenham Hotspur ikiizamisha Manchester City bao 1-0.

Mabao ya Liverpool yalifungwa na Naby Keita 1-0 dakika ya 5 na Roberto Firmino akiweka msumari wa mwisho dakika ya 61.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp baada ya mchezo huo alisema ushindi huo dhidii ya Porto sio mwisho wa vita kwani kikosi chake kinatakiwa kujipanga kwa ajili ya mechi ya marudiano.

Kocha wa FC Porto, Sergio Conceicao alisema anaamni kikosi chake kilistahili kushinda licha ya kutundikwa mabao 2-0.

Katka mchezo mwingine wa robo fainali, Spurs waliibuka kidedea baada ya kuitandika City, bao ambalo lilifungwa na Heung-Min Son dakika ya 78.

Hata hivyo Sergio Aguero alikosa penalti dakika ya 13 kipindi cha kwanza huku wachezaji wa kikosi hicho Aymeric Laporte na Riyad Mahrez wakilimwa kadi za njano kila mmoja.

HABARI MICHEZO

# Real Madrid kumuuza Bale



**MADRID,** Hispania

REAL Madrid inaweza kumwachia nyota wake Gareth Bale kuondoka klabuni hapo wakati kukiwa na uvumi kwamba raia huyo wa Wales ataondoka kwenye dimba la Bernabeu kipindi cha majira ya joto.

Wakala wa Bale, Jonathan Barnett, mapema wiki hii alibainisha kwamba, mteja wake ana furaha kubakia Madrid, huku akikanusha taarifa kuwa ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

Bale, ambaye atafikisha umri wa miaka 30 Julai mwaka huu, amekuwa akitajwa kuwa ni mmoja wa wachezaji ambao Real watawauza msimu huu.

Taarifa za hivi karibuni kutoka gazeti la AS zimebainisha kwamba, Barnett na mshauri wa Bale, Luis Alonso walikutana na mmoja wa maafisa wa hapo Bernabeu, Luis Angel Sanchez Jumatatu kwa ajili ya kujadili majaliwa yake ya mshambuliaji huyo.

Katika kikao hicho hicho, Sanchez alithibitishia Barnett na Alonso kwamba, Real Madrid wana mpango wa kumuuza Bale.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Los Blancos hao wapo tayari kumuachia Bale ili kuweza kukiimarisha kikosi chao kwa kusajili wachezaji wapya.

Gazeti la AS limezitaja Klabu za Manchester United na Bayern Munich ndio zinawania saini yake.

# SOLSKJAER: TUTAIFUNGA BARCA KWAO



**MANCHESTER,** England

MANCHESTER United inaweza kupata ushindi dhidi ya Barcelona wakiwa ugenini, kwa mujibu wa kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Barca waliifunga United 1-0 katika mechi ya kwanza ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya kwenye Uwanja wa Old Trafford, bao likifungwa dakika ya 12 baada ya mlinzi wa United, Luke Shaw kujifunga.

Mechi ya marudiano itapigwa kwenye dimban la Nou Camp, Jumanne ijayo na mshindi atafuzu kucheza hatua ya nusu fainali.

"Tumecheza na timu kubwa. Ni timu ngumu, tutaenda nyumbani kwao tukijua kuwa tutaweza kushinda kule," alisema Solskjaer wakati anazungumza na kituo televisheni cha BT Sport.

"Tunaenda kule tukiwa na kitu kimoja tu kichwani: tunatakiwa kushinda."

Katika hatua ya mtoano, United walionekana kama wameshayaaga mashindano baada ya kupoteza mabao 2-0 dhidi ya Paris St-Germain wakiwa nyumbani, lakini wakawaacha watu midomo wazi baada ya kwenda kupata ushindi wa magoli 3-1 nchini Ufaransa, na kufanikiwa kufuzu robo fainali.



# *Neville ataka Mata, Pogba waondoke Utd*

**LONDON,** England

GWIJI wa Manchester United, Garry Neville, ametoa orodha ya wachezaji wanne akidai kwamba wakiondoka hakuna hata mtu mmoja atakayeteseka.

Wakati kocha Ole Gunnar Solskjaer akijiandaa kufanya usajili mkubwa mwishoni mwa msimu huu kwa kuwanasa mastaa kibao wanaotajwa kama Kalidou Koulibaly, Jadon Sancho na Aaron Wan-Bissaka kuna wachezaji wengine wataondoka kwenye timu hiyo ya Old Trafford, lakini Neville anadai kuna mastaa wanne wakiondoka, hakuna atakayekuwa amewamisi.

"Kuna wachezaji wengi Ole atahitaji kufanya uamuzi. Ni hasara Darmian akiondoka? Sidhani kama itakuwa mwisho wa dunia. Ni pigo Antonio Valencia akiondoka? Anasumbuliwa sana na majeruhi, nadhani United inahitaji beki mpya wa kulia. Ashley Young, ana nafuu na yupo kwa miezi mingine 12," alisema Neville.

"Nadhani Mata (Juan) na (Ander) Herrera wanawindwa na timu nyingine. Nadhani hao ni wachezaji wanaotakiwa na timu nyingine, kwangu mimi sioni kama itakuwa mwisho wa dunia kama wote wataondoka."

Wakati huo huo, wachezaji wa United wameripotiwa kwamba watakatwa mishahara yao kwa asilimia 25 kila mmoja kama timu hiyo itashindwa kumaliza katika "Top Four" ili kufuzu Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

Taarifa za kutoka Old Trafford zinafichua hivyo, huku kukiwa na madai kwamba mambo kama hayo ndiyo yatakayomfanya "supastaa" Paul Pogba kukusanya virago vyake na kuondoka kuliko kubaki kwenye timu hiyo akatwe mshahara na timu ikiwa imekosa kufuzu kucheza michuano ya Ulaya msimu ujao.

# DONDOO Z KA
## MAGAZETI Y AYA




# VIGOGO LA LIGA, EPL WAMGOMBEA NIGUEZ

## ●●● Aeleza hana furaha kubakia Atletico...

**MADRID,** Hispania

ATLETICO Madrid inatarajia kukutana na upinzani katika kufanikisha mchakato wa kumbakisha kiungo wake, Saul Niguez, ambaye anawaniwa na klabu mbalimbali za barani Ulaya.

**Klabu za Manchester City, Manchester United na Barcelona zote zimetajwa kuonyesha nia ya kumhitaji kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Hispania, gazeti ya AS limeandika.**

Gazeti hilo limeendelea kusema kuwa kiungo huyo hana furaha kutokana na tofauti ya kiwango cha mshahara anacholipwa yeye na mshambuliaji nyota wa timu yake, Antoine Griezmann.

Mwaka juzi, Niguez alisaini mkataba mpya wa miaka tisa wa kuendelea kuitumikia timu hiyo katika mkataba huo inaonyesha kwamba anaweza kuondoka kwenye klabu hiyo endapo timu inayomtaka itatoa kiasi cha pauni milioni 129.

Vigogo hao wa Hispania wanajiandaa kumpa ofa mpya kiungo huyo endapo atafikia uamuzi wa kubakia kwenye timu hiyo yenye makazi yake Wanda Metropolitano.

Katika kipindi cha majira ya joto mwaka jana, mshambuliaji nyota, Griezmann alisaini mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia Atletico Madrid ambao unamfanya alipwe mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki baada ya kukubali kubaki klabuni hapo.

Mfaransa huyo alikubali kubakia Atletico Madrid ndani ya wiki moja baada ya kukataa ofa ya kujiunga na Barcelona.

Wakati huo huo, Niguez, anaamini kuwa anaweza kulipwa mshahara wa pauni 90,000 kwa wiki.

Imeelezwa kuwa nyota huyo mwenye umri wa miaka 24 amebadilisha wakala wake na sasa atakuwa chini ya Kampuni ya Stellar, ambao pia ni washauri wa mshambuliaji, Gareth Bale.

Kwa kipindi fulani msimu huu, Niguez alibadilishiwa majukumu na kucheza nafasi ya beki wa kushoto kutokana na wachezaji, Filipe Luiz na Lucas Hernandez kuwa majeruhi.

Kwa ujumla, Niguez ameichezea Atletico Madrid mechi 38 katika mashindano mbalimbali msimu huu na kufanikiwa kufunga mabao sita.

## ZISIKUPITE

### POGBA, SOLSKJAER KUMEKUCHA

UHUSIANO kati ya Paul Pogba na Kocha wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer umeanza kuingia dosari na kiungo huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 26 anajiandaa kujiunga na Real Madrid. ***(Le Parisien via AS)***

### FERNANDES KUTUA UNITED

MANCHESTER United imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Sporting Lisbon na Timu ya Taifa ya Ureno, Bruno Fernandes ambaye ana umri wa miaka 24. ***(A Bola - in Portuguese)***

### BALE KUONDOKA MADRID

IMEELEZWA kuwa mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale (29), hayuko katika mipango ya msimu ujao ya Real Madrid na klabu hiyo ya Hispania inatarajia kumruhusu kuchagua timu ya kujiunga nayo wakati tayari Manchester United na Bayern Munich zimeonyesha nia ya kumhitaji. ***(AS)***

### MATA KUINGIA SOKONI

KIUNGO wa United, Juan Mata (30), anajiandaa kufanya uamuzi kuhusu hatima yake ndani ya Old Trafford, huku Mhispania huyo akipokea ofa kutoka klabu mbalimbali. ***(Manchester Evening News)***

### HAZARD AITAMANI MADRID

MSHAMBULIAJI wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard (28) anaamini kuwa 'huu ndio muda sahihi au ndoto zake kupotea' za kujiunga na Real Madrid. ***(Goal)***

### DRINKWATER MAMBO MAGUMU

KIUNGO raia wa England, Danny Drinkwater (29), amesema hana nafasi katika kikosi cha Stamford Bridge ambacho kiko chini ya Maurizio Sarri. ***(Guardian)***

### LIVERPOOL, EVERTON VITANI

LIVERPOOL imeweka wazi nia yake ya kumsajili mshambuliaji wa Ajax, David Neres (22), huku watani zao kutoka Merseyside, klabu ya Everton nao wameonyesha kumhitaji Mbrazili huyo. ***(Mirror)***

### CLYNE ANUKIA HAMMERS

WEST Ham inaongoza katika vita ya kuwania saini ya beki wa kulia wa Liverpool, Nathaniel Clyne (28), ambaye kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu ya Bournemouth. ***(Football Insider)***

### NEIL KUTUA BROM

WEST Brom iko tayari kufanya mazungumzo na Kocha wa Preston, Alex Neil ili kumshawishi atue katika klabu yao. ***(Telegraph)***

### ERRAS KUHAMIA ENGLAND

NEWCASTLE imefanya mazungumzo na Nuremburg kwa ajili ya kumsajili kiungo wake Mjerumani, Patrick Erras ambaye ana umri wa miaka 24. ***(Bild via Newcastle Chronicle)***

### NIASSE ATAKIWA BESIKTAS

KLABU ya Besiktas ya Uturuki imeweka wazi nia yake ya kumsajili straika wa Everton na Timu ya Taifa ya Senegal, Oumar Niasse (28), ambaye kwa sasa yuko Cardiff kwa mkopo. ***(Fanatik - in Turkish)***

## HABARI MICHEZO

# Malindi yazinduka Ligi Kuu Z'bar

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Malindi imerejea katika mbio za ubingwa baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya KMKM katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar iliyochezwa juzi kwenye Uwanja wa Amaan, Visiwani hapa.

Kutokana na ushindi huo, Malindi imepanda hadi katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 19 huku KMKM yenye pointi 65 wakifuatia.

Bao pekee katika mchezo huo ambao ulihudhuriwa na idadi kubwa ya mashabiki lilifungwa na Ibrahim Abdalla dakika ya 24 baada ya kutokea vuta nikuvute katika lango la mabaharia wa KMKM.

Mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Mau iliwakutanisha Polisi ambao walipata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Chuoni na kufikisha pointi 46 wakati Jamuhuri ilitoka sare ya bao 1-1 na Kizimbani katika mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Gombani.

Mwenge yenye ilifanikiwa kutoka ushindi mnono wa mabao 3-0 dhidi ya Hard Rock.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa KVZ kuikaribisha Zimamoto huku Polisi wakivaana na Mlandege wakati Chuoni watawavaa Malindi.

Wakati huo huo, Kamati ya Mashindano ya Chama cha Soka Zanzibar (ZFA) imeirejesha timu ya Ujamaa katika hatua ya Sita Bora ya Ligi Daraja la Pili Taifa baada ya kuitupa rufaa iliyowasilishwa dhidi ya timu hiyo.

### MSIMAMO LIGI KUU BARA



| | P | W | D | L | F | A | PTS |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. Yanga | 30 | 22 | 5 | 3 | 48 | 20 | 71 |
| 2. Azam | 30 | 18 | 9 | 3 | 48 | 18 | 63 |
| 3. Simba | 22 | 18 | 3 | 1 | 48 | 7 | 57 |
| 4. Lipuli | 33 | 12 | 12 | 9 | 30 | 28 | 48 |
| 5. Mtibwa Sugar | 31 | 13 | 6 | 12 | 32 | 24 | 45 |
| 6. Kinondoni MC | 32 | 9 | 15 | 8 | 32 | 23 | 42 |
| 7. TZ Prisons | 32 | 10 | 12 | 10 | 26 | 25 | 42 |
| 8. Coastal Union | 32 | 9 | 14 | 9 | 28 | 31 | 41 |
| 9. Mbeya City | 31 | 11 | 7 | 13 | 31 | 33 | 40 |
| 10. Singida United | 33 | 10 | 10 | 13 | 24 | 32 | 40 |
| 11. Ndanda | 31 | 10 | 10 | 11 | 21 | 30 | 40 |
| 12. JKT Tanzania | 32 | 9 | 12 | 11 | 20 | 27 | 39 |
| 13. Stand Utd | 33 | 10 | 6 | 16 | 30 | 41 | 39 |
| 14. Mwadui | 33 | 10 | 7 | 16 | 37 | 43 | 37 |
| 15. Alliance | 32 | 9 | 10 | 13 | 23 | 33 | 37 |
| 16. Mbao | 33 | 9 | 11 | 13 | 19 | 33 | 37 |
| 17. Kagera Sugar | 31 | 8 | 12 | 11 | 24 | 31 | 36 |
| 18. Ruvu Shooting | 33 | 8 | 12 | 13 | 28 | 39 | 36 |
| 19. Biashara Utd | 31 | 8 | 10 | 13 | 22 | 29 | 34 |
| 20. African Lyon | 33 | 4 | 10 | 19 | 19 | 43 | 22 |

# DSTV YAJITOSA KUIBEBA SERENGETI BOYS U-17

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha kuwa Tanzania inaendeleza wimbi la ushindi kwenye mashindano ya kimataifa, DSTV imesema kuwa itarusha mubashara mechi za Fainali za vijana za Afrika za umri chini ya miaka 17 (AFCON U-17) ili kuongeza hamasa ya ushindi kwa timu mwenyeji, Serengeti Boys.

**Akizungumza katika hafla ya kuzindua kampeni hiyo ya DStv ijulikanayo kama 'DStv Inogile', Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Baraka Shelukindo, alisema kuwa katika kuunga mkono kampeni ya kuifanya nchi yetu ifanye vizuri katika michezo mbalimbali, DStv itarusha fainali hizo katika kifurushi cha chini cha Sh. 19,000.**

Shelukindo alisema kuwa wanaamini uamuzi huo utawawezesha Watanzania wengi kushuhudia timu yao ikicheza na kuwaongezea ari ya kuwaunga mkono kwa hali na mali.

"Hili ni suala la kitaifa, hivyo tunataka Watanzania popote walipo waweze kushuhudia timu yetu ikipambana kwa ajili ya sifa ya nchi yetu" alisema Shelukindo.

Aliongeza kuwa DStv inaonekana kote barani Afrika na hivyo kitendo cha kuonyesha michuano hiyo ambayo inafanyika kwa mara ya kwanza hapa nchini, kitaufanya ulimwengu kushuhudia mashindano hayo na pia kutangaza jina la Tanzania.

"Kwa michuano hii kuonekana DStv, ina maana kubwa sana kwa nchi yetu, hii ni njia moja wapo pia ya kuitangaza nchi yetu Afrika na dunia nzima itambue kuwa na sisi tuna uwezo siyo tu wa kuandaa mashindano haya bali pia wa kuyaonyesha," alisema Shelukindo.

Naye Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Omar Singo, alisema kuwa kitendo cha DStv kuonyesha mubashara michuano hiyo ni cha kupongezwa na ni sifa kwa nchi.

"Serikali inathamini sana michango ya aina mbalimbali inayotolewa na wadau kama DStv katika kukuza michezo hapa nchini. Tunaamini kuwa kwa ushirikiano huu, mafanikio haya ambayo tumeanza kuyapata yataendelea na tutafikia azma yetu ya kuwa taifa kubwa kimichezo duniani," alisema Singo

Amri Kiemba, akizungumza kwa niaba ya wachezaji wenzake waliowahi kuichezea Timu ya Taifa (Taifa Stars) ambao walishiriki katika hafla hiyo, alisema ni wajibu wa Watanzania kuonyesha uzalendo kwa nchi yao kupata heshima ya kuwa mwenyeji wa fainali hizo.

Kiemba alisema kuwa Serengeti Boys inatakiwa kuungwa mkono ili ifanye vizuri katika michuano hiyo na kupata tiketi ya kwenda kwenye mashindano ya Kombe la Dunia la Vijana yatakayochezwa baadaye mwaka huu nchini Brazil.




Mkurugenzi wa Maendeleo wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Omar Singo (aliyevaa koti) akimkabidhi mpira mchezaji wa zamani wa Taifa Stars, Amri Kiemba, wakati wa uzinduzi wa kampeni maalum ya 'DStv Inogile' ambayo inalenga kuhamasisha umma kuishangilia Serengeti Boys ambayo inashiriki Fainali za Vijana za Afrika (AFCON U-17) zinazotarajiwa kuanza Jumapili hapa nchini. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Ngorongoro Race mambo yameiva

**Na Renatha Msungu**

FOMU kwa ajili ya kushiriki mbio za Ngorongoro (Ngorongoro Race 2019) mwaka huu zinatarajiwa kuanza kutolewa kuanzia leo mjini Karatu, Arusha imeelezwa.

Mbio hizo zitafanyika Aprili 20 mwaka huu kwa kushirikisha wanariadha kutoka sehemu mbalimbali nchini.

Mratibu wa mbio hizo, Meta Petro, alisema jana kuwa tayari baadhi ya wanariadha nyota wa hapa nchini na wengine kutoka Kenya, wamethibitisha kushiriki katika mbio hizo zinazofanyika kila mwaka.

Petro alisema kuwa matarajio yake ni kuona wanariadha wengi wanajiandikisha kwa ajili ya kushiriki mbio hizo, ambazo mwaka huu zimeboresha.

Alisema kuwa wameamua kuweka kituo kimoja cha usajili wa wanariadha ili kuhakikisha kila mwanariadha anayenunua fomu anapewa risiti na fedha stahiki inaingia katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia mashine ya kielectoniki wanayotumia katika mchakato huo.

"Tutaanza usajili Ijumaa na kila mwanariadha atakayenunua fomu atapewa risiti ya TRA ili Serikali ipate fedha zake stahiki kwa ajili ya maendeleo ya taifa, "alisema Petro, ambaye ni kocha wa Timu ya Taifa iliyoshiriki mbio za dunia za nyika.

Aliongeza kuwa fomu kwa wanariadha wanaotaka kushiriki mbio za kilomita 21 zitatolewa kwa gharama ya Sh. 20,000 wakati zile za kilomita tano kila moja itauzwa kwa Sh. 10,000 na Sh. 5,000 ni kwa wale watakaokimbia mbio za kilomita 2.5 ambazo ni maalumu kwa watoto.

Alitaja zawadi kwa mshindi wa kwanza kwa mbio za nusu marathoni itakuwa ni Sh. milioni moja, mshindi wa pili ataondoka na Sh. 500,000 wakati mshindi watatu atapewa Sh. 200,000 huku mshindi wa nne akipewa Sh. 100,000.

Naye Kaimu Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro, Joyce Mgaya, alisema washiriki 100 wa kwanza wa mbio za kilomita 21 watapata ofa ya kutembelea hifadhi hiyo katika siku ya sikukuu ya Pasaka.

# Michezo

Ijumaa Aprili 12, 2019

Nipashe




Vigogo Ulaya wamgombea Niguez

UKURASA 30



Beki wa Manchester United, Chris Smalling (kulia), akipambana kumkaba straika wa Barcelona, Luis Suarez katika mechi ya kwanza ya hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyochezwa juzi usiku, kwenye Uwanja wa Old Trafford. Barca ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Yanga SC yazidi kutakata Bara

## ●●● Yaichapa Kagera Sugar 3-2, Yondani akionyeshwa kadi nyekundu...

**Na Adam Fungamwango**

IKITOKEA nyuma, Yanga imeendelea kujiimarisha katika kinyang'anyiro cha kuusaka ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara baada ya kuifunga Kagera Sugar mabao 3-2 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM, Kirumba jijini Mwanza.

**Kutokana na ushindi huo, Yanga ambayo imecheza mechi 31 sasa imefikisha pointi 74 wakati Kagera Sugar yenye 36 bado imeshindwa kujinasua kutoka katika janga la kushuka daraja, ikiwa katika nafasi ya tatu kutoka chini ya msimamo wa ligi hiyo.**

Iliwachukua dakika 30 Kagera Sugar wanaofundishwa na Mecky Maxime kuandika bao la kwanza lililofungwa kwa kichwa kupitia kwa straika wake mkongwe, Paul Ngwai baada ya kuunganisha mpira wa kona iliyopigwa upande wa kulia mwa goli la Yanga.

Dakika tano baadaye, Kassim Khamisi ambaye alikuwa na matukio mengi uwanjani, alijifunga mwenyewe katika harakati za kutaka kuokoa mpira katika lango lake na kuwafanya Yanga wapate nguvu na kuongeza mashabulizi.

Mshambuliaji raia wa Kongo, Heritier Makambo alifunga bao la pili katika mchezo huo likiwa ni la 15 kwenye orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu msimu huu.

Alilifunga kwa kichwa dakika ya ya pili tu baada ya kuanza kwa kipindi cha pili, kufuatia pasi ndefu ya beki mkongwe, Kelvin Yondani.

Khamisi alisawazisha makosa yake ya kujifunga, alipoipatia Kagera bao la pili dakika ya 57, baada ya kupiga krosi iliyokwenda moja kwa moja wavuni na kumuacha kipa wa Yanga Klaus Kindoki akigaagaa bila mafanikio.

Thabani Kamusoko aliihakikisha Yanga kubaki na pointi zote tatu kwenye mechi hiyo dakika ya 71, alipoandikisha bao la tatu kwa mkwaju wa faulo karibu kabisa na eneo la hatari.

Hata hivyo, nahodha wa zamani wa timu hiyo, Kelvin Yondani alionyeshwa kadi nyekundu dakika ya 82, baada ya kumpiga kiwiko kwa makusudi, Kassim.

Kutokana na kadi hiyo nyekundu, Yondani sasa atakosa mechi tatu na zitakuwa ni dhidi ya Mtibwa Sugar, Azam FC, zote za Ligi Kuu na moja ya hatua ya nusu fainali ya Kombe la FA dhidi ya Lipuli FC ya Iringa.

# Simba yaenda Kongo kibabe

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI wawalikishi pekee wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Simba wakiondoka nchini leo asubuhi kuelekea Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Aussems, amesema kuwa kikosi chake kinakwenda Lubumbashi huku kikiogopewa.

Simba inatarajia kuwavaa wenyeji wao, TP Mazembe katika mchezo wa marudiano wa hatua ya robo fainali ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa kesho kwenye Uwanja wa Lubumbashi.

Aussems aliliambia gazeti hili kuwa hatua ambayo Simba imefika msimu huu ni ya kujivunia na bado wana nafasi ya kufanya vizuri na kusonga mbele katika mashindano hayo ya kimataifa yanayofanyika kila mwaka.

Mbelgiji huyo alisema kuwa wanakwenda Lubumbashi kuendelea na kazi waliyoianza katika mchezo wa kwanza na kamwe hawafikirii kucheza kwa mfumo wa "kupaki basi".

Naye meneja wa timu hiyo, Patrick Rweyemamu, alisema kuwa kikosi chao kitaondoka nchini saa mbili asubuhi, kikiwa na wachezaji 18.

"Leo (jana) tumefanya mazoezi asubuhi tu, mchana wachezaji wamepata muda wa kupumzika na jioni (jana jioni) tutakuwa na kikao, hapo ndio tutajua wachezaji watakaosafiri, ila iko wazi Wawa (Pascal) yeye alishajulikana mapema hayuko katika programu ya mchezo wa Jumamosi," alisema meneja huyo.

# Wapinzani wa Stars AFCON kujulikana leo

**Na Mwandishi Wetu**

WAPINZANI wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars) katika Fainali za Kombe la Afrika zitakazochezwa Juni mwaka huu, wanatarajia kujulikana rasmi leo baada ya kufanyika kwa droo ya mashindano hayo huko jijini Cairo, Misri.

Fainali za Afrika (AFCON 2019) zinatarajiwa kufanyika kuanzia Juni 21 hadi Julai 13 mwaka huu na zitashirikisha timu 24.

Hata hivyo, Jumapili iliyopita, Shirikisho la Soka Afrika (CAF) lilitangaza makundi ya awali ya timu zote zilizofuzu kucheza fainali hizo huku Morocco, Nigeria na Algeria zikiwekwa katika kundi moja.

Kundi la kwanza: Misri, Ghana, Tunisia, Ivory Coast, Cameroon na Senegal wakati Morocco, Nigeria, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Algeria, Mali na Guinea wako katika kundi la pili huku kundi la tatu likiundwa na Uganda, Afrika Kusini, Guinea-Bissau, Zimbabwe, Angola na Burundi.

Kundi la nne na la mwisho linaundwa na Mauritania, Namibia, Benin, Kenya, Tanzania na Madagascar.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >